ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni

53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nane - Tarehe 30 Januari, 2015

(Kikao kilianza Saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pamdu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mradi wa Maridhiano namba moja ya mwaka 1999 na kutunga sheria mpya kwa ajili ya kuanzisha na kuendesha mashirikiano baina ya sekta ya umma na binafsi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Usajili na Usimamizi wa Wasanii na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Vile vile Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Kamisheni ya Ardhi na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Kuanzishwa Baraza la Sensa ya Filamu ya Utamaduni Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 72

Nani Mmiliki wa Pango la Watoro

Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Aliuliza:-

Kwa kuwa pango la Watoro ni sehemu moja ya historia ambapo wageni kutoka ndani na nje ya nchi hupenda kutembelea pango hiyo. Na kwa kuwa muwekezaji wa Manta Resort amelihodhi pango hilo na kulipanga kama ni sehemu yake ya hoteli na kufanya kivutio cha hoteli hiyo.

Je, eneo hilo la pango bado ni mali ya Serikali au aliuziwa muwekezaji huyo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 72 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Pango la Watoro lililoko kwenye ufukwe mkabala na Hoteli ya Manta Resort ni mali ya Serikali, linatunzwa na kushughulikiwa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale na wala hakuuziwa Mwelekezaji wa Hoteli ya Manta Resort.

Mhe. Spika, si kweli kwamba pango hilo limehodhiwa na Mwekezaji huyo na kulipanga kama ni sehemu yake na kufanya kivutio cha hoteli yake.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mhe. Waziri alisema kuwa sio kweli kuwa Pango hilo limehodhiwa na Mwekezaji wa hoteli hiyo. Lakini ni kwa sababu gani inayompelekea mwekezaji huyo kuifunga njia ambayo wanapita watalii wa ndani, kwenda kuangalia Pango hilo na watu kulazimika kupita njia ilioko kwenye hoteli yake, ni kwa sababu gani kama sio lake.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nadhani Mhe. Mwakilishi hajafanya utafiti mzuri sana. Taarifa niliyonayo ni kwamba Pango lile zaidi linatumiwa na wananchi wa maeneo yale kwa shughuli zao za kijadi, na kuna njia maalum imetolewa kutoka nje ya hoteli moja kwa moja mpaka kwenye Pango lenyewe. wananchi wakati wowote wanakwenda pale wakifanya shughuli zao za kijadi kama zamani bila ya usumbufu wowote. Wakati wowote Mhe. Mwakilishi akitaka twende pamoja nikamuoneshe hiyo njia, niko tayari hata baada ya kikao hiki tukijaaliwa twende nikamuoneshe kwamba wananchi wanapita njia hii, wakienda kufanya shughuli zao mbali mbali za kimila.

UTARATIBU

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Spika, mimi suala hilo Mhe. Waziri akaangalie kitabu cha ripoti ya ukaguzi yakinifu ya PAC, na kwa ruhusa yako Mhe. Spika, kama utaniruhusu naomba ninukuu hiki kitabu.

Mhe. Spika, kitabu hiki kinaeleza hivi;

Kwanza hapa juu nisome hii *heading*, Pango ya Watoro Kigomasha.

> " Ukaguzi umebaini kwamba eneo hili halitumiki kwa shughuli za kitalii kutokana na vikwazo mbali mbali vinavyowekwa na Mwekezaji anayemiliki hoteli ya Manta Resort. Aidha, wageni mbali mbali wa nje na wa ndani wenye lengo la kutembelea Pango hilo, wanalazimika kupita ndani ya hoteli hiyo, kwani njia ya kuelekea katika Pango imefungwa na Mwekezaji huyo.
>
> Kutokana na hali hiyo Pango hili limekuwa kama ni sehemu ya hoteli hiyo na linatumika kama ni kivutio cha watalii wanaofika katika hoteli hiyo na kuikosesha serikali mapato yanayotokana na eneo hilo la kihistoria". Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Bikame Yussuf nakupa taarifa hiyo ili uifanyie kazi vizuri uone kauli yako ulioitoa hapa kama iko sahihi au la.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa umakini wake wa hali ya juu. Hii wiki haijatimia humu ndani alitoa ahadi kuwa ataleta mswada unaohusu mambo ya filamu. Alichokifanya ni kitendo cha kiungwana, suala hili kwa Waheshimiwa Wawakilishi hasa wananchi wa Jimbo la Muyuni ni kilio kikubwa na Mwakilishi wa Kiembe Samaki katika jimbo lake.

Kwa hivyo, nimpongeze sana Waswahili wanasema "mpe mtu haki yake kabla jasho halijakauka". Kwa hivyo Mhe. Waziri nikushukuru sana kwa umakini wako. Mimi nilikuwa nataka kujua Pango hilo liko katika jimbo gani, na wananchi wanafaidika kiasi gani na Pango hilo kuwemo katika kijiji chao.

Mhe. Spika: Hebu lifafanuwe swali lako kwa uwazi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Pango hilo liko katika jimbo gani na wananchi wanafaidika na neema hiyo iliyoko kijijini kwao kwa kiasi gani? Yaani faida wanayoipata wananchi hao.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, Pango hili liko katika Shehia ya Makangale katika Jimbo la Konde. Wananchi wanavyofaidika kama nilivyosema awali, kwamba hili ni Pango ambalo wenyewe wanalitumia kwa shughuli zao za kijadi na wanalitumia kwa shughuli hizo. Kama nilivyosema awali kwamba njia imewekwa vizuri, na sio vizuri hata kidogo kuchukua ripoti za *CAG* na kuzitungia maswali. Ni vizuri labda baada ya ripoti ya *PAC* ambayo imekwenda katika eneo hili wakathibitisha kwamba Pango linatumiwa na wananchi na liko huru kutumiwa na sehemu ya Mwekezeji.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, bado nasisitiza kwamba Pango hili liko huru kwa wananchi, *PAC* imekwenda, Mhe. Makamu Mwenyekiti Mhe. Fatma Mbarouk yupo pale wamekwenda na wamethibitisha hilo. Kwa hivyo, sio vizuri

kuchukua ripoti za *CAG* ikawa ndio msingi wa kutuulizia maswali katika Baraza hili, na ndio maana ripoti za *CAG* zinakuja hapa kwanza kuthibitishwa na kamati yako Mhe. Spika, ya *PAC*. (*Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu cha 37 ndicho kilichonisimamisha hapa. Waziri au Mjumbe yeyote anauliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi, isipokuwa kwamba swali aliloulizwa waziri mmoja linaweza kujibiwa kwa waziri mwengine. Nauliza wananchi wa jimbo lile wamenufaika vipi na Pango lile, neema iliyokuwepo.

Mhe. Spika: Fafanua zaidi Mhe. Waziri, namna wananchi wanavyofaidika na Pango lile.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nilivyojibu ni kwamba Pango lile tokea awali mafanikio yake kwa wananchi ni kwamba wanalitumia kwa shughuli zao za kimila na kijadi. Kwa hivyo, bado manufaa hayo yapo na wananchi wanaendelea kulitumia. Kwa hivyo, manufaa makubwa ya Pango lile kwa wanachi wa Jimbo la Konge na hasa wa Shehia ya Makangale, ni kwamba bado limeachwa kwa ajili ya shughuli zao ambazo walikuwa wanazitumia tokea zamani.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Wawekezaji wengi wanaomiliki mahoteli wamekuwa na tabia ya kutumia Mapango au *natural resources* za serikali ili kutangazia huduma yao ya utalii.

Mhe. Spika, ukiangalia kwenye *website* ya hoteli mbali mbali ikiwemo hiyo Manta Resort, wamekuwa wakitangazia hoteli yao kwa sehemu ya Pango lile. Ni kwa nini huanzishi utaratibu mzuri ili mapato yanayotokana na vyanzo vyetu vya asili yakachangia uchumi wa nchi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli kwamba wawekezaji wengi katika nchi yetu wanatumia fursa mbali mbali zilizopo karibu na hoteli zao, kuongezea kama ni vivutio vya hoteli zao, hilo ni jambo ambalo linatumika sana. Hoteli ya Manta Resort kwa siku za karibuni zaidi imekuwa ikitumia kivutio cha chumba chini ya bahari kama ni kivutio cha hoteli yake. Imekuwa ikijitangaza hivyo sana na kwa kweli imekuwa ikipata wageni wengi zaidi kuliko Pango la Watoro. Hata hivyo, ushauri wake tumeuchukua na tutaufanyia kazi.

Nam. 122

Kujaa Maji Katika Eneo la Abiria la Uwanja wa Ndege Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kwanza nichukuwe fursa hii kutoa pole kwa Mhe. Waziri Juma Duni, kwa kufiwa na ndugu yake Mwadini Juma Mjaja kilichotokea jana usiku, kwa taarifa hii niliyokuwanayo. Sasa kama serikali itakuwa na majibu sawa, na kama itakuwa hamna basi nitaliwacha suala hili kutokana na kifo huwezi kukizuwia. Mimi sijui saa ngapi nitahitajika, kwa hivyo naweza kuliwacha mpaka serikali itakapokuwa tayari.

Mhe. Spika: Hebu Mhe. Jaku Hashim, naona kama kuna taarifa imechanganyika. Hebu nipeni ufafanuzi wa hili jambo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwanza nitowe pole kwa Mhe. Waziri Juma Duni Haji, maarufu Babu, kwa kifo cha ndugu yake kilichotokea usiku. Kibinadamu na kiungwana siwezi kulazimisha swali hili lijibiwe, kifo hakina saa, hakina dakika. Mhe. Naibu Waziri vile vile sababu aliyokuwanayo mimi naijua, kwa hivyo siwezi kulazimisha hili swali lijibiwe. Kwa busara sifikiri.

Naambiwa hapa jibu lipo Mhe. Spika, naomba serikali itowe jawabu sasa hivi. *(Makofi)*

Hivi karibuni uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar umejaa maji ya mvua eneo la mbele ya Abiria wanaoteremka wakitoka safari na kusababisha watalii na wananchi kupandisha suruali zao mpaka kwenye sehemu nisizoweza kuzitaja kwenye chombo hichi.

(a) Je, Serikali inalijua tatizo hili lililotokea hivi karibuni na hatua gani imezichukua.

(b) Je, kitendo hicho siyo cha aibu kwa Serikali yetu na kuivunjia hadhi na sifa ya Zanzibar.

(c) Je, fedha zinazopatikana pale kwenye makusanyo mengi yakiwemo *Parking* za magari na Ofisi zilizojengwa majuzi na kukodishwa kwa watu mbali mbali zinatumika VIP au ni makosa kuzitumia katika matengenezo ya mitaro ya maji.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: (Kny: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, nakushukuru. Mkono wa pole wa Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano tumeupokea kutoka kwa Mhe. Mwakilishi. Naomba kumjibu Mhe.Mwakilishi swali lake Nam. 122 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, hivi karibuni uwanja wa ndege wa kimataifa Zanzibar umejaa maji ya mvua eneo la mbele la abiria wanaoteremka wakitoka safari, linalosababisha watalii na wananchi kupandisha suruali zao mpaka kwenye sehemu nisizoweza kuzitaja kwenye chombo hiki.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa maelezo ya swali hili kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, serikali inalijua tatizo hilo lililotokea hivi karibuni ambalo lilitokana na kuzidiwa kwa miundombinu ya kupitisha maji machafu. Miundombinu iliyopo ni ya zamani na imeshachakaa na uwezo wake wa kufanyakazi umekuwa ni mdogo.

Hatua iliyochukuliwa ni kumwita mtaalamu kutoka Kampuni ya SOGEA SATOM kuja kufanya vipimo na kutayarisha michoro ya kuifanyia marekebisho miundombinu hiyo na kuifanya iwe na uwezo wa kupitisha maji mengi zaidi kwa wakati mmoja. Marekebisho hayo yatapelekea kuondoa tatizo liliopo.

(b) Mhe. Spika, matokeo ya majanga, mvua za ghafla hazitabiriki. Serikali siku zote inaendela kuongeza na kuboresha huduma ili changamoto zote ikiwemo hadhi ya nchi yetu iweze kuboreka zaidi.

(c) Mhe. Spika, fedha zinazopatikana kutokana na makusanyo hayo zinagawiwa katika makundi mawili. Kundi la kwanza zinatumika kwa ajili ya kuharamia huduma za uendeshaji wa Viwanja vya Ndege na kundi la pili zinatumika kwa ajili ya maendeleo ya uwanja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri makini, naomba kumuuliza maswali mawili madogo tu ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa tatizo hilo limejitokeza mbele ya sura ya nchi, serikali inatumia muda gani kuliondoa hasa kwa kuzingatia wageni wanaoingia kutoka nje wanachangia pato katika uwanja ule.

(b) inakuwaje uwanja ujae maji wakati mradi kabla ujenzi unaanza mipango yote ikiwemo sehemu ya maji machafu na vile vile sababu gani mwanamme pale kupekuliwa na mwanamke uwanje ule wa kimaitaifa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nikushukuru na naomba nimjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub maswali yake mawili ya nyongeza kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali lake la msingi ni kwamba mara baada ya kutokea tatizo hilo mtaalamu wa Kampuni ya *SOGEA SATOM* ameitwa na analifanyia kazi suala hili. Sasa hili ni suala la kiufundi linahitaji *design* na pia mambo mengine, naomba Mhe. Mwakilishi aipe muda wizara ishirikiane na mtaalamu, lakini ni jambo

ambalo kwa kweli tumeliona na Serikali tutahakikisha kwamba tutajitahidi kuweka miundombinu imara na mikubwa zaidi ya kisasa, ili tatizo hilo lisitokee tena.

Kuhusu suala hili limetokea kwamba inakuwaje, ni kwa sababu kama unavyojua kwamba uwanja wa ndege bado umo katika marekebisho, kuna miradi mitatu inaendelea sasa hivi ya jengo, ya *apron* na *take away*. Kwa hivyo yote haya ni miradi ambayo inaendelea hivi sasa. Miradi yote ikikamilika Mhe. Spika, yote hii mitatu Serikali itahakikisha kwamba kiwanja chetu cha ndege kiko katika hadhi kubwa zaidi.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, ninashukuru kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa wataalamu wetu wengi wa majengi mbali mbali ya Serikali ya Mapinduzi wanajenga majengo ambayo hayafikii kiwango ikiwa ni pamoja na kuchelewa kwa maji hapo uwanja wa ndege. Kwa mfano kuna majengo mbali mbali ya skuli zimejengwa vizuri tu lakini zimefikia kiwango ambacho siyo sahihi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha hali hii ili isipate gharama kuendelea kila siku katika majengo mapya.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ninashukuru na ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, shughuli za ujenzi na uhandisi katika nchi yoyote ile ni shughuli ambazo mara kwa mara zinahitaji kufanyiwa marekebisho kulingana na maendeleo husika ya nchi hiyo. Nchi yetu katika siku za karibuni sote tunaelewa kwamba imeanza kufanya mapitio ya sheria mbali mbali ili kuona kwamba utaratibu wa ujenzi katika nchi yetu unakwenda sambamba na maendeleo yanayokuja.

Kwa hivyo udhaifu ambao ameutaja Mhe. Mwakilishi Serikali umeuona na tunaufanyia kazi na ndiyo maana ukaona kwamba Serikali inaleta Miswada mingi, hata Wizara ya Ujenzi kuna Miswada ambayo inakuja ameshaanza kuisoma kwa mara ya kwanza Mheshimiwa Waziri husika, ameweka hati mezani kuona kwamba tunafanya marekebisho katika suala zima hili la ujenzi na miundombinu kwenye nchi yetu.

Na. 123

Msongamano wa Magari Kutokana na Kupelekwa
Makontena katika Eneo la Bwawani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Shirika la Bandari la Zanzibar hivi sasa limeanzisha kutoa makontena kupeleka katika eneo la Bwawani wakati wa asubuhi na mchana na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaoelekea kufanya majukumu yao yao kazi, kutokana na msongamano mkubwa wa foleni ya magari kusimama kutokana na gari zao kubeba makontena kupeleka hapo Bwawani.

a) Kwa nini Shirika la Bandari halijapanga kama nchi nyengine zinazofanya kazi kwa utaratibu maalum kazi hizo kufanywa usiku ili wananchi wasipate usumbufu. Je, Wizara inatoa kauli gani juu ya kadhia hii.

b) Hivi karibuni Shirika hili la Bandari wametoa kauli ya kuifanya bandari ya Forodha Mchanga kwa kusema imekuwa ikiwatesa wananchi kwa msongamano hapo Forodha Mchanga. Haioni ni sawa kufanya mzaha huko mlango wa nyumba wa mbele na kuufunga na kuufungua mlango wa nyuma.

c) Je, ni lini Serikali itatoa kauli ya ukweli wa kununua vifaa vya uhakika wa kufanyia kazi ili kupunguza msongamano kwani ni mazoea kuwa vifaa hivyo vimenunuliwa na viko njiani.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano) - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kujibu swali Na. 123 la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, naomba kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa kutokana na ufinyu wa eneo la kuhifadhia mizigo katika bandari ya Malindi, Shirika linalazimika kulitumia eneo lililofukiwa la Bwawani kuhifadhia makontena matupu ili kupata nafasi ya kuhifadhi makontena yenye mzigo bandarini. Kutokana na wingi wa makontena yanayopita bandarini hivi sasa, Shirika linalazimika kuyaondoa makontena hayo matupu muda wote kwani bila ya kufanya hivyo Shirika halitoweza kumudu kuyaondoa makontena yote matupu nyakati za usiku tu.

b) Bandari ya Forodha Mchanga imefungwa kwa amri ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kupitia Kamati maalum iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa kwa sababu za kiusalama pamoja na kuhifadhi Mji Mkongwe siyo Shirika la Bandari.

c) Shirika la Bandari linaendelea kununua vifaa vya kufanyia kazi bandarini kwa awamu kulingana na uwezo wa shirika. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita shirika limefanikiwa kununua vifaa mbali mbali vya wafanyakazi bandari kwa *Reach Stackers* tatu, *Empty Handler* pamoja na Tagi kubwa la kisasa. Vifaa vyote vimeshafika na vinatumika kupunguza msongamano wa mizigo. Aidha, shirika limeanza utaratibu wa kununua vifaa zaidi vya kufanyia kazi bandarini ndani ya mwaka huu wa fedha 2014/2015.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu kutokuwa na afya ya Mhe. Waziri ingawa wizara si yake anakaimu, naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa chimbuko la mrundiko wa makontena yanayotoka Bwawani na sasa kuelekea au Serikali ina mpango wa kuweka makontena katika uwanja wa Malindi. Serikali inashindwa kuweka *yard* kutafuta njia muafaka kama hawa wenzetu Dar es Salaam walivyojipanga ili kuondoa mrundukano huo.

La pili, bandari ya Forodha Mchanga imefungwa tumeshuhudia lakini kipi kinasababisha na sisi ndiyo tunaopitisha sheria, leo magari mule ndani yanapita na uzito kule na makontena juu kupeleka kule katika hoteli inayojengwa. Kipi kinachosababisha huyu afanye, huyu asifanye. Serikali inatoa kauli gani, huu si ubaguzi?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano): Mhe. Spika, ninashukuru na naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, suala la kurundikana kwa makontena katika bandari ya Malindi ni jambo ambalo limekuja kwa sababu ya uwezo wetu mkubwa sasa katika bandari yetu. Bandari yetu *alhamdulillah* sasa inapokea meli nyingi na kwa hivyo wafanyabiashara wanaitumia vizuri zaidi akiwemo yeye Mhe. Jaku Hashim. Kwa hivyo ni kweli kwamba tuna tatizo hilo la eneo la *container terminal*. Jambo hilo tunalo na tumekukuwa tukitafuta mahali mbali mbali mwa kuweka makontena yetu. Serikali imeunda kamati, imepitia sehemu nne, tano kuona kwamba wapi tuweke makontena yetu. Uamuzi wa kuweka makontena katika eneo la Malindi la muda huku Serikali ikiwa imeanza kufanyia kazi eneo jengine ambalo litakuwa karibu na bandari na ambalo litatumika kwa ajili ya kuwekea makontena.

   Kwa hivyo, hili musiwe na wasi wasi Mhe. Mwakilishi kwamba uamuzi huo umechukuliwa kwa dharura lakini wakati huo huo tunalifanyia kazi eneo jengine ambalo wapi tutaweka makontena eneo la kudumu karibu sana na eneo la bandari. Eneo Serikali imeshalipata na tayari tunalifanyia kazi kwa kutumia wataalamu wa ndani na wa nje ya nchi.

b) Kuhusu suala lake la kwamba eneo la Forodha Mchanga. Mhe. Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba eneo lile kutokana na usalama wa nchi yetu tumeona kwamba ni vizuri zaidi kulifunga kuliko kuacha eneo ambalo watu wanaweza kuingia, halafu nchi yetu kwa kweli ikapata matatizo kiusalama. Usalama ni jambo muhimu zaidi katika nchi kuliko eneo jengine.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, jana kwenye ziara ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Bandarini, watendaji wa Shirika la Bandari walikiri kwamba miongoni mwa sababu za msongamano wa makontena hayo ni tabia ya baadhi ya wafanyabiashara kugeuza ile bandari kama sehemu ya ghala, kama hivyo ndivyo ni lini Shirika la Bandari litatumia sheria ya kuyapiga mnada makontena ambayo yamezidi siku 21.

(b) zipo taarifa kwamba mfanyabiashara maarufu hapa Zanzibar ameomba eneo la Fumba ili apatiwe kwa kujenga parking ya makontena yote ya Zanzibar. Je, suala hilo ni kweli na kama ni kweli na lini mutampatia.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano): Mhe. Spika, ninakushukuru na ninaomba nimjibu Mhe. Hija maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo.

a) Ni kweli kwamba kuna wafanyabiashara wanacheleweshe sana kutoa mizogo yao bandarini na hili husababisha usumbufu mkubwa wa mrundikano wa makontena pale. Jitihada zimefanywa siyo mara moja siyo mara mbili za kuwaelimisha ili kuona kwamba hali hiyo inaondokana na kwa kiasi fulani tumepata mafanikio kidogo, lakini bado hatujapata mafanikio katika kiwango kikubwa zaidi. Jitihada za kuelimisha zinaendelea na tutakaposhindwa basi hatua za kisheria tutachukua.

b) Mfanyabiashara anayeleta wazo la kuanzisha *container terminal* Fumba; suala hilo bado wizarani kwangu halijafika, ninadhani lipo katika maeneo ya *ZIPA* na maeneo mengine, wakati muafaka ukifika basi Serikali itatoa kauli kuhusiana na suala hilo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe**.** Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, ipo kampuni moja Dar es Salaam ambayo makao makuu yake yapo Korea imeonesha azma ya kufanya shughuli ya kuondosha makontena katika bandari na tayari wameshapatiwa eneo la *ZIPA* kwa ajili ya kufanya shughuli hiyo hapo Fumba. Kinachowakwamisha ni suala la kibali kutoka Wizara yake ili waanze kufanya shughuli hiyo.

Je, Mhe. Waziri ni kitu gani kinachowakwamisha kuwapa kibali watu hao ili wafanye hiyo shughuli ambayo kwa kweli imekuwa kero sana kwa wananchi wa Zanzibar na wafanyabiashara.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano): Mhe. Spika, ninashukuru na naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba mwekezaji huyu amefika *ZIPA*, mawasiliano ya *ZIPA* na mwekezaji yanaendelea lakini pamoja na kwamba mawasiliano na *ZIPA* yanaendelea na sisi kama Wizara inayoshughulikia na mambo ya *handling* ya makontena na sisi tuna sheria zetu kupitia Shirika la Bandari.

Kwa hivyo, kabla ya kumaliziana lazima wataalamu na wanasheria wetu wa Shirika la Bandari wahakikishe kwamba uwekezaji utakaofanywa utakuwa na maslahi na Shirika letu la Bandari, hatuwezi tu kukuripuka kutoa kibali cha mwekezaji kufanya shughuli hizi, huku pia ikiwa shughuli zetu ambazo pia zina maslahi na shirika letu zikapotea.

Mhe. Spika, kwa hivyo, kama nilivyosema awali bado tuachieni Serikali ikilimaliza, Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano itatoa uamuzi kuhusu suala hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kuuliza swali langu hili naomba uniruhusu dakika moja tu.

Mhe. Spika: Sijakufahamu Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kabla ya kuuliza swali langu hili Mhe. Spika, naomba unigaie dakika moja tu ya kutoa neno shukurani.

Nikubaliana na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kauli aliyetoa juzi katika ukumbi wa *Ocean View* kuwa tumepiga hatua kidogo katika sekta ya afya. Hili nishukuru ni kweli tusiwe tunawalaumu kiasi fulani, lakini mabadiliko kidogo katika sekta ya afya yapo. Vile vile Mhe. Spika, mimi uwakilishi wangu umetokana na kuajiriwa na wananchi wa Jimbo la Muyuni na wakaja kuniambia kazi basi ninafikiri itakuwa basi, na baadhi walioniajiri wapo katika ukumbi huu.

Katika kipindi cha Novemba-Disemba kumejitokeza uhaba mkubwa wa dawa za matibabu ya binadamu na kuathiri vituo vya afya vijijini ikiwemo vituo vya afya vya Jimbo la Muyuni, kama vile Jambiani, Bwejuu, Kitogani na Muyuni yenyewe.

a) Je, Serikali inawaeleza nini wananchi juu ya tatizo hilo.

b) Kwa kuwa wananchi wa vijiji tegemeo lao kubwa ni vituo vya afya vya Serikali kutokana na kutokuwepo vituo vya afya vya watu binafsi Serikali ilichukua hatua gani za dharura ya kukabiliana na tatizo hilo.

c) Kwa kuwa suala la matibabu ni haki ya msingi Kikatiba kwa kila mwananchi. Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama ikiwemo kutonunua magari yenye gharama kubwa na badala yake kuelekeza nguvu zake katika kuimarisha huduma za afya hasa katika hospitali za vijijini.

d) Mhe. Rais alisema meneno hapo Bwawani siku ya tarehe 6/12/2014 Jumamosi katika kilelel cha udhalilishaji watoto na ubakaji maneno haya, "anayevunja Katiba ni mhalifu". Haioni Wizara ya Afya inavunja haki za msingi ya Kikatiba kwa kuwakosesha huduma za afya wananchi wake ikiwemo kukosekana kwa huduma za dawa katika vituo vya afya vijijini.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa wazima wa afya na tukiwa katika Baraza lako tukufu kuwakilisha wananchi wetu. Kwanza kabisa Mhe. Spika, naomba kabla sijamjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, naomba sana nichukue fursa hii kumpongeza kwa kuwa karibu na wananchi wake na kushirikiana na pia panapokuwa na suala huwashirikisha wananchi hao ili wajumuike pamoja.

Mhe. Spika, naomba kutambua uwepo wa wananchi maeneo hayo yaliyotajwa katika hili swali kutoka Jimbo la Muyuni; wananchi wa Jambiani wakiongozwa na Sheha wao wa Jambiani Mzee Ali Mtumwa ambaye yupo pale juu na akiwa amefuatana na wananchi wake. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Hebu wasimamie basi tuwaone. Haya ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa kuwa suala hili limewagusa moja kwa moja wananchi hao wa Jimbo la Muyuni na utaratibu mzuri sana kwa Wawakilishi kuja na wananchi wao humu, ninaamini Wawakilishi wengi wataiga mfano mzuri wa Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa kuja na wananchi wao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 121 kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, naomba kulieleza Baraza lako tukufu kwamba katika miezi ya Novemba na Disemba pamoja na miezi mengine ya nyuma ni kweli kulikuwa na uhaba wa dawa kutokana na mipangilio ya kibajeti kwa upande wa Serikali na pia kwa upande wa mfadhili wetu mkuu katika masuala ya madawa ambao ni *DANIDA* chini ya Serikali ya Denmark.

Mhe. Spika, ninafikiri kuwa tatizo hilo lililokuwepo ni kumalizika kwa baadhi ya dawa na siyo dawa zote na hii ilitokana na matatizo ya uagiziaji. Mfumo mzima wa uagiziaji pamoja na fedha kufika

kwa wakati kupitia mfumo mpya ambao vituo vya afya husika hufanya makisio ya mahitaji yao ya dawa kwa kipindi cha miezi mitatu mitatu.

Mhe. Spika, mfumo huo mpya ambao umeanzishwa unajulikana kama ni mfumo wa *Zanzibar Integrated Logical System* ambao tunafanya kazi pia na Serikali mbali mbali ikiwemo DANIDA na Serikali ya Marekani.

(b) Mhe. Spika, inapotokea hali ya kuishiwa na dawa kabla ya kipindi cha agizo jengine la dawa, hatua za usambazaji wa dharura huchukuliwa mara tu timu za afya za Wilaya zinaporipoti upungufuhuo uliojitokeza. Pamoja na kufanya hivyo, hatua za dharura zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana kwa ajili ya ununuzi wa dawa.

Aidha, ninapenda kutoa taarifa kwa Baraza lako tukufu kwamba hapa ninapozungumza leo nimesimama tayari dawa zote zimeshanunuliwa na hivi sasa kazi ya usambazaji wa dawa hizo unaendelea.

Mhe. Spika, naomba kulijuulisha Baraza lako tukufu kwamba Jimbo la Muyuni katika mpangilio wa kugawa hizo dawa na hii ratiba, hizo dawa ziligaiwa zote katika maeneo yote hayo jana na zilifika.

(c) Kwa mantiki hiyo Mhe. Spika, jibu la kifungu (d) la swali hili kwamba wananchi hawajanyimwa haki yao ya msingi ya Kikatiba ya Zanzibar pamoja na sera za Afro Shirazi Party ambazo bado zinaendelea kutumika kwa kutoa matibabu bila ya malipo au matibabu bure pamoja na huduma zote afya zikiwemo dawa.

Mapungufu haya Mhe. Spika, hutokana na mawasiliano ambayo pia huathiri usambazaji baadhi ya wakati, lakini hivi sasa magari yapo ya kutosha na hivi karibuni tu tumepata pikipiki ambazo huwa zinaleta taarifa panapotokea mapungufu sehemu yoyote.

Mhe. Spika, hatua nyengine zilizochukuliwa ni kukamilisha taratibu za ununuzi wa dawa kupitia *framework contract* ambapo makampuni badala ya kuitisha *tender*, makampuni maalum huchaguliwa na kupewa kazi ya kusambaza dawa badala ya *Medical Stores Dar es Salaam (MDC)* kama ilivyokuwa hapo zamani, ambayo yenyewe pia nayo ina uhaba mkubwa wa dawa muhimu.

Tunatarajia tena mwishoni mwa mwezi wa Februari kupokea mzigo mkubwa wa dawa baada ya kupatikana fedha za *DANIDA* na fedha za SMZ kupitia *framework contract* hiyo hiyo ambayo itasaidia kuwapatia wananchi huduma ya dawa bila ya usumbufu na uhakika kwa miezi sita ijayo.

Mhe. Spika, naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kuwa vituo hivyo pamoja na vyengine vyote havitokuwa na upungufu wa dawa kwa miezi sita ijayo hadi hapo mzunguko huu wa awali utakapokuwa umekamilika.

(d) Lengo la Wizara ya Afya ni kuwapatia wanachi huduma za afya bila ya usumbufu wowote na zilizokuwa nafuu. Huduma hizi hupatikana bila ya malipo katika vituo vya afya mjini na vijijini.

Ununuzi wa magari ya kifahari ambayo Mhe. Mwakilishi ameyataja, haumo kabisa katika vipaumbele vya wizara. Gari nyingi ambazo mtakuwa mnaziona gari hizo kweli ni za Wizara ya Afya, lakini ni misaada kutoka kwa wafadhili wa maendeleo moja kwa moja ambayo huletwa kwa shughuli maalum, na sio kupitia fedha ya bajeti yetu. Ahsate sana Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahasnte sana Mhe. Spika, pamoja na Mhe. Naibu Waziri kukiri kwa dhati kabisa kuwa palikuwa pana upungufu muda mrefu wa madawa.

(a) Je, wizara yako kama mwakilishi kajitolea jimboni kwake na wakati sio wajibu wake kupeleka dawa, mko tayari kumlipa gharama zake zile za kuwasaidia wananchi wake, wakati jukumu lile ni la wizara na sio la mwakilishi.

(b) Kwa kuwa tatizo la dawa kuwa tutapewa tena kwa wakati umekuwa ni wimbo wa taifa kwa muda mrefu. Hii mipango ya kujipanga hadi hivi sasa kuna maeneo yangu mimi kama nilivyoyataja. Ni lini dawa hizi zitafika na wakati mwengine kutokana na sababu ambazo sio za msingi, dawa ziko Bohari Kuu, kutoka Bohari Kuu mpaka Mnazi Mmoja kwa mwendo wa miguu, haufiki nusu saa. Dawa zinaharibika Bohari Kuu Mnazi Mmoja hazipatikani, unawaeleza nini wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza naomba niseme kwamba tatizo hili sio la muda mrefu, huwa ni tatizo la kipindi maalum, huwa linatokea na kuondoka kutokana na uagiziaji wa dawa.

Mhe. Spika, pia hatuwezi kuagiza dawa nyingi zikakaa kwa pamoja. Kwa sababu kila dawa ina tarehe ya kuharibika. Kwa hivyo, hilo hatuwezi kufanya, ndio maana inabidi kila baada ya muda hususan miezi sita tunatakiwa tuagizie. Kwa hivyo, kwa mwaka tunafanya yale maagizo mawili makuu. Lakini pindipo panapotokea shida yoyote ya dawa fulani, basi huwa zinaagizwa mara moja.

Mhe. Spika, vile vile kama mwakilishi kajitolea kununua dawa katika jimbo lake ama vituo vyake. Hilo naweza kusema sote tunajitolea, naamini ni wajibu kwa wananchi wetu, kwa sababu tulipoapa sote tuliapa kuwatumikia wananchi pia kuitumikia serikali yetu iliyokuwepo madarakani. Naamini hakuna mwakilishi anayedai malipo kama hayo pamoja na mimi.

Mhe. Spika, kama juzi Kituo cha Chukwani kiliharibika pampu ya maji pale na tuliweza kuchangia bila ya kudai malipo yoyote na mimi niko katika Wizara hiyo hiyo ya Afya. Kwa hivyo, sidhani kama hilo ni jambo la busara sana.

Mhe. Spika, nitapenda kutoa mfano mwengine, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika Kituo cha Kitope. Kwa kweli naomba nimpongeze sana na ni mfano wa aina ya pekee, kwa Kituo cha Kitope, kinajulikana kama Kituo cha Balozi Seif Ali Idd, wala sio cha Wizara ya Afya kwa mambo mengi anayo yafanya yeye pale. Kuna ukarabati wa hospitali, kuna lile shimo la kutupia *pleasanter pit* na mambo mengine yote. Hata upande wa madawa, kwa kweli ameonesha mfano mzuri sana.

Mhe. Spika, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ametuonesha mfano, kiasi cha kwamba hivi sasa katika Wizara ya Afya tumekaa kikao tunataka kufanya utaratibu maalum, kila tunapotembelea Vituo vyetu vya Afya, hususan vijijini basi tuwashirikishe wawakilishi wanaotokea maeneo yale, ama vijiji vile, ama jimbo lile ama wale wawakilishi wa viti maalum wanaotokea wilaya zile. Kwa sababu katika kufanya hivyo, tutaweza kufanya vile vituo vya afya vionekane vya jamii zaidi, kuliko kubakia vya Wizara ya Afya tu.

Huwa tunarudia mara kwa mara, kweli viko chini ya Wizara ya Afya, lakini ni vituo ambavyo vinatoa huduma kwa jamii. Mhe. Spika, Kituo hiki cha Jambiani kinapokosa huduma yoyote wanaoathirika zaidi ni wananchi wa Jambiani, sio wengine wowote.

Mhe. Spika, jambo la mwisho kabisa, Mhe. Mwakilishi amesema kwamba ni wimbo wa muda mrefu. Ulikuwa wimbo wa muda mrefu kwa sababu tulikuwa hatuna *Computerize System*. Sasa hivi tunashukuru Serikali ya Watu wa Marekani wametuletea *Computerize System*, tunaweza kujua *stock* iliyokuwa imebakia, tunaweza kujua tarehe za kuharibika zile dawa, tunaweza kujua *stock* yote, pengine kuna dawa Jambiani; ziko nyingi zaidi, lakini Kituo cha Muyuni hakuna dawa zile.

Kwa hivyo, kwa *system* hii sasa hivi tunaweza kujua kwamba Kituo cha Jambiani kinatakiwa kipunguziwe dawa hizi kwa sababu ziko nyingi, zipelekwe kituo cha Muyuni. Kwa hivyo, kwa *system* hiyo tunaamini wimbo huo hautokuwepo tena, sio kwamba wa muda mrefu hautokuwepo tena. Ahsante sana.

Nam. 126

Kusimamishwa Kazi Kwa Muuguzi Mkuu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza:-

Kanuni za Utumishi wa Umma zinaelekeza kwamba pindipo mtumishi wa umma anapofanya kosa kuhusiana na kazi yake, Katibu Mkuu, Mkuu wa Taasisi au Mkuu wa Idara husika anapaswa kuzingatia kama kosa hilo ni la jinai au ni uvunjaji wa nidhamu za kazi au aina zote mbili.

Kama kosa hilo ni nidhamu, Mkuu anaehusika atampa taarifa ya dai hilo mtumishi husika na kupewa nafasi ya kujieleza na baadae kuchukuliwa hatua muwafaka. Kama kosa ni la jinai ataripotiwa kwa chama cha wafanyakazi na hatimae polisi kwa uchunguzi zaidi.

(a) Je, uongozi wa wizara umefuata taratibu za kanuni hizo ya kumpa taarifa ya dai mtumishi wake, aliyekuwa anafanya kazi kama Muuguzi Mkuu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja na kumpa nafasi kujieleza na hatimae ikadhihirika na kosa lake na kumvua cheo hicho.

(b) Kwa vile hakupelekwa polisi ni dhahiri halikuwa kosa la jinai, sasa wizara ilibaini kosa gani la nidhamu walipomsimamisha kazi Muuguzi Mkuu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja na kumpa likizo la lazina na bila ya malipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 126 lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, uhamisho wa wafanyakazi katika idara moja kwenda idara nyengine, au uhamisho ndani ya idara uko chini ya mamlaka ya Katibu Mkuu au Mkuu wa Wizara au Idara husika, kama Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya 2011 inavyojieleza katika kifungu 65(i). Ni hivyo hivyo Mkuu wa Idara anaweza kupendekeza ama kuteua mtu kushika dhamana ndani ya Wizara au Idara yake kama sheria hiyo inavyoelekeza.

Mhe. Spika, mtumishi aliyehusishwa katika suala hili, hakupewa likizo bila malipo na wala hakuna kosa lolote alilolifanya, ndio maana hakupewa barua ya onyo au kuitwa kujieleza, wala kuchukuliwa hatua yoyote mbele ya uongozi wa wizara.

Mhe. Spika, utaratibu wa kumhamisha sehemu nyingine umefanywa kwa lengo la kuleta ufanisi na maelewano zaidi kwa taasisi husika, na hauna lengo la kumkomowa mtu yeyote yule kwa namna yeyote ile.

Mhe. Spika, aidha wizara imekuwa ikifanya mabadiliko ya watumishi wake wa ngazi mbali mbali kwa nyakati tofauti, na tumekuwa tukifanya hivyo pia kwa kada ya madaktari kuwaondosha kutoka vituo mbali mbali kuwahamisha na kuwapeleka katika wilaya nyengine mbali mbali au mikoa mingine.

Mhe. Spika, naomba ninukuu barua ambayo wizara imemjibu mfanyakazi husika pale alipoleta malalamiko yake ya utaratibu wa kawaida uliofuatwa. Naomba ninukuu barua hiyo;

> "Naomba kukujulisha ndugu mfanyakazi kuwa uhamisho uliopewa sio adhabu bali ni utaratibu wa kawaida wa kisheria, ambapo Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi anayo mamlaka kamili ya kumpa uhamisho mtumishi kutoka sehemu moja hadi nyengine.
>
> Aidha, barua yako ya kuingizwa kazini uliyopewa kipengele namba 4 kinahusika. Kwa vile hakukuwa na shauri la utovu wa nidhamu juu yako kazini au jambo lolote lile dhidi yako, basi hakukuwa na haja ya kutumika vifungu ambavyo umevitaja cha 82 cha sheria namba 2 ya mwaka 2011 na kifungu cha 107 cha kanuni za utumishi wa umma.
>
> Kwa hivyo, hakukuwa na haja ya kupewa fursa yoyote ya kujieleza kabla ya kuchukuliwa hatua yoyote ile. Kwa hivyo, kwa barua hii unajulishwa kuwa uhamisho huo ni halali na unaombwa kuwa mtulivu sana katika kazi yako. Aidha, unatakiwa uendelee kuzingatia maadili ya kazi na kada yako uliopangiwa kisheria. Nakutakia utekelezaji mzuri wa majukumu yako mapya". Ahsante sana Mhe. Spika, mwisho wa kunukuu.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa mabadiliko ya muda mfupi yaliyotokea katika hospitali hiyo, kuanzia nidhamu za wafanyakazi hadi usafi wa hospitali yenyewe kwa kuwepo muuguzi mkuu huyo, hilo kosa alilofanya halitowi nafasi ya kupewa onyo na kumrudisha hospitali ya Mnazi Mmoja, ili aendelee kusimamia zogo la watazamaji na wanaouguza wagonjwa, usafi wa hospitali, utoro wa wafanyakazi na udokozi wa hapa na pale, jambo ambalo lilianza kuonesha kuzaa matunda.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kurudia tena, ni kweli uvumi umekuwa kama yule mfanyakazi alifanya kosa. Ni kweli hata mimi uvumi huo niliusikia, lakini hapa, hatufanyi kazi kwa uvumi, tunafanya kazi kwa ushahidi kamili. Naomba kurudia tena kwamba hakuna kosa alilolifanya mfanyakazi huyu. Uhamisho wake kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja kwenda Hospitali ya Mwembeladu, basi Mhe. Mwakilishi aelewe kwamba ile hali nzuri aliyoifikisha pale Mnazi Mmoja kuwa inafanyakazi vizuri sasa hivi, tunataka hali ile ile ihamie Hospitali ya Mwembeladu.

Mhe. Mjumbe umeeleza suala la utoro, umeeleza suala la uchafu, umeeleza suala la usafi, umeeleza suala la hali nzima ya hospitali kuwa nzuri. Kwa hivyo, pale pakishakaa sawa Katibu Mkuu ama Mkuu wa Idara ana mamlaka ya kumpeleka katika kituo chengine, pengine Kivunge au kwengine ili kuiweka hali nzuri. Kwa sababu kuna wafanyakazi wengine Mwenyezi Mungu kawajaaliwa kipaji, wanakuwa viraka, anapelekwa pahala kuweka mambo sawa akishamaliza anapelekwa kwengine, ile hali inakuwa imeshakaa sawa.

Kwa hivyo, naomba niseme kwamba hali iliyokaa sawa Mnazi Mmoja inaendelea vizuri na sasa hivi hali hiyo hiyo anaitekeleza vizuri sana na tunampongeza pale hospitali ya kinamama ya Mwembeladu. Juzi niliwaona wajumbe wa akinamama wanakwenda pale kujitolea, nawapongeza sana kwa hilo. Nadhani mlipata mashirikiano ya kutosha kutoka kwa mfanyakazi huyu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipatia nafasi hii ili niweze kumuuliza Mhe. Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza nimsifu sana Mhe. Naibu Waziri anajibu maneno mazuri, yenye ufasaha kabisa na ananukuu sheria ambazo zinamuajibikia mtumishi.

(a) Ni muda gani ambao anatakiwa mfanyakazi katika *section* ili aweze kubadilishwa kupelekwa *section* nyengine. Lakini pamoja na hayo kutokana na hiyo ripoti ambayo uliyoisoma hivi sasa, muhudumu huyu kama ulivyoeleza alikuwa Muuguzi Mkuu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, na yeye alikuwa na sheria ya kuweza kuwahamisha watu kuwapeleka kitengo hadi kitengo.

Je, ni hasara ipi ya kuwa yeye kwa mujibu wa sheria kupelekwa sehemu nyengine?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwanza naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba katika sheria ya utumishi hakuna muda maalum kwa mfanyakazi kukaa sehemu moja kwamba baada ya muda ule ahamishwe kwengine, hakuna muda maalum uliopangwa. Muda maalum tunao sisi wawakilishi. Ikifika tarehe 30 Julai ama baada ya hapo Baraza likishavunjwa kila mtu mmoja anarudi jimboni kwake au kwenye kiti chake maalum anachokwenda kukitetea.

Kwa hivyo, kwa wafanyakazi wa serikali hakuna muda maalum wa kukaa sehemu moja; ule ni utaratibu ambao Idara ya Utumishi katika kila wizara inapangilia kwa wafanyakazi wake kutokana na mahitaji na kada nyengine zozote zilizokuwa zimepangwa kisheria. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, ni kweli alipokuwa Muuguzi Mkuu alikuwa na haki ya kuwahamisha wafanyakazi kama Mkuu wa Idara na yeye anakuwa ni Mkuu wa Idara pale, ana haki hiyo na haki hiyo aliitumia. Lakini ilipofikia wakati kwamba tumeona mahitaji yake, uwezo wake aliokuwa nao, utendaji wake, umahiri wake unahitajika sehemu nyengine, basi na yeye mkubwa wake wa juu kamchukua pale kamuhamisha kumpeleka kwengine, ili akaweze kuweka sawa huko kwengine kulikokuwa kumeharibika. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri ametuambia kwamba mfanyakazi huyu alihamishwa kwa uhamisho wa kawaida kupelekwa hospitali nyengine kutokana na kazi yake nzuri aliyoifanya ya kuweka usafi na mambo mengine katika hospitali ya Mnazi Mmoja, na ndio maana wamempeleka Hospitali ya Mwembeladu kwa ajili ya kuweka mambo sawa kama alivyofanya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri. Je, mfanyakazi huyo kuna posho lolote mlilomuongeza kutokana na kazi yake nzuri. Au kuna motisha mliompatia kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kama nilivyosema hapo awali kwa kazi yake nzuri ndio amehamishwa hapo. Jambo hilo ni kwa sababu hata huyo mfanyakazi hatukumtaja jina mpaka sasa hivi. Jambo hilo la kuongezewa. Kupunguziwa hajapunguziwa, naweza kusema. Lakini jambo hilo la kuongezewa tunajadiliana hivi sasa kwa hivyo nisingependa kutoa siri za vikao vyetu ambavyo tunafanya juu ya wafanyakazi. Kwa sababu kitu kama mshahara, posho kumtajia moja kwa moja mtu, huwezi kutoa siri hiyo. Lakini jambo hilo tunajadiliana kwenye vikao vyetu na hivi sasa linazingatiwa Mhe. Spika. Ahsante sana.

Nam. 94

Upungufu wa Watendaji Zawa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa ZAWA imekuwa na uhaba wa wafanyakazi, hali inayozorotesha baadhi ya shughuli zao.

a) Je, ni lini serikali itafanya utaratibu wa kuajiri wafanyakazi wapya.

b) Kuchelewa kuajiri watendaji wapya si kurudisha nyuma maendeleo ya Mamlaka ya Maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 94 kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, wizara yangu kwa kupitia Mamlaka ya Maji inaendelea na utaratibu wa kuajiri kulingana na mahitaji ya fani husika kwa kadiri ya uwezo unaporuhusu. Hali ambayo kama inavyoeleweka suala la ajira ni suala endelevu kulingana na mahitaji na wakati husika.

Mhe. Spika, naomba kutokukubaliana na Mhe. Mwakilishi juu ya dhana, kuchelewa kuajiri ni kurejesha nyuma maendeleo ya mamlaka, bali afahamu ya kwamba kuwapa na mafunzo wafanyakazi tulionao, ndiko kutaleta ufanisi kwa serikali kwa ujumla, hali ambayo inapelekea wizara yangu kwa kupitia Mamlaka ya Maji kuwa na chuo cha taaluma ndani ya mamlaka, chenye lengo la kuwakuza wafanyakazi kiuwezo na kufanyakazi zao ipasavyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Pamoja na majibu ya kusikitisha aliyotoka Mhe. Naibu Waziri hivi sasa na ya kuvunja moyo, hasa kwa wananchi wa Jimbo la Muyuni, naomba kumuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Suala la upatikanaji wafanyakazi, hivi sasa limekuwa ni suala la muda mrefu. Ni muda mrefu Mhe. Naibu Waziri napiga kelele; kuna wananchi wangu wa Jimbo la Pete, Mungoni, na Muyuni baadhi ya sehemu wamekosa maji kutokana na uhaba wa mafundi.

Mhe. Spika, nilikwenda kuripoti sio mara ya kwanza wala sio mara ya pili kuwa sio mara ya tatu. Vile vile kwa kushirikiana na Mbunge wangu Mamlaka ya Maji inajua kazi tuliyofanya sisi, sina nia ya kutaka kujisifu. Lakini ni lini mtaongeza na ukenda Mamlaka ya Maji unaambiwa mafundi ni haba. Hayo sizungumzi kwa kubahatisha wala kwa kukurupuka tu. Bado kilio hiki kipo ukikitaka usikitake Mhe. Naibu Waziri, ni lini mtaongeza wafanyakazi.

Pia, tatizo hili la Jimbo la Muyuni ni lini mtalitatua kwa kushirikiana na Mbunge na Mwakilishi. Wananchi baada ya kujishughulisha na kilimo kwa muda mrefu, sasa umekuwa muda mrefu wa kuhangaika na maji. Je, ni lini wimbo huu utamalizika?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nisharti: Suasla la kuongeza Wafanyakazi ndani ya Mamlaka ya Maji hili suala tunalifanya kila pale tunapohitaji wafanyakazi, na hili suala tumelifanya si muda mrefu tumeajiri wafanyakazi kwa fani tofauti, mafundi na fani nyengine si muda mrefu ambapo tumewaajiri na tumewafanyia *interview* ndani ya Mamlaka ya Maji, kwa hivyo suala la ajira ni kwamba tunajitahidi kuajiri kwa kadri ya vile hali inavyoruhusu.

Mhe. Spika, suala la pili ni kuhusu Jimbo la Muyuni maeneo ya Pete kuhusu tatizo la maji, hili suala vile vile tunalishughulikia na tunajua kwamba bado kuna matatizo ya upunugufu na hili nimuahidi Mheshimiwa Mwakilishi, kwamba kupitia Mamlaka ya Maji tutashirikiana nae, ili tuweze kulitatua tatizo hili kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyotuwezesha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu kifungu cha 37 tena naomba nikinukuu Mhe. Spika, Waziri au Mjumbe yeyote anayeulizwa suali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu suali hilo, kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi, isipokuwa kwamba suali lililoulizwa na Waziri Mmoja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine.

Mhe. Spika, siwezi kusema kwamba nimetiwa mchanga wa macho lakini suala lina muda mrefu kwa wananchi wangu na nitaendelea kulisimamia mpaka dakika ya mwisho, aniambie baada ya kikao au kesho kushirikiana na mie na mafundi wake twende tukakague kero hizo ambao huu mwaka wa tano unaingia hivi sasa.

Nataka unipe muda wa uhakika humu kwenye Baraza, huu ni mwaka wa nne tokea kuingia na kilio hiki na niko tayari kuchangia kwa gharama yoyote, unipe muda ambao utakamilika kesho, keshokutwa unipe muda ili *Hansard* zikae sawa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nisharti: Mhe. Spika, kama ingelikuwa Watu wa Pete kwa muda wa miaka minne hawajapata maji basi hali ingekuwa mbaya sana, isipokuwa kinachotokea Pete ni kutengenea maji na kuharibika maji kama inavyotokea katika maeneo mengine, kuna baadhi ya wakati maji yanatengenea watu wanapata kama inavyotokea katika maeneo mengine, maji yanatengenea watu wanapata, na baadhi ya wakati maji yanaharibika mitambo watu hawapati na maeneo mengine yanatokea hivyo hivyo.

Hata hivyo mimi niko tayari kufuatana na yeye twende Pete tukaione hiyo hali halisi ilivyo, lakini kusema kweli suala la kushughulikia maji tunashughulikia na kinachofanya kazi ni mitambo na mitambo wakati mwengine inaharibika na wakati mwengine inakuwa mizima.

Mhe. Spika: Waziri anakubali muende mukaangalie hilo tatizo, pangeni siku wewe na Waziri mwende huko.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, Waziri ameshanipa katika chombo hiki kauli mara tatu au mara mbili katika chombo hiki hiki mwisho biashara yoyote inayoendelea.

Mhe. Spika: Pangeni tena muende muniletee taarifa. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba niulize suala dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa mara baada ya ule mradi uliofunguliwa katika Sherehe za Mapinduzi hizi za miaka 51 pale Vikunguni, ule mradi wa Kichina kuanza wafanyakazi wa *ZAWA* walikwenda katika kijiji cha Kibokoni katika jimbo langu la Wawi, na wakawahamasisha watu waunge maji na wakasema na kuwaambia wazi kwamba, kwa wale ambao hawana vifaa vimewapungukia tutawakopesha, kwa bahati wananchi wa Kibokoni waliuza njugu zao zile, wakauza ndizi zao na wakaunga maji kwa wingi. Lakini maara baara ya ufunguzi maji siku ile yalitoka kwa sana, lakini baada ya siku moja maji yamekata hadi leo hii.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zilizosababisha wa Kibokoni, Matungu, pamoja na Vunja Membe na Ungali mpya ikawa hawapati maji.

(b) Kwa kuwa Mfikiwa kipo kisima kimeshajengwa kisima cha maji lakini kisima kile hadi leo hii hawajaungiwa watu wa Mfikiwa ni sababu gani za msingi zinazosababisha kisima kile kisifungwe

mashine na kuanza kuhudumiwa watu wa Mfikiwa na hadi leo hii ikawa wanapata shida ya maji, huku fedha nyingi za Serikali zilitumika katika kuchimba kisima kile.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nisharti: Kwanza napenda kugusia kwamba Mhe. Jaku Hashim Ayoub mara nyingi anakuja ofisini kwangu lakini akija anaomba hati ya viwanja hazungumzi habari ya maji.

Mhe. Mwenyekiti, kisima cha Vikunguni ambacho kwa bahati mbaya kilipigwa maji na anasema hivi sasa maji hayapatikani, Mheshimiwa Muwakilishi angalinijuulisha mapema suali hili mie ningejua sababu. Kwa sababu mimi si ruhani kwamba ninaweza kujua kitu fulani kinatokea vipi, mahala fulani, kwa hivyo nataka nipewe taarifa mahala fulani pana hiki, mahala fulani pana hiki. Mfano mzuri hapa Mheshimiwa Ali Salum kazungumza habari ya Kwaalimsha, nikasema hapa nitalifuatilia suala hili na hapa ndio nilipata taarifa. Lakini kwa bahati saa ile ile maji yameanza kutoka mpaka saa mbili ya usiku kwa sababu kalieleza, sasa angenieleza mapema nisingepata tatizo hili.

Sasa na hili la Mheshimiwa Saleh Nassor Juma, vile vile nalo angelinieleza mapema ningelijua nafanya nini maana pamoja na kuwa nipo Unguja lakini kule nawasiliana na najua mambo yanavyoendelea, ila najua tu kusijekuwa kuna tatizo la umeme kwa sababu tuna visima vyetu vipya ambavyo tuko kwenye majaribio navyo, lakini tunashindwa kuyajaza maji matangi yake kwa sababu ya tatizo la deni la umeme. Pengine hiyo inaweza kuwa ndio sababu na hivyo vipengele tunashindwa kuvijaza maji.

Kwa hiki kisima ambacho kwa bahati mbaya hivi sasa hakijaungwa kwanza, hiki kilichoungwa kinatosha kwa ajili ya tangi lile na hakina matatizo yoyote, hiki ni kisima cha hakiba na tukipata hali matatizo ya huku tutakuwa tunatumia huku bila ya tatizo lolote.

Nam. 50

Kupatiwa Mikopo na Masoko Wafugaji wa Nyuki Wawi

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aluliza:-

Wanawake wa Jimbo la Wawi katika suala la kupambana na umasikini pamoja na kujiongezea kipato wamewekeza maisha yao katika ufugaji wa nyuki na kilimo cha mboga mboga. Na kwa kuwa suala la ufugaji wa nyuki linahitaji taaluma na upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya kinga maalum wakati wa kuvuna au kufua asali hiyo.

(a) Ni lini Serikali kupitia taasisi za fedha itatoa mikopo yenye masharti nafuu ili wafugaji hao waweze kufuga nyuki katika misingi ya kitaalumu.

(b) Kwa kuwa soko la mboga mboga katika masoko ya Chake Chake likiwemo lile la Qartar huzidiwa na bidhaa hiyo na hatimae wakulima hulazimika kuuza kwa bei ya chini jambo linalorudisha nyuma maendeleo yao. Je, Serikali inawashauri wafanye nini akina mama hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake nambari 50 lenye vipengele (a), na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili haitowi mikopo kwa wakulima wake ikiwemo wafugaji wa nyuki. Suala la kuwawezesha wananchi linatekelezwa na Wizara ya Uwezeshaji Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Wizara hii ina jukumu la kuwshajihisha na kuwahamasisha wananchi kujiingiza katika ufugaji wa nyuki na kujiunga katika vikundi. Wizara inatowa mizinga na mafunzo ya mbinu bora za ufugaji wa nyuki kwa wale wanaojishughulisha na kazi hiyo kama hao wanaushirika wa Tujiendeleze wa Jimbo la Wawi Chake Chake, Pemba.

Kinachofanyika ni jitihada za kupunguza umasikini na kuwaongezea kipato wananchi kwa kupitia shughuli mbali mbali. Hata hivyo wafugaji wa nyuki wanaweza kupata mikopo binafsi na vikundi vya kukopa na kuweka kama vikoba au kupitia taasisi za fedha zinazotambuliwa na Serikali alimradi tu watimize vigezo na masharti ya taasisi hizo.

(b) Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili inawashauri wakulima hao kusarifu mazao na kuyaongezea thamani (*Agro-processing*) kwa madhumuni ya kuyatunza na kuyaongezea thamani mazao hayo. Wizara hii na pia Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kupitia *program* mbali mbali hutoa mafunzo ya kusarifu mazao kwa njia mbali mbali kwa kina mama na makundi mengine katika jamii.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa Wizara hii moja ya SMZ inayoshughulika na mambo ya mazingira hivi karibuni iliwapeleka madiwani wetu nchini Kenya, kwenda kuangalia mambo ya *environmental rehabilitation* katika sehemu zile zenye *serious environmental degradation* wakaondoka Madiwani wakenda kule kupitia hiyo hiyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa kuwa Vitongoji kuna wafugaji nyuki tena akina mama wenzako Mhe. Naibu Waziri na kwa kuwa mambo ya ufugaji nyuki wanahitaji taaluma ya hali ya juu, na kwa kuwa sehemu hizi ule Mkoa anaotoka Mheshimiwa Waziri Mkuu ni wafugaji wazuri wa nyuki na wanafuga kitaalam kabisa. Je, pamoja na kwamba hamutawapatia mikopo Serikali wala hamutoi ruzuku kwa akina mama wenzako mama;

(a) Je, ni lini Serikali itafanya kama ilivyofanya Wizara ile inayoshughulika na mambo ya mazingira kuwapeleka Nairobi, nyie musiwapeleke Nairobi muwapeleke kwenye Mkoa wa Mheshimiwa Mizengo Pinda waweze kwenda kujifunza kuhusu mabo ya kufuga nyuki.

(b) Kwa kuwa wakulima hawa wa Jeshini akina mama wale pale katika eneo la jeshi pale wa mama wale na kinamama katika jijiji changu cha Vitongoji Umangani pale, Udusini sehemu za mji wa chini huku wanapanda mboga mboga tena kwa kumwagiliaji maji ambao wanachukua maji masafa ya mbali sana, na kwa kuwa sasa hivi kuna kitu kinaitwa *drop irrigation* imestawi sana mambo haya na hii taaluma hii haiko kule kwangu.

Sasa ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara yako itafanya jitihada za hali ya juu kwenda kuwafundisha wale mama walioko Vitongoji Kibokoni, Udusini, Umangani, na Mfikiwa wakaweza kujua hii taalum ya *drop irrigation* na hatimae wakapata mpango wa kutekeleza ule mpango wa SMZ wa kupunguza umasikini na kujiengezea kipato.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Saleh Nassor Juma nakumbuka ziara yangu iliyopita nilikwenda kutembea katika Jimbo lako la Wawi, nikaonana na wafuga nyuki na katika wafuga nyuki wako hao wamo baadhi wameshakwenda kusoma huko kwa Mheshimiwa Mizengo Pinda, washapelekwa na wameshapata taaluma, tukawauliza kwa kauli yao sikutaka kauli za watendaji tu lakini nilizungumza nao uso kwa uso na akatoka mfuga nyuki mmoja akasema, mimi nimeshapata mafunzo kwenda kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mizengo Pinda. Kwa hivyo wako wafuga nyuki wanapelekwa kupata taaluma hii.

Jengine la kupata taaluma ya *drop irrigation* katika sehemu yetu ya Kizimbani kuna eneo ambalo tunawapa taaluma wakulima hawa wanaoutumia *drop irrigation*, kwa hivyo Watu wako wa Wawi sina uhakika kwamba hawajapelekwa lakini nitalifuatilia suala hili na ikiwa bado hawajapelekwa kwa sababu tunachukua kutoka Pemba, kutoka sehemu mbali mbali ikiwa bado hawajapelekwa basi tutafanya mpango japo wakulima wawili waje wapate nao taaluma hii ya *drop irrigation*.

Mhe. Subeti Khamis Faki: Nashukuru Mhe. Spika, kunipa na mimi nafasi nimuulize Mhe. Waziri suala moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri, alipokuwa na ziara ya kutembelea jimbo la Micheweni kwenye mradi wa kilimo na mambo mengine, ziara yake ilitokewa na dharura ikakatika njiani na mpaka leo hii bado hajarudi tena kuja kutembelea eneo la Micheweni, na kwa kuwa Micheweni pia kuna kikundi cha kufuga nyuki katika kijiji changu, na yeye hajawahi kufika hata siku moja akaja kukiona kile kikundi na kukifariji. Na kwa kuwa hakuna hata mmoja aliyepelekwa kwenye hayo mafunzo, ni lini Waziri atakuja kuwaona na kutembelea na wao kuwapangia ili kwenda kupata mafunzo zaidi ili waendeleze ufugaji wao wa nyuki na kujipunguzia umasikini.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Ni kweli nilifanya ziara na ziara hiyo ikatokea msiba tukakatisha, lakini nia na lengo na madhumuni yako pale pale, nia na lengo ni Wizara kuwatembelea wafugaji nyuki wetu wote, kwa sababu wako katika himaya ya Wizara yetu na nia na lengo kuwapatia mafunzo, kwa hivyo hilo nina imani hatutorudi nyuma kufanya ziara na wale ambao wanastahiki kupata mafunzo tutawapatia mafunzo inshaalla.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri suala dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Wizara yake haina mpango wa kutoa mikopo kuwawezesha wakulima wafugaji wa nyuki na wakulima wa mboga mboga, lakini kwa kuwa Unguja wafugaji wa mboga mboga imewapatia soko Jumaatano Darajani kuwasaidia kuuza mboga mboga zao;

Je, kwa Pemba Wizara yake ina mpango gani wa kuwapatia wakulima hawa wadogo wadogo na wao soko maalum la kuweza kuuza mboga mboga zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Ni kweli Wizara ya Kilimo kupitia mradi wa *VSO* maarufu tunaita *UWAMWEMA* tumewawekea soko kila siku ya Jumatano Darajani, lakini hatukuishia hapo hivi sasa tumo katika mpango kupitia mradi wa *MIVAS* kututafutia eneo Pemba, ili nao kuwapatia soko kama hili ambalo lipo Darajani.

MUONGOZO

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipatia na mimi fursa hii nimesimama hapa kuomba muongozo wako kupitia kanuni ya 35 fasili ya pili ambayo inasema;

"Taafira zote za masuali zitakazowasilishwa na Spika, zitaingizwa katika kitabu cha shughuli za Baraza endapo mkutano wa Baraza utafungwa kabla ya siku ambayo suali lililopangwa kujibiwa basi suala hilo litajibiwa katika mkutano utakaofuata, endapo yule aliyeuliza taarifa ya swali atakuwa bado ni Mjumbe.

Mhe. Spika, nimesimama hapa kwa muongozo huu, kipindi hiki cha Baraza nilileta Maswali matano, ambapo nikapata barua hii iliyothibitishwa na Katibu, lakini katika maswali hayo matano nikajibiwa wali moja tu la Namba 106 na ambapo barua hii ilisema tarehe 26 nitajibiwa swali Namba 108, tarehe 29 nitajibiwa swali Namba 10, na swali Namba 106 na 107 na tarehe 30 nitajibiwa swali Namba 109.

Mhe. Spika, nimejibiwa swali langu moja tu na ukiangalia katika *order paper* huwa yanakuja maswali ya Waheshimiwa Wajumbe wenzetu yanayopata matano, sita kwa mtu mmoja.

Je, ni sababu zipi zinazopelekea kwamba sisi wengine maswali yetu yasijibiwe na wakati ni maswali machache unaweza ukapangiwa moja moja tu likaingia ili hata kipindi cha Baraza kinapomalizika ikawa masuala yako haya yamejibiwa. Iwapo maswali haya na sisi tunayauliza kwa manufaa ya wananchi wetu ambao tunawawakilisha hapa. Ni sababu zipi Mhe. Spika, naomba muongozo wako. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Tatizo hapa ni ufinyu wa muda, ni tatizo kubwa. Lakini kama kuna maswali ya mjumbe mmoja mengi yanajibiwa na kwa bahati mbaya maswali ya Wajumbe wengine hayakupata nafasi, inawezekana ikawa hilo tatizo linatokana na Mawaziri wanaohusika na eneo hilo au pengine majibu yalikuwa hayajapatikana. Lakini kwa hapa na katika Mkutano huu tatizo ni ufinyu wa muda.

Kwa kawaida maswali ambayo hayakupata majibu katika mkutano huu na kama yalikuwa hayajasawazishwa matatizo yake, Mkutano unaofuata huwa yanapewa kipaumbele katika kuulizwa na kujibiwa. Sasa na haya ambayo yamekosa majibu kipindi hiki itabidi tufanye subra kwa kipindi kinachokuja yapate kipaumbele katika kujibiwa,

kabla hayajaingia mengine ili kama ni tatizo basi serikali iweze kuchukua hatua haraka sana katika yale maeneo ambayo maswali hayo ambayo yameulizwa.

Kimsingi tatizo kubwa ni ufinyu wa muda kufuatana na bajeti ambayo imepangwa kwa mkutano huu. Zipo shughuli nyengine ambazo zilikuwa zimeombwa zifanyike katika Mkutano huu nikatoa maelekezo kwa kuwa shughuli zetu zinaishia leo, basi tatizo hilo lizingatiwe katika mkutano ujao na maswali kama hayo pia tunaomba yazingatiwe katika mkutano ujao. Kama shughuli zitakuwa za maswali zimepungua, wakati mwengine watu wanakuwa na utaratibu wa hata kuongeza muda wa maswali kwa idhini yenu, ili Maswali mengi yawe yamepata nafasi ya kujibiwa. Kwa hiyo tatizo ni ufinyu wa muda, lakini muongozo ni kwamba kipindi kijacho maswali yaliokosa majibu sasa kwenye Mkutano huu yapewe kipaumbele. Nashukuru, muongozo mwengine Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, japokuwa umejibu vizuri sana lakini kuna jambo ambalo ningeomba nipate ufanisi zaidi wa lugha au muongozo kwa mujibu wa utaratibu nilivyoona miye kwenye *order paper*.

Mhe. Spika, mama ameeleza kwa mujibu wa barua ambayo amepewa kuwa maswali yake yatajibika moja, mbili, tatu, lakini *order paper* ya leo Mheshimiwa kuna mtu mmoja ana sehemu zaidi ya mbili mpaka tatu. Isitoshe Mheshimiwa mimi hapa sasa hivi nimeshakuwa nina wasi wasi na kama inawezekana Mheshimiwa tuunde Kijikamati kidogo kwa nini watu hawa hawa kila siku wanakuwa wana sehemu tatu kuliko watu wengine.

Mhe. Spika: Ofisi ya Katibu, tutashauriana kurekebisha jambo hilo ili kila Mjumbe ambaye ameuliza maswali, maswali yake yapate nafasi ya kujibiwa. Wajumbe wote katika Baraza hili wako sawa, hakuna mjumbe aliye mkubwa zaidi au aliyebora zaidi kuliko mwengine. Tofauti ndogo tu kuna Wajumbe ambao wametoka Majimboni, kuna Wajumbe wa kuteuliwa na kuna Wajumbe wa viti maalum na Mwanasheria Mkuu ambaye ameteuliwa na Rais vile vile. Lakini kimsingi kwa mnasaba wa shughuli hizi Wajumbe wote wako sawa na kwa hivyo wapate fursa sawa za kuuliza maswali mengine.

Kwa hivyo, Ofisi ya Katibu itazingatia kuona kwamba kila mjumbe aliyeuliza swali basi majibu yake yapatikane kufuatana na muda uliopangwa. Nadhani sasa tuendelee.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria wa Maadili ya Viongozi wa Umma na Kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Nimepewa taarifa kwamba majadiliano yalimalizika na leo ni siku ya kuomba Mhe. Waziri kufanya majumuisho. Naomba basi nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi wa Rais Ikulu na Utawala Bora.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi wa Rais Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa niwasilishe au nifanye majumuisho ya michango mbali mbali ya Waheshimiwa Wajumbe waliopata fursa yakuuchangia Mswada huu unaohusu Maadili ya Viongozi wa Umma na Kuanzisha Tume ya Maadili pamoja na Mambo Yanayohusiana nayo.

Mhe. Spika, naomba nitangulize shukurani zangu za dhati kabisa kwa Waheshimiwa wote waliopata fursa kuchangia hapa ukumbini na mmoja alipata fursa kuchangia kimaandishi. Lakini vile vile wengine kwa utulivu wao mkubwa na hamu ya kuusikiliza na kuuchangia, ni imani yangu kwamba wangependa na wao wachangie Mswada huu muhimu sana katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kubwa ninalotaka kusema kwamba *spirit* au muelekeo ambao Waheshimiwa Wajumbe niseme takriban wote wameonesha ni kwamba lazima tubadilike na wameafiki mtizamo wetu wa suala zima la utawala bora katika nchi yetu.

Mswada huu ni moja wapo katika muelekeo huo wa utawala bora. Nafikiri kwa ufupi tu Madhumu na Shababu tulisema kwamba kutungwa kwa Sheria ya Rushwa na Uhujumu Uchumi baada ya kutungwa Sheria hiyo serikali imeamua kuwasilisha Mswada huu ambao utasimamia maadili ya Viongozi wote hapa Zanzibar na kwa kuanzia kwa hawa waliotajwa kwenye jaduweli la pili la Mswada huu.

Mhe. Spika, mimi naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, niseme kukubali kwamba Mswada huu uletwe na ni imani yangu kwamba tutaupitisha kwa nguvu moja ili hili suala zima la utawala bora ambalo serikali yetu imeliona linaumuhimu wake katika jamii yetu na hasa tukiwa sisi kama viongozi ambao tunapaswa tuoneshe mfano, tuwe kiyoo cha utendaji wetu, basi serikali imehisi tuanzie hapa kwa sisi.

Mhe. Spika, kwa jumla kulikuwa kuna Waheshimiwa 18 waliopata fursa ya kuchangia Mswada huu. Wajumbe 17 liwachangia hapa ukumbini na Mheshimiwa mmoja alichangia kimaandishi. Naomba sasa niwataje kwa kuwatambua mmoja baada ya mmoja wale waliochangia:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali
3. Mhe. Subeit Khamis Faki
4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
5. Mhe. Saleh Nassor Juma
6. Mhe. Hamad Masoud Hamad
7. Mhe. Hija Hassan Hija
8. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
9. Mhe. Fatma Mbarouk Said
10. Mhe. Asaa Othman Hamad
11. Mhe. Muhammed Haji Khalid
12. Mhe. Hassan Hamad Omar
13. Mhe. Ashura Sharif Ali
14. Mhe. Omar Ali Shehe
15. Mhe. Salma Muhammed Ali
16. Mhe. Panya Ali Abdalla
17. Mhe. Ali Mzee Ali

Naomba kuutambua mchango wa Mwenyekiti wetu wa Baraza naye ni

18. Mhe. Mgeni Hassan Juma

Tunamshukuru sana kwa mchango wake, najua alikuwa kitini lakini angekuwa ukumbini naamini na yeye angejumuika na waliochangia kwa mdomo.

Mhe. Spika, sisi tumefarijika sana kwamba Waheshimiwa wametoa michango ya kuuendeleza Mswada huu baada ya kuona mantiki nzuri ya Mswada huu. Kama wengi walivyosema au walijiuliza kwanza je, tutaweza?

Sisi tunasema kama serikalini tumeshajipanga na tutaweza. Muhimu tanaomba sana mashirikiano yenu Waheshimiwa huu Mswada baada ya kupitishwa kama walivyoshauri waheshimiwa wengine, tutafanya semina na taaluma nzito kwa hao waliotajwa na wengine wajue nini madhumuni hasa ya sheria hii.

Mhe. Spika, hii sheria sio madhumuni yake kutafutana, sio kujua nani ana mali gani, hapana. Sheria hii ni kwenda na mwenendo mzuri wa viongozi sote. Kama nilivyosema wananchi kwa jumla lakini lazima tuanzie mahala. Ndio tukasema tuanzie kwa hawa viongozi waliotajwa kwenye sheria hii.

Mhe. Spika, Waheshimiwa wengi walizungumza historia, tulikotoka, matatizo tuliyokumbana nayo, tumekwenda vipi, tukabuburushana kidogo, tukenda hivi, tukenda hivi. Sasa ndio tunasema kweli baadhi ya watendaji wetu lazima tukiri, kweli katika watendaji wengine labda walikiuka maadili, walikwenda kinyume na taratibu, walikwenda kinyume na sheria, sasa tunapiga mstari, tunasema hawa viongozi wawe na chombo cha kuwasimamia. Haidhuru serikali ilikuwepo inayosimamia lakini serikali kubwa, mambo mengi.

Sasa kuwe na chombo moja kwa moja wananchi wanakijua, vipi anaweza kwenda kumshtaki Mheshimiwa fulani kwamba hatendi vizuri. Hayo ndio madhumuni hasa kwamba wapi apeleke malalamiko yake kama yupo kijijini, Shehia, Wilayani, wapi apeleke malalamiko tena kwa fomu maalum analalamika kwamba bwana kiongozi fulani anafanya hivi hivi hivi. Sasa chombo hiki ambacho Tume ndio kitaingia kazini sasa kuyachunguza yale yaliyosemwa, wao hawatoi hukumu.

Naomba Waheshimiwa mtufahamu vizuri, wao sio chombo cha kutoa hukumu. Wao watayachunguza sasa yale maadili kayakiuka huyu mtu. Kama kakiuka maadili sasa, mamlaka husika aliyonayo yule Ofisa ndio itamuhukumu.

Mhe. Spika, juzi nimesikia wazi wazi Mhe. Kikwete katika suala zima la *Escrow* alitamka Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Nishati, kamuachia *Chief Secretary*, Waziri wale kasema Kamati ya Maadili itasema. Walipoona tayari, basi wakashauriwa kwamba wajiuzulu, ama yeye mwenyewe akawawajibisha, huo hasa ndio utaratibu. Kwa hiyo hii ni kama Kamisheni ya Kuchunguza na kutizama maadili yale kweli kayafanya, kayavunja. Naomba sana Waheshimiwa hapa tuifahamu hii *concept* yenyewe. Kwa sababu tukifikiria kwamba watu wakitangaza mali atatizamwa kajaza mali. Hapa hilo sio lengo letu, huo ni utaratibu tu utawekwa.

Mhe. Spika, suala la msingi ambalo naomba sana Waheshimiwa, wengine waliimba nyimbo hapa kwamba sheria, sheria, sheria. Hilo ndilo suala la msingi sana. Sasa zile sheria lazima tuzitekeleze ipasavyo. Waheshimiwa walizungumza kwamba tumekuwa tunatunga Sheria lakini zinakuwa hazitekelezeki. Hilo sio lengo la serikali, lengo la serikali kutunga sheria ambayo inatekelezeka, kama kuna matatizo ya utekelezaji basi tu- *review* hiyo sheria.

Wenzetu Bara Kamati walikwenda wakaona kweli wanayo na wameona tatizo la utekelezaji wake. Kwa hivyo sasa hivi wana *review* wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Sheria hii, kuona vipi wanaweza wakaifanya iwe bora zaidi.

Mhe. Spika, halafu kwa jumla naomba sana Waheshimiwa bora niseme mapema hili. Pale tunasema Waziri anaweza au Rais anaweza, wengi wametushauri kwamba tuseme atafanya au atafunga. Yaani kwa lugha ya kisheria wanasema anaweza hatusemi *shall,* ukisema *shall* kama unamlazimisha. Haidhuru ni wajibu wake, kwa hiyo yeye anatarajiwa afanye. Lakini ukisema *shall* kama maana yake unamlazimisha. Kwa hiyo naomba sana Waheshimiwa pale wingi tuliposema anaweza tuichukulie hivyo.

Mhe. Spika, naomba niishukuru sana Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kwa marekebisho waliyoyafanya. Mhe. Mwenyekiti mwenyewe, Mhe. Hamza Hassan Juma maelezo aliyoyazungumza kwa kweli sote tumeyakubali na tumeyapokea. Kwanza marekebisho ambayo yametajwa pale na marekebisho mengine ambayo kwa kweli kama kwenye kifungu Namba. 15, 17, tumeyachukua na tutayafanyia kazi.

Pia, kwa ujumla niseme Waheshimiwa wengi walitushauri hapa na pale. Mhe. Ismail Jussa mbali ya michango aliyoitoa hapa katuletea michango ipatayo 30 kimaandishi, tena mengine ya maneno kisheria. Sisi wengine sio wanasheria lakini tumekaa tumeona mengine kwa njia moja au nyengine yametajwa. Lakini mengine nitamuuomba baadae kwa sababu ni uwandishi na *translation* labda kutoka Kizungu kuja kiswahili. Ili tubadilishane mawazo zaidi kwa lengo la kuiboresha sheria hii. Kuliko kwamba tutajibu hapa yeye atasema hivi naona hatutofika mahala. Lakini tu-*save* muda, sisi tuko tayari.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako baadaye tukae naye, kwa sababu ana michango mingi, zaidi ya 30 na *Alhamdulillahi* katuletea na tumeifanyia kazi yote. Lakini sasa mengine tafsiri, ukisema *against* kwa kizungu sisi tumefikiria hivi, labda yeye atafikiria vyengine. Sasa mimi nitamuomba baadaye kwa michango yake ambayo ni mizuri *constructive.* Lakini ni bora tuje tukae tubadilishane mawazo. Halafu haikugusa sana *substance* ya ule Mswada wenyewe zaidi ni uwandishi tu. Ile iliyogusa *substance* tumeigusa na tutaitolea maamuzi.

Mhe. Spika, kama nilivyosema Mhe. Mwenyekiti, tunamshukuru sana kwa yale aliyotuelezea, aliyotushauri, aliyotuelekeza na hiyo ndiyo hekma ya Uenyekiti. Alishauri kwamba ni vyema ifanyike semina kwa wahusika wote. Ni suala zuri na tumelichukua. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, wa Tume apewe ulinzi kamili. Hilo ni kweli na ni jambo la busara, huyu mtu atakuwa anatizamwa na anafuatiliwa. Halafu pia alituomba kwamba angefaa tufanye kama *study tour* au twende tukajifunze kwa wengine huko nchi za nje walivyofanya wenzetu waliowahi. Hilo tutalizingatia kwa kushirikiana na Ofisi yako Mhe. Spika, tuone kwamba tunalitimiza vipi.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kamati yake tunawashukuru sana pamoja na wenyeviti wengine waliokuja ku-*join force* kutia nguvu, kwa kweli wametusaidia sana wote tunawashukuru kwa pamoja kama alivyosema mwenyewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli juhudi zao za pamoja maana ule mswada mwanzo ulionekana kama unatisha, lakini hapa baada ya kuchambuliwa vizuri umeonekana kweli ni mswada wa kawaida. Lakini kama viongozi inatupasa tuwajibike, inatupasa tubadilike sasa utendaji wetu, *mind set* sasa twende kwenye utawala bora.

Mhe. Raza na yeye tunamshukuru alizungumza kwamba kwenye kifungu cha 28 ushahidi utakaotolewa mbele ya Tume unaweza kutumika kama ushahidi mahkamani? Sisi tunasema kwamba inategemea na sheria inayoongoza, kama sheria imeeleza basi tutajitahidi itekelezwe kwa sheria hii, ushahidi wake utatumika mahkamani.

Mhe. Raza alizungumza sana pia suala la madeni, tunachosema tu kwamba Serikali haioni tabu kukopa na Serikali yoyote inakopa ulimwenguni wala usione haya. Lakini suala muhimu ni kulipa na kadiri uwezo ulivyo yanalipwa maana tusingekuwa hapa wengine wanatusamehe. Kuna misaada ya ki-*Multilateral,* ya *Bilateral* ya nchi na nchi, wengine wanafika mahala mpaka riba wanasamehe zile mwisho wanaufuta kabisa madeni au mikopo. Tunachoomba sana madeni yahakikiwe na tuyaone kwamba kweli yana ukweli na basi yakisha hakikiwa hakuna tatizo, mazungumzo yataendelea yatalipwa, hilo halina ubishi Mhe. Spika.

Mhe. Subeit kwa kweli tunakushukuru sana ni mjumbe wa Kamati umezungumza mengi sana na maudhui ulioulizo kama walivyouliza waheshimiwa wengine je tutaweza. Nasema tutaweza kitu muhimu nia. Uwezo muhimu nia na *commitment na dedication* sote tukubali sasa kwamba tubadilike, *mind set* zetu tujibadili twende kwa mujibu wa taratibu, kwa mujibu wa sheria, huo ndio utawala bora wenyewe huo.

Kwa hivyo, nasema Mhe. Subeit kwamba tutaweza. Ulizungumza mifano mingi huko ya Zan ID na nini na nini lakini tunasema mote humo kuna taratibu zake, kukitokea tatizo imeelekezwa ifanywe nini. Kwa hivyo, mimi ningeomba sana tujielekeze kwenye ule utaratibu uliowekwa katika utekelezaji wa hizo sheria.

Umeshauri pia kwamba Tume iwe na bajeti kubwa kwa sababu kazi zao zinahitaji ufuatiliaji, tunaukubali ushauri wako, tumeupokea na tunategemea keki tutakayopata, lakini tunaiomba Serikali kwa hili na hasa ilivyokuwa chombo kipya basi inafaa kwa kweli tupate bajeti nzuri.

Mhe. Makame Mshimba tunakushukuru na wewe ulizungumza mengi kabisa lakini ulitaka kujua kwamba sheria hii itakapopita itaifanyia kazi kamati nyengine au mambo ya nyuma? Tunasema la, sheria hii haitokuwa *retrospective* haitochukua mambo ya nyuma baada ya kumaliza Mhe. Rais kuisaini pale ndio itaanza kutumika. Lakini lile suala fomu sasa anapojaza kila mtu anatakiwa ajaze fomu atangaze mali zake, sasa utakapotangaza mali zako ndio utafuatiliwa pale. Mbona mwaka huu Mhe. Mshimba tumeona ghaflla mwaka huu una nyumba mbili una gari tatu, mwakani umeseme una nyumba tano, una gari 12, sasa pale kidogo ndio patatisha. Sasa ule ufuatiliaji ndio utaonesha kuwa mwenendo wako vipi kama kiongozi wa kutia shaka japo si vizuri kutia shaka lakini ndio mwenendo utakavyokwenda lakini huko nyuma tena la.

Jengine labda nigusie tu kwamba labda imeonekana kwamba zile kamati zilizofanya kazi kama Serikali imezidharau, hata kidogo. Mhe. Spika, ninakuhakikishia kwamba ripoti zote za kamati tumezijadili Serikalini kwa undani wake, tumekaa kwenye Baraza la Mapinduzi chini ya Mwenyekiti wetu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tumezijadili (a) to (z) labda tofauti sasa yale yalopendekezwa kwenye kamati pengine sio mtizamo wa Serikali kwa sababu na wao tumewapa *benefit of the doubt* nao wajieleze, waone basi si lengo kwamba au tusiwe na mtizamo kwamba Serikali imezidharau lalala. Serikali imezijadili ripoti hizo na imekuwa makini na hatua zimechukuliwa, labda tofauti pengine waheshimiwa hamjajulishwa baadhi ya hayo masuala.

Kwa hivyo, Mhe. Makame Mshimba alizungumzia kama Serikali iko makini katika suala hili, niseme iko makini na tumejiandaa. Yeye kasema kwamba apelekewe Mhe. Rais autie saini mapema iwezekanavyo. Tunakubaliana lakini utafuata utaratibu ule uliowekwa ili mpaka Mhe. Rais naye aweze kuutia saini.

Alishauri kwamba wafanyakazi watakaoteuliwa wasitoke katika Taasisi za Serikali watoke nje katika majimbo, wilaya, ushauri wake mzuri tumeukubali tutauzingatia. Lakini pia tusisahau suala la uzoefu ni chombo kipya lakini tunahitaji watu wazoefu na sifa ambazo zimetajwa.

Ameshauri kwamba Tume iwe na vyombo vya usafiri, teknologia ya habari ya ICT na iwe na mamlaka kamili, ushauri wake ni mzuri tumeusikia na tumeupokea.

Naomba sasa nimgusie Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii inayosimamia viongozi wakuu Mhe. Saleh Nassor Juma wa jimbo lile la Wawi; yeye alitaka kujua kama kifungu cha 4 kinasema itaanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambayo itakua na Wakala wa Serikali, huo uwakala ukoje?

Uwakala huu wa Tume ni kuwa Taasisi sio wakala wa kumfanyia kazi zake Serikali, ni *authority,* ni wakala, ni Taasisi, tuseme inayotejitegemea kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma namba 2 ya mwaka 2011. Hiyo ninataka tumjulishe tu Mhe. Saleh, kwamba hii ni wakala itakayojitegemea kufanya kazi zake. Mheshimiwa ushauri alioutoa wote tumeusikia, tumeuchukua na tutaufanyia kazi.

Mhe. Hamad Masoud tunamshukuru na yeye kwa michango mizuri hasa aliulizia kifungu cha 7, kinasema "mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti...", nimesema lazima sifa gani na zimetajwa kwenye kifungu cha 7, awe mzanzibari na mwenye sifa ya kuwa ni Jaji wa Mahkama Kuu, hiyo imetajwa waziwazi akifungua kifungu cha 7 ataiona.

Pia, alisema makosa ya jinai bado yamo kwenye kifungu, aliuliza masuala ya kosa la jinai je, sisi tumesema tumeyataja kwenye sheria hii makosa ya jinai, bado yamo kwenye kifungu cha 7(3)(c). Na tunasema kwamba mtu aliyetiwa hatiani na mahkama au na chombo chengine chochote cha kinidhamu kwa makosa ya uadilifu au uaminifu, mtu huyo hatofaa kuteuliwa kuwa mwenyekiti. Hilo liko wazi kabisa. Lakini pia aliuliza kwa nini isiwekwe na mtu ambaye amefanya kosa la jinai kama alivyosema hii, tusiyapangue makosa haya yaliyotajwa kwenye 7(3)(c), yamo ya jinai na yapo ya maadili. Sasa tukiyaweka ya jinai peke yake tuta-*under rate* yale mengine. Kwa hivyo mimi ningeshauri sana akisome vizuri kifungu cha 7(3)(c) kimetoa ufafanuzi mzuri.

Uwezo pia wa kumfanya mwenyekiti kuwa huru katika kutoa maamuzi kipengele hiki kimeongezwa maneno rushwa na uhujumu wa uchumi na tumekubali tumefanya marekebisho katika kamati.

Vile vile, aliuliza kwamba mwenyekiti amepewa uwezo kushinda Rais? Si kweli mwenyekiti mamlaka yake si kama ya Rais, Rais ni mmoja tu wa nchi hii na yeye ana mamlaka kamili ya nchi hii. Isipokuwa tu kwamba kwa Tume yeye ndio *authority,* yeye ndio lazima tumpe mamlaka na lazima tufahamu waheshimiwa kwamba huyu ata-*deal* na viongozi hawa wote tuliorodhesha. Ni viongozi kwa hivyo lazima na yeye aliyekuwa Jaji wa Mahkama Kuu mwenye sifa hiyo, kwa hivyo lazima na yeye awe na *authority,* awe na nguvu ku-*deal* na wakubwa asije akayumbishwa au asije akatikiswa tikiswa. Kwa hivyo, awe madhubuti na asimame kidete kutetea hoja zake.

Mheshimiwa alishauri kwamba iongezwe kauli chafu na atakaechochea chuki, hiyo ninafikiri imo imesemwa hiyo wazi kwamba kiongozi lazima asiwe na yeye na kauli chafu na kutetea chuki. Kifungu cha 21 kinaeleza kwamba waziri anaweza kutunga kanuni kwa utekelezaji mzuri wa sheria. Kifungu kinaelezea Mwenyekiti na Makamishna na sio Naibu Kamishna, tumefanya marekebisho pale ile Naibu Mwenyekiti imefutwa ni Mwenyekiti na Makamishna.

Mhe. Spika, pia alishauri waziri alazimike kutunga kanuni na isiwe jambo la hiari ndio pale niliposema kwamba tusiseme *shall* lazima kwa taratibu iwemo.

Kifungu cha 43 kinaeleza kutangaza mali kwa Mwenyekiti na Kamishna, na yeye atatangaza kwa sababu na yeye yumo kwenye orodha, atatangaza na utaratibu utawekwa vipi na yeye atatangaza na kuchunguzwa, hawezi kukiuka utaratibu na yeye pia yumo.

Kifungu cha 7 Mhe. Hamad Masoud na alielezea kila kiongozi wa umma aheshimu, asaidie na atekeleze maamuzi ya mahkama; ile mahkama maalum ikiwa ni pamoja na mahkama ya viongozi. Tumefuta pale ile haimo na katika marekebisho ya Mwenyekiti waheshimiwa pale tumewafuta, ipo wazi kabisa kwamba tumeishia mahkama.

Katika jaduweli la kwanza kifungu cha 1(19)(a) amependekeza neno 'uaminifu' liondoke liwekwe neno 'uadilifu'. Sisi tumeongeza tumesema tuliondoe 'uaminifu' ubaki lakini na 'uadilifu' tumekubali ushauri wake kwamba tumetia.

Mhe. Hija Hassan Hija wa Kiwani, Mheshimiwa alizungumza mengi alitoa ushauri mwingi tumeyazingatia na mengi niseme ya kufanyiwa kazi. Kifungu 18(1) kuzingatia miko ya kijamii, ulevi wa kupindukia, ile tumefuta ukiangalia marekebisho ya Mwenyekiti suala zima la ulevi limefutwa. Lakini kifungu cha 7(3)(b) sifa za Mwenyekiti asiwe mtu aliyetangazwa kuwa amefilisika. Tunaposema mtu amefilisika ni kimali sio kisiasa au aina nyengine yoyote ya kufilisika. Kwa hivyo hapa zaidi ni kimali, ameuliza mtu huyu kafilisika vipi.

Halafu tulizungumza suala la adhabu, adhabu iliyowekwa katika kifungu cha 32 iwe kubwa kuliko ile ya kifungu cha 31. Sisi kwa mtizamo wetu katika Wizara tumehisi kwamba kutoa siri ni kosa kubwa zaidi kuliko kusema uongo na hizo adhabu hazikupishana sana. Lakini tumeona hii ya kutoa siri ni kubwa zaidi tena kwa mfanyakazi. Kwa hivyo tumeona bora tuweke adhabu kubwa kwa mfanyakazi lazima adhibiti siri, akizitoa siri kwa kweli aadhibiwe ipasavyo. Kwa hivyo tunakuomba sana Mhe. Hija utukubalie mantiki yetu kwa nini tumeona bora adhabu ile ya kutoa siri iwe kubwa zaidi.

Mhe. Hija ulizungumza mengi lakini kama nilivyosema kwa sababu ya muda naomba niishie hapo, lakini mengi uliyoyasema, uliyoyashauri tumeyasikia na tutayasimamia ipasavyo.

Mhe. Jussa kama ulivyosema alipata nafasi ya kuchangia ukumbini Mhe. Spika, baadae pia alipata nafasi ya kuleta kimaandishi mambo yasiyopungua 30. Mambo ya kisheria, mambo mengi madogo madogo lakini yana mantiki. Sasa naomba niyapitie haraka haraka, ni mengi kama nilivyosema bora nitamuomba baadae tuje tukae kwa sababu kuna mengine ya *translation,* ili tuje tufanikishe vizuri hili suala letu. Lakini kubwa anasema mswada wa kiswahili una majaduweli mengi wakati ule wa kingereza hauna baadhi ya majaduweli. Sasa hilo tunakubali, kweli wakati wa kutafsiri tulifanya haraka kidogo ili mswada tuuchapishe ndio maana baadhi ya majaduweli hayakuwahi kutafsiriwa kwa kingereza. Hilo tutalifanya, ushauri wake huo tumeusikia.

Mswada alisema hautoi fursa kwa mlalamikiwa kukata rufaa baada ya maamuzi ya Tume, tunachosema kwamba kuna fursa ya kwenda Mahkamani iwapo mlalamikiwa hakuridhika na maamuzi, na hii ni fursa ya kikatiba hata sheria hii fursa hii hiyo pia inayo.

Pia, Mhe. Jussa anasema vifungu vingi vimempa mamlaka Mwenyekiti, anayesikiliza ni Tume au Mwenyekiti? Dhamana wa Tume ni Mwenyekiti na yeye ndie hasa anayesikiliza kesi, wale Makamishna ni wasaidizi wake lakini pia kuna wafanyakazi wengine ambao ndio wanaunda hiyo Tume, sio kwamba watu watatu tu hao, pia kuna wafanyakazi wengine.

Kwa hivyo, nakumbuka Mhe. Salma alisema kwamba Tume ni ndogo, kweli ni ndogo hiki chombo muhimu na kinabidi kifanyekazi ipasavyo, kwa hivyo kuweka watu Tume kubwa ikawa hawana kazi si jambo la busara, tuangalie muundo wa Tume tumeweka wazi tumeelezea hasa aina gani ya hiyo Tume iwe.

Mhe. Jussa, alisema pia jaduweli la kwanza mahkama maalum ya viongozi kifungu cha 5(b) kwenye jaduweli la kwanza kimefanyiwa marekebisho na sasa kinasomeka; "aheshimu, asaidie na atekeleze maamuzi ya Mahkama na Mahkama Maalum". Kama nilivyosema tumerekebisha hii.

Kifungu cha 27(1) mswada haukuzingatia haki ya kusikilizwa kwa mlalamikiwa. Sisi kwa mtizamo wetu tumesema kwamba hakuna kusikilizwa tena kwa sababu atakuwa ameshasikilizwa kwenye Tume, haki aliyonayo ni kukata rufaa na kukata rufaa hiyo baada ya adhabu kutoka sasa hapo tena atakata rufaa kama taratibu za kikatiba za nchi za kisheria zinavyosema. Lakini kwamba arudi tena kwenye Tume itakuwa kama tunarudia kazi mara ya pili ambayo kwa kweli tunahisi si busara.

Zawadi iweke kiwango cha kupokea baina ya mtu binafsi na kiongozi, ushauri wake tumeusikia, tutajitahidi tutaweka katika Kanuni kile kiwango. Kiwango gani cha zawadi kiwe *acceptable* ambacho hicho apokee na hiki kibaki kwa taasisi. Ni ushauri wake mzuri tumeusikia.

Kifungu cha 22(4) ushauri kwamba daftari la kumbukumbu za mali liwe wazi kwa watu wote, hapa kidogo Mhe. Spika, sisi tuna mtizamo mwengine; unajua daftari lile watu watakuwa wanaelezea mali zao, siri zao, sasa kuonekana na watu wote kwa kweli si jambo la busara. Wataona wale wahusika watu wa Tume hata waziri akitaka na yeye aombe ruhusa, na yeye pia hayuko *accessible,* nalo lazima aombe ruhusa. Maana yake tusilinganishe labda na daftari la wapiga kura kwamba linawekwa kila mmoja akaangalie aa, hili tofauti. Hii ni mali za watu, sasa

kuziweka *open* kwa mtu yeyote akachungulie aa, tunafikiri tutawasha moto ambao kwa kweli haustahiki, huo ndio mtizamo wetu Mhe. Spika.

Jaduweli la pili anasema tuangalie kumuingiza sheha na diwani katika mswada. Kwa kweli Mheshimiwa tumelitafakari sana hili tumeona kwamba kwa hivi sasa bora tuachie hapa hii orodha, kwa kuanzia tuanzie hapa kwa sababu kuna watu wengi ambao wana dhamana muhimu kama walimu wakuu, tukisema nao tuwaingize kwenye huu mswada na kuna wengine, lakini tuanze hapa baadae kadiri tunavyokwenda tutaona.

Halikadhalika waheshimiwa wengine walishauri madiwani na hata wenyeviti wa halmashauri tunahisi kwamba aa, kwa sasa hebu tuanzie hapa tuone. Kwa sababu tukifikiria wote hawa na ukitizama level kimapato halali ambayo fursa za sheha kisheria ni mshahara ukilinganisha na hawa ni tofauti kubwa sana. Sasa sisi kwa mtizamo wetu tunasema tuanzie hapa kwanza, lakini kanuni iko wazi wakati wowote ikifika haja basi waziri anaweza akashauriwa kuingiza watu wengine.

Kifungu cha 3 jaduweli la kwanza alitoa pongezi tunazichukua suala la Umoja wa Kitaifa yote hayo tumelipokea na tumeyasikia.

Kifungu cha 2 sheria hii itatumika kwa viongozi wote waliotajwa kwenye kifungu hiki au inayohusu waliotajwa kwenye jaduweli la pili tu? Sheria hii itatumika kwa waliotajwa katika jaduweli la pili. Pale mwanzo tulisema kwa ujumla ujumla lakini *specificaly* wametajwa kwenye jaduweli la pili.

Kifungu cha 7(3)(c) kinahusu jinai na madai vile vifungu viko aina mbili; pale wanaohusu mambo ya jinai na madai. Sasa tumeona tuyafanye *separate* kabisa ili kuweza kutafautisha.

Lakini vile vile, kifungu cha 8, nini, nafasi, uwezo na kazi za Kamishna. Tumesema wazi wazi kwamba Makamishna wao watakuwa wasaidizi, yaani watakuwa kazi yao kumsaidia Mwenyekiti katika kuendesha kazi za Tume. Na imesemwa wazi wazi kwamba wao ni wa muda, si wa kudumu kwa muda wote, hao ni wasaidizi wa Mwenyekiti na si lazima wawe wanasheria, kwa mfano Tume ya Marekebisho ya Sheria.

Kifungu cha 9, kwa nini sifa iliyotajwa kwenye kifungu cha 7 (1) (b) kisiowahusu Makamishna kwa chombo kama hiki? Kama nilivyosema mwenye dhamana ya chombo ni Mwenyekiti ambaye tumesema lazima awe Jaji wa Mahakama Kuu, wale wengine si lazima tuwaachie. Lakini sifa zile nyengine ukiachia hiyo ya kuwa Jaji Mkuu, sifa zile zote zika-*prevail* zile, yaani zote zikafanya kazi.

Kifungu cha 12, 13 na 14, pia kifungu cha 14 mamlaka ni ya Tume kama taasisi ikiwa ni pamoja na Kamishna au ni ya Mwenyekiti kama kiongozi wa taasisi? Pia, tumesema ni jukumu la Mwenyekiti au ya Tume? Mamlaka ni ya Mwenyekiti ambaye ndiye kiongozi wa taasisi ambapo Makamishna ni wasaidizi wake. Kimsingi vifungu hivi vya 16 (1) (a) na (c) yake cha sheria. Kifungu kingine kumradhi ulioulizia suala la riba na kwenye akiba.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwa mtizamo wetu kwamba kama shamba lile au kwenye akaunti yeyote kuna *principal* na *interest*, sasa hiyo lazima vitaufautishe, hata wewe ukienda kutizama unaona duh! Nimeweka pesa hii baada ya muda riba iliyoingia ni hii. Kwa hiyo, vile lazima hiyo kwenye *statement* ile inaonesha wazi wazi, kwa hiyo, tumeona tukichanganya pamoja si jambo la busara, bora tuitenganishe na mtu yeyote itaonekana wazi kwamba duh! Mwaka fulani kumbe aliweka milioni moja baada ya muda iko milioni 1.5 au 1.6, kwa hiyo, ni vyema itafautishwe.

Lakini pia, ulizungumza kwamba kifungu cha 16 (1) (e), sisi kwa mtizamo wetu kifungu 16 (1) (e), kulikuwa na makosa katika tafsiri kizungu kwenda kiswahili, nafikiri kidogo haiko vizuri. Hilo tunakiri tutatafsiri tena tuone tunaipata *correct version* kwa kiswahili, kidogo tuliitafsiri moja kwa moja kama neno kwa neno. Kwa hiyo, tutashirikiana na Ofisi ya Mhe. Mwanasheria Mkuu, tuone tunapata *correct translation* ya kizungu, ambayo ya kizungu imekaa vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa upande wa 16 (1) (f), mashamba yanayoendeshwa kibiashara, kwa nini yasiwe mashamba yote yanayoendeshwa kibiashara tu? Katika kifungu hiki yatafanyiwa marekebisho ambapo mashamba ya kibiashara na yasiyokuwa ya kibiashara yatatajwa. Tumeona kweli tusichanganye ya biashara yawe mbali na yale

yanayomletea tija yule mtu mwenyewe kwa kula tu (*subsistence*) peke yake mwenyewe yawe mbali. Kwa hiyo, tutajitahidi kuweka sawa hilo.

Mhe. Spika, kifungu chengine cha 16 (1) (g), kwa nini isiwe mali zote? Yaani pale kuna manufaa na sio faida, tutafautishe *beneficial* na *profit*. Sisi mtizame wetu kwamba lazima tutafautishe na tumerekebisha kwamba sio faida, ile ni kwa manufaa yake.

Kifungu cha 16 (2), Waziri asipewe mamlaka kwa sheria kama hii pawepo na mtu ambaye atakabidhiwa majukumu kwa mujibu wa sheria hii. Waziri ndio atakuwa na wajibu huo, lazima awepo mtu mwenye dhamana haiwezekani kwamba iwe hakuna mtu, mbali ya Mwenyekiti lakini lazima kuwe na msimamizi mkuu. Na mtizamo wetu kwamba waziri ndio atapewa jukumu hilo.

Kifungu cha 17, kuna mgongano wa kimaslahi katika kutangaza haya maslahi. Sasa mtizamo wetu ni kwamba anatakiwa kumuarifu mkubwa wake pale panapo migongano ya kimaslahi ili aweze ku-*declare,* sio ku-*announce* kwenye vyombo vya redio, aah, aweze ku-*declare* kwamba mimi nilichonacho ni hiki na hiki *immediately boss* wake awe ndio kama hivyo itakuwa msimamizi wake.

Kifungu cha 20, nini tutaje baadhi tu ya maadili wakati kilikiuka kifungu chote cha sheria hii ni kuvunja maadili? Kwa sheria hii kuna vifungu vya jumla (*general*) na vyengine ni mahususi (*specific*).

Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyosema Mhe. Jussa, ana mengi sana ya aina hiyo, kwa hiyo, ningemuomba sana anikubalie tumeyafanyia kazi yote hatukuacha hata moja, lakini sasa tukianza atauchukua muda wako mwingi sana Mhe. Spika. Mimi ningemuomba sana Mhe. Jussa, baadae tukae pamoja kwa lengo la kuifanya sheria hii iwe nzuri zaidi tubadilishane mawazo yeye kama Mwanasheria.

Labda moja tu nitalisema lile kwenye kifungu cha 18 kuhusu mawasiliano bila ya kificho, ayatafsiri sawa sawa neno la kiingereza "*interacting"* ndio kama haya. Kwenye kizungu kuna *interucting* na sio tulisema mawasiliano bila ya kificho na yeye kakubali kwamba aah! Mbona halioneshi kweli. Ndio hayo ninayosema, sasa yapo kama haya, wacha tukae pamoja tutizame pamoja na Ofisi ya mwenyewe Mhe. Mwanasheria Mkuu ili tuone vipi tunaweza tukaweka sawa.

Mhe. Spika, naomba sasa nimguse Mhe. Fatma Mbarouk wa Amani…

Mhe. Spika: Tuzingatie muda, leo ni siku ya Ijumaa, tuzingatie muda ili tuweze kumaliza shughuli hii ya kupitisha vifungu kipindi hiki.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Ahsante nakushukuru sana.

Mhe. Fatma, tunakushukuru kwa pongezi na pale ulipotusisitiza kwamba taratibu za kisheria hasa maamuzi ya Kamati nayo yatekelezwe nimeshazungumza na pia, ulizungumza suala la matumizi ya “anaweza” na “ataweza”.

Lakini umesema kifungu cha 41, Waziri anaweza na iwe ataweza nayo hiyo tumeshaizungumza, lakini kwa ujumla umetushauri, umetuelekeza na yote hayo kwa ujumla tumechukua michango yako.

Mhe. Asaa…

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, si muda mkubwa tutapitisha vifungu niwaombe wanaotoka kwa dharura wakumbuke kurudi tuje tumalize shughuli hii.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Asaa, alizungumza vipi tutaipima nia njema? Nia njema kwa kweli Mahakama yenyewe ndio itakayoamua nia njema iweje, mwelekeo ule wao ndio wataona kwamba kweli kulikuwa na nia njema au kulikuwa na nia kidogo tofauti.

Nafasi ya Mwenyekiti ulisema itangazwe, kwa nafasi nyengine za kiutendaji ni utaratibu wetu tushaingia sasa nafasi zinatangazwa, lakini kwa hii ya uwenyekiti ambayo sisi mtizamo wetu kwamba lazima apatikane mtu mwenye maadili, uadilifu na sifa hiyo ya Jaji wa Mahakama Kuu ni wachache tu waliofika *level* hiyo. Kwa hiyo,

Mhe. Raism kama cheo kwa nafasi yake bila shaka hatoamua tu atashauriwa na washauri alionao na halafu atapima huyu anatufaa.

Mhe. Mohammed Haji Khalid, tunakushukuru umesema kwa nini Mhe. Rais kaingizwa katika sheria wakati hashtakiwi. Tumeamua kumuingiza Mhe. Rais kwa sababu utaratibu upo kikatiba wa kumuweza kumuajibisha Mhe. Rais na yeye ni mfano mzuri kwamba na yeye pia ajaze fomu na atajaza kipindi kile kama sisi tunapotakiwa tujaze na yeye atajaza, hiyo ndio na yeye anaonesha kuwajibika kwake. Nafikiri itakuwa ni kigezo kizuri kwetu kwamba hata Mhe. Rais, nae anajaza fomu.

Kiwango gani cha mali kichukuliwe na je, Tume ikinyanganya mali, itakwenda wapi? Pendekezo wameshauri kwamba mali ichukuliwe na kiongozi ashtakiwe.

Kazi ya Tume kama nilivyosema si kutoa adhabu wala sio kunyanganya mali. Tume hii inatoa maamuzi ya uvunjaji wa maadili. Kazi yake kuchukua hatua za kinidhamu yenye mamlaka husika, itakapotokea mali zimechukuliwa taratibu za kisheria zitafuata.

Mhe. Omar Ali Shekhe na wewe tunakushukuru pia kwa michango yako na hasa uzoefu wako katika Kamati ile ya *PAC* na hasa ufafanuzi uliotoa katika ukurasa wa 54, suala zima lile la mali. Sisi tunasema kwamba mali huku mwanzo ndio imeelezwa kwenye ufafanuzi wa maneno yaliyotumika, kwa hiyo, kuipeleka kwenye kifungu cha 16, si barabara, kifungu cha 16 ndio matumizi yenyewe ya lile neno "mali" linatumika vipi kule. Na kwa sheria hii kuitafsiri mali ina maana gani? Kwa hiyo, ukisoma ukurasa wa 54 ndio *translation* yenyewe hasa, fasili yenyewe mali kwa sheria hii iweje?

Lakini umezungumza pia waziri kupewa mamlaka ya kifungu cha 16 (2), kwa vile thamani ya mali zinabadilika kwa wakati ni vyema Mhe. Waziri apewe kwa sababu thamani ya mali leo tofauti na baada ya miaka miwili. Kwa hiyo, lazima kuwe na *flexibility* yeye kama waziri kuweza kuongeza au kupunguza.

Tatu, waziri asipewe fursa kuliona daftari la kumbukumbu. Kama nilivyosema waziri nae hana ruhusa, Mhe. Waziri anatoa ruhusa tu na akitaka kuliona anafuata taratibu, yeye pia haruhusiwi moja kwa moja kuliona. Haruhusiwi kabisa na yeye akitaka basi lazima afuate taratibu.

Kifungu cha 34 (2) na 37 (1) kirekebishwe, tumekubali ushauri wako uende na taasisi nyengine za kiserikali wakati wa kufunga hesabu na kutayarisha bajeti, kama taasisi nyengine za serikali basi na taasisi hii nayo au Tume hii ifuate taratibu tusi-*create* mpango mwengine.

Mhe. Salma, tunakushukuru na wewe kwa mchango wako umezungumza suala la udogo wa Tume. Tume sio ndogo kwani kama nilivyosema inajumuisha Mwenyekiti, Makamishna pamoja na watendaji wengine. Lakini umesema ulishauri kwamba kifungu 18 (3) kwamba tuongeze vitendo vya kibaguzi. Ushauri wako tumeusikia, kwa hiyo, tutaongeza.

Mhe. Panya Ali Abdallah, tunakushukuru, ulisema tusiwaonyeshe vidogo viongozi wengine tujiheshimu wenyewe na sisi tuwe msitari wa mbele, tuelewe wajibu wetu na tutumie vizuri kauli zetu na kwenye kifungu cha 18 (2) kuna maneno ya utapeli, wizi na ubakaji viondolewe vipelekwe 18 (1). Sisi tumesihisi kwamba ni vizuri vikabaki kama ilivyo kwani kifungu 18 (1) na vinahusu maadili na 18 (2) vinahusu jinai, ni tofauti kidogo bora tuviache kama vilivyo.

Mhe. Ali Mzee Ali, tunakushukuru sana kwanza kwa historia nzuri uliyoitoa na kumpongeza Mhe. Ramadhan Abdallah Shaban, kwenye Baraza la mwanzo la Wawakilishi, tunampongeza kwa ku-*maintain* mpaka hii leo.

Lakni vile vile, tunampongeza Mhe. Rais kwa kuwapatia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi semina ambapo moja kati ya mada zake zilizohusu maadili. Tunakushukuru kwa pongezi hizo na wasia wako mzuri na wasaa wa kutuwaidhi nini umuhimu na mtizamo wa serikali yetu katika suala zima la utawala bora. Tume ikishaundwa itawajibika kwa nani? Tume itawajibika kwa Mhe. Rais.

Mhe. Bi Ashura, tunakushukuru na wewe na utulivyotuelekeza yote katika kutekeleza sheria hii, tunasema lazima tubadilishe *mind set* zetu. Kwa kweli tunakubaliana na wewe na ndio mtizamo wetu na viongozi wote kwamba sasa tupige *blue print* kwamba aah! Sasa tubadilike jamani, tuwe safi, tufate sheria na taratibu za nchi.

Mhe. Mgeni Hassan Juma, tunakushukuru na wewe na pongezi uliotupa, ushauri na michango yako yote tumeipokea.

Mhe. Spika, narudia tena kusema kwamba michango ilikuwa mingi, mizuri, lakini yote yenye nia ya kufanya mswada wetu uwe bora zaidi. Kwa hiyo, tumeichukua, tutaifanyia kazi na wale walioandika kimaandishi kama Mhe. Jussa, tutamuomba sana tuje tukae pamoja na yeye na hasa aliyosema uchambuzi wake kuhusu maneno ya kisheria ili tuone kwamba tunafanya mswada wetu uwe bora vipi.

Mhe. Spika, kwa haya machache sasa. naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. sasa Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji basi wale wanaokubaliana. Kuhusu utaratibu Mhe. Ismail Jussa.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ili tuingie katika hatua hiyo Kanuni ya 72 inatuelekeza kwamba tujiridhishe kwamba idadi ya wajumbe waliomo ndani wanafikia angalau nusu au zaidi ya nusu ya wajumbe. Kwa hiyo, ningeomba tujiridhishe kabla hatujaingia hatua ya kufanya maamuzi, maana ukianza kutuhoji Mhe. Spika, kuanzia sasa tunaingia hatua sasa ya kufanya maamuzi.

Mhe. Spika: Ni sawa kabisa, wajumbe walioko nje waingie ndani haraka ili tumalize kazi hii, nilitoa hilo tangazo mapema ili tuweze kufanya shughuli zetu hizi kwa mujibu wa taratibu zetu. Tuwaite wajumbe walioko nje waingie ndani haraka, haraka sana. Watendaji kuna wajumbe wangapi hapo?

Waheshimiwa Wajumbe, walioko nje waingie ndani haraka sana ili tuweze kumaliza kazi hii na tuwe tunajitahidi kuzingatia kwamba tunapofika wakati wa maamuzi kama vile nilivyotoa tangazo wakati ule, wakati wajumbe wengine wanatoka nikasema kwamba wakumbuke kurudi kwa sababu kuna kazi ya kumaliza.

Wakati tunawasubiri wajumbe wengine kuna tangazo moja dogo.

Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti, anawatangazia wajumbe wenzake Wenyeviti wa Kamati zote mara baada ya kuakhirisha kikao hiki wakutano, yeye kasema humu ndani, lakini sio humu ndani ukumbi wa Kamati pale juu kuna mambo kidogo wakazungumza. Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti anawaomba Wenyeviti wenzake wa Kamati mbali mbali wakutane pale juu katika ukumbi wa Kamati kuna mambo kidogo washauriane. Nafikiri hayatochukua muda mkubwa huko ili wawahi shughuli nyengine za Ijumaa. Nafikiri sasa tumefikia pahala.

Waheshimiwa Wajumbe, basi sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, chombo chetu hiki ni kikubwa sana na wajumbe walioingia baada ya kutaka waongezeke wameingia wajumbe wawili. Kwa hivyo, hata ikiwa kwa sababu Mhe. Spika mpaka tulipohesabu mara ya mwisho tulikuwa ni wajumbe 33, kwa hivyo, bado tulikuwa na kasoro ya wajumbe wanane.

Kwa hivyo, bado Mheshimiwa chombo hiki kikubwa na kwa sababu tunafanya kazi kubwa ya kutunga sheria za nchi hapa, nadhani itakuwa si utaratibu mwema kufanya shughuli hiyo bila ya kujiridhisha kwanza kwamba tumetimia angalau nusu kama Kanuni zetu zinavyotaka.

Mhe. Spika: Makatibu hebu tuhesabu tena. Wajumbe tuweke nidhamu ya shughuli zetu hizi, tunaelewa ni wajibu wetu huu, tunatoka majumbani tunakuja hapa kwa kazi hii. Hesabu wajumbe walioko nje haraka sana waingie, mpaka tunapiga kura mara mbili, hapana. Nasithibitishiwa sasa wameingia 43 na wa 44 ni mjumbe mwenzenu niliyoko kitini hapa na mimi ni mjumbe.

Baada ya hayo basi tupige kura tena, wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar ya mwaka 2014

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake

Kifungu 2 Matumizi ya Sheria

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake wa baadhi ya hoja, isipokuwa labda niweke indhari kabla sijaingia katika nukta hii, kwamba utaratibu wa kusema baadae tutakaa pamoja, nadhani sio utaratibu sahihi. Kwa sababu sheria inatungwa na chombo hiki kupitia Kamati hii, sasa tukishamaliza hapa hatuwezi tena tukakaa pembeni watu wawili tukasema tunarekebisha sheria namna ilivyoandikwa. Kwa hivyo, nadhani tujiridhishe kabisa hapa Kanuni zetu zinavyoelekeza ili tuhakikishe kwamba tumetenda kazi yetu.

Baada ya maelezo haya mafupi, naomba niseme katika kifungu hiki cha 2 katika mchango ambao nilimpelekea wa maandishi wa vifungu vingi kama alivyokiri mwenyewe. Mimi nahisi kuna matatizo katika kifungu cha 2 na katika kifungu cha 3 kwenye maneno ya tafsiri ya kiongozi wa umma juu ya sheria hii inawahusu nani hasa. Kwa sababu ya uzito wa sheria hii, nadhani ni muhimu sana kujiridhisha kwa yale ambayo tunayapitisha.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu nini? Kifungu cha 2 kinasema; "Sheria hii itatumika kwa viongozi wote...", naomba tuzingatie neno "wote","...wa utumishi wa umma na utumishi wa kisiasa ikiwa pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na viongozi wa Mahakama, viongozi wote..." naomba tuiangalie tena neno "wote", "...wanaofanya kazi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au wanaofanya kazi kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndani au nuje ya Zanzibar".

Mhe. Mwenyekiti, sasa hoja yangu ambapo nasikitika Mhe. Waziri hakunitosheleza na sijakubaliana na maelezo yake, naomba chombo hiki kijiridhishe kabla ya kuendelea, ni kwamba ukisoma kifungu cha 3 ambacho kinatafsiri maneno mbali mbali. Hoja yangu iko katika viongozi wa umma, inasema kiongozi wa umma maana yake ni mtu yeyote mwenye dhaana kwa mujibu wa Katiba na Sheria nyengine yoyote ya Zanzibar na waliotajwa kwenye jeduali la 2 la sheria hii.

Sasa hoja yangu ni kwamba hapa tujiridhishe kabisa, sheria hii inahusu viongozi wote ama viongozi wa umma ambao wameorodhesha katika jeduali la pili. Naomba hili tuwekewe wazi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli katika michango yake ya kimaandishi Mhe. Ismail Jussa, aliliuliza suala hilo na nilijaribu kumfahamisha, lakini naomba niongezee tu labda hakunipata vizuri. Kifungu cha 2 kwenye Mswada wa Sheria ambapo unaonesha matumizi ya sheria pale limezungumzwa *generally*, lakini sasa kwenye jeduali la pili ndio umetajwa hasa wale viongozi wa umma wenyewe waliokusudiwa kwa sheria hii na ndio maana ikasemwa kwamba chini ya kifungu cha 3.

Kifungu cha 3 ukitizama utaona hapo orodha ndio hiyo tunayokusudiwa, kwamba viongozi wa umma waliokusudiwa ni hawa, sio wote *as such,* wote ni hawa waliotajwa kwa sasa. Kwa hiyo, tuko *specific* kwa waliotajwa kwenye jeduali la pili.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwa hili kwa sababu si kubwa Mhe. Waziri akubaliane tufanye marekebisho madogo tu ili tukidhi hiyo haja aliyoeleza yeye, kwamba pale mwisho wa kifungu cha 2 paongezwe maneno "kama walivyoorodheshwa katika jeduali la pili la sheria hii", basi itakuwa inajulikana kwamba si wote kwa maana waliotajwa hapa, lakini wote hii inarejea kwenye jeduali la pili. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti nimekubali ushauri.

Kifungu 2 Matumizi ya sheria pamoja na marekebisho yake

Mhe. Mwenyekiti: Marekebisho ndio hayo ambayo Mhe. Ismail Jussa Ladhu, amependekeza nakukubaliwa.

Kifungu 3 Ufafanuzi wa

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 3 kinahusu ufafanuzi wa maneno. Hoja yangu inajikita katika tafsiri ya neno "kiongozi wa umma" na zaidi kwa sababu ndiyo inayofanya jeduali la pili kupata uhalali katika sheria hii. Sina tatizo kama ni tafsirim lakini nazungumza jeduali la pili ambalo limepata uhalali kupitia kifungu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, jeduali la pili limetaja orodha ya viongozi hao na katika orodha hiyo nilipendekeza kwamba tuongeze masheha na madiwani na pia, nilisema Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ingawa pengine tukitaja madiwani kwa sababu wenyeviti na mameya wanatokana na hao hao, wanaweza wakawa wamejumuishwa. Ingawaje hoja pia inapaswa kutiliwa nguvu kama ambavyo wametajwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, lakini wametajwa na mawaziri, haidhuru mawaziri wanatokana na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Sasa nilikuwa napendekeza kwamba waziri akubali pamoja na maelezo aliyoyatoa kuwaongeza masheha na madiwani.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu iko katika mswada wake aliyotuletea yeye mwenyewe kama nilivyomueleza katika waraka wangu. Ukiangalia katika jeduali la kwanza kifungu cha 12 kinachohusu kuwaheshimu watu, mengi na kwa kuokoa muda sitaki kukisoma, mengi yaliyotajwa ambayo yanahusu utoaji wa huduma kwa wananchi wetu huduma hizi nyingi zinatolewa na masheha. Sheha kwa hadhi yake kafika pahala kuwa anapeperusha bendera ya nchi kwamba ni kiongozi mkubwa katika nchi.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nadhani si vyema kuwa tunatunga sheria kama hii tukasema kwamba masheha tuwaache. Hoja ya Mhe. Waziri kwamba tuangalie vipato vya mshahara, nadhani sheria hii ya maadili lengo lake ni kuweka misingi ya kuzuia matumizi mabaya ya madaraka, ingelikuwa mfano tunaaminika kwa mishahara yetu tunajitosheleza, tusingekuwa na sheria hii.

Lakini tuna wasiwasi kwamba kuna watu wanaweza wakatumia nafasi zao kujitajirisha na watu kama masheha na madiwani, mara nyingi wametajwa hata katika ripoti za Kamati Teule za Baraza hili, ukitizama za Manispaa, tumeonyeshwa wanapotumia nafasi zao hizi kujitajirisha kwa kujimilikisha mali kwa nafasi zao kinyume na taratibu za sheria.

Kwa hiyo, nilikuwa nadhani ili kuhakikisha uwajibikaji na hawa nao wangeingia katika jeduali hili la pili ili na wao vile vile wakatakiwa kuwa na uwajibikaji kama ambavyo viongozi wengine wametakiwa. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli katika mapendekezo yake Mhe. Ismail Jussa, alishauri kwamba waingizwe masheha, madiwani na wenyeviti wa Halmashauri. Kama nilivyosema ukitizama kwa viongozi waliotajwa na waliopendekezwa kwenye jeduali la pili, ukiwatizama wote kuhusu *level* yao, sio *level* ya sheha, tafauti kabisa.

Sasa akazungumza suala jengine la dhamana zao, suala la utendaji wao, hilo ni suala jengine. Sasa hapo sheha ana wakubwa wake, ndio tunaposema wajibu (*accountability),* sheha ana wakubwa wake, sheha anasimamiwa na nani. Sasa huyo mkubwa wake atamsimamia sheha ipasavyo ili aone kwamba ndivyo. Lakini sheha kwa kumtia humu, kama nilivyosema tunahisi kuna walimu wakuu, mwalimu mkuu anasimamia skuli na watoto 1500, 2000 tuwatie humu? Wana dhamana kama hizo, wengine wana dhamana za pesa, lakini hawamo humu.

Pia, naomba kusisitiza kwamba sisi tumeshauri tuanze na *list* hii, huko mbele waziri kapewa wasaa wa kutunga Kanuni, tukiona kuna umuhimu tutawatia, hakuna tatizo, tutakuwa *flexible,* tutawatia kwa huko mbele. Lakini kwa sasa hebu tizama hii orodha sasa hivi ni watu 79. Mimi nahisi kwa sasa tuanzie hapa ili tuone tunakwendaje, tuko *flexible* Kanuni tutatunga tutawaingiza wengine kadiri ya haja itavyokuwa. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima siafikiani na maelezo ya Mhe. Waziri. Nadhani sitaki kujadili habari ya walimu wakuu kwa sababu si hoja yangu, hoja yangu nimejikita kwenye madiwani, masheha na wenyeviti wa Halmashauri. Kwa hivyo, naomba tujielekeze hapo ili kuupa mjadala wetu uhai na uwe *specific*.

Mhe. Mwenyekiti, hapa katika orodha hii aliyotuletea nambari 59 kwa jeduali ya pili ni Katibu Halmashauri ya Wilaya. Sasa hii hoja yake inakuwa *defeated* na mswada wake mwenyewe, unamuingizaje Katibu wa Halmashauri ya Wilaya, lakini Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hawajibiki.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine tumezungumza msingi wa mswada huu ni kulinda maadili kwa viongozi wanaohudumia watu, yaani viongozi wa umma. Mhe. Waziri, anaposema kwamba hayo ya utendaji wao tusiyalete hapa, unadhani jana nilipoanza kuchangia nili-*quote* nukuu ya Mhe. Abraham Lincoln aliyekuwa Rais wa Marekani, alisema kwamba; "Binadamu yeyote anaweza ku-*stand adversity,* lakini ukitaka kumjua tabia yake mpe *power*".

Kwa hivyo, sheria hii imekuja kwamba waliopewa madaraka na masheha na madiwani wana madaraka, kama ambavyo wawakilishi wana madaraka, kila mmoja katika ngazi yake. Kama masuala ya matumizi mabaya ya madaraka hayahusu hawa waliorikodiwa hapa tu, hata wao wanatajwa.

Kwa hivyo, nasema ili kuwasaidia wananchi na kwama kweli tunasema lengo la serikali hii kuwa na uwajibikaji tunahofia nini kuwajumuisha masheha na madiwani ili na wao wawajibike kutangaza mali zao, wahakikishe kwamba wanafuatiliwa nyendo zao na wahakikishe wanafuata maadili haya kama viongozi wengine wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hawa ndio wanaoshughulika na wananchi takriban katika kila siku katika harakati zao za maisha. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri, kwa hili tusivutane sana akubali tuwaongeze hawa ili tuwaridhishe wananchi kweli kwamba serikali hii lengo lake ni kuwafanya kila anayetumikia umma kwa nafasi yake ambaye maslahi yake yanaweza kuleta mgongano basi awajibike kufungwa na maadili haya. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru kwa ku-*quote* ma *philosopher* wakubwa kina Mhe. Abraham Lincoln, lakini sasa Mhe. Abraham Lincoln kwa Marekani, sio huku Zanzibar tena na mtizamo wetu haidhuru vile ndio vigezo, lakini ukichukulia *philosopher* ya Mhe. Abraham Lincoln wakati wake huo *century* ya ngapi, sijui leo tuko *century* nyengine. *Anyway*, ninachotaka kusema mimi narudia pale pale Mhe. Mwenyekiti, sisi hatukatai nakubali *observations* zake, lakini kwa sasa tuanzie orodha hii.

Kwa sababu kama nilivyosema bado kuna watu tuli-*brainstorm* sasa, kwa nini huyu asiwemo, huyu awemo, tukasema aa, sasa kazungumza suala la dhamana. Kama alivyosema dhamana huyu ana mkubwa wake na anamuangalia, anakwenda naye. Sasa hayo mwenye dhamana atamsimamia vizuri na sheha anateuliwa na Mkuu wa Mkoa na tayari masheha wengine wapo na wameondoshwa na Mkuu wa Mkoa na mambo waliyoyafanya.

Mimi nakubaliana naye kwamba kuna viongozi wangepaswa waingie, lakini ndio nasema kwa sasa hebu tuanzie hii, yaani tuanzie orodha hii tusiufanye uwe *exhaustive*, wakati wowote sisi tutahisi, tutafanya kazi pamoja nchi yetu ndogo hii, tunakwenda, tutaambizana jamani, ee, tunahisi hivi.

Pia, kamzungumza Katibu wa Halamashauri. Katibu wa Halmashauri ni mtu mkubwa sana na ndio mtendaji mkubwa, yeye ndiye *dictionary* pale la Halmashauri nzima. Kwa hiyo, yule lazima na yeye awe *subjected* kwa hili.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ametoa hoja yake na msimamo wake mara mbili na upande wa serikali kama mtoa hoja alivyosema ameshaweka msimamo wa serikali kwamba kwa sasa kwa sababu ambazo amezieleza Mhe. Waziri, naona hakuna haja ya kuongeza hao ambao wanatakiwa kuongezwa, kama ambavyo Mhe. Ismail Jussa, ameshauri.

Sasa nadhani maamuzi yafanywe maana sasa Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Waziri watasimama na kukaa kwenye hoja hii na nadhani hoja ambayo Mhe. Waziri, bado hajakubaliana na Mhe. Ismail Jussa. Kwa hiyo, mimi nadhani kwenye hili tungefanya maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kuna hoja hiyo, Mhe. Ismail Jussa, yeye anapendekeza kwamba tungewajumuisha masheha, madiwani na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya katika orodha ile kwenye nyongeza ya pili kwamba nao waingie katika viongozi wa umma. Serikali wao wanaona kwamba kwa sasa twende na orodha hii iliyopo ambayo haijumuishi hao viongozi watatu tuliowazungumza, naomba sasa tufanye uamuzi juu ya hilo, tunasemaje?

Wale wanaokubaliana na hoja ya kwamba wajumbe hao waliopo katika orodha ya pili kwa sasa iwe ndio inatosha, hebu wanyanyue mikono tuone. Wale wanaosema kwamba tuongeze na wajumbe hao masheha, madiwani. Wale wanaosema kwamba orodha iliyopo kwa sasa itoshe wameshinda.*(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Nadhani tunaendelea.

Sehemu ya Pili

Kuanzishwa kwa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Kifungu 4 Kuanzishwa kwa tume
Kifungu 5 Muundo wa tume pamoja na marekebisho yake
Kifungu 6 Uteuzi na muda wa kushika madaraka na kinga kwa mwenyekiti
Kifungu 7

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Katika kifungu cha 7 katika mchango niliotoa nilipendekeza kwamba kifungu cha 7 (3) (c) pale mwisho kiongezwe "na makosa ya jinai".

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ilikuwa kwamba ukiisoma sifa za Mwenyekiti na sifa ambazo zinamfanya Mwenyekiti, mtu asiweze kutoka kwa Mwenyekiti 7(3)(c) inasema ni mtu alietiwa hatiani na Mahakama au chochote chengine chochote cha kinidhamu kwa makosa ya uadilifu au uaminifu.

Sasa nilipendekeza pamoja na Wajumbe wengine, lakini kwa sababu niliyesimamia hoja ni mimi, kwamba tuongeze pia na makosa ya kijinai. Maelezo ya Mhe. Waziri yalisema kwamba ukishasema uadilifu na uaminifu inachanganya.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo hayo si sahihi na yanapotosha Baraza, inawezekana makosa ya uadilifu na uaminifu ndani yake yamo makosa ya jinai.

Lakini hoja ya Waheshimiwa Wajumbe ilikuwa ni kwamba Mwenyekiti aliyepewa mamlaka makubwa ya kusimamia sheria hii hapaswi kuwa na upungufu wa maadili kiasi ambacho yeye mwenyewe wale wanaochunguza wakatilia shaka kwamba anaweza kutenda haki. Hasa ikiwa Mjumbe Baraza la Wawaklishi tu kugombea kama umetiwa hatiani kwa kosa ambalo la jinai ambalo linazidi miezi sita kifungo chake, huruhusiwi kugombea, seuze kwa nafasi ya mtu ambaye anamchunguza mpaka Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, tukasema kwamba ni muhimu itaje kwamba ni mtu ambaye amewahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai lolote linamuondoshea sifa ya kuweza kuongoza chombo kama hiki. Nadhani Mhe. Waziri, akubali kwamba tuongeze sifa hii. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, tumekubali ushauri wake tutaongeza.

Kifungu 7 Sifa za Mwenyekiti pamoja na marekebisho yake

Kifungu 8

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 8 kinahusu Uteuzi wa Makamishna na swali ambalo nimeliuza ambalo bahati mbaya sikuridhika na maelezo ya Mhe. Waziri, naomba anifafanulie vizuri zaidi ili turidhike na tukipitishe kifungu hichi. Niliuliza nini nafasi, uwezo na kazi za Makamishna waliotajwa katika kifungu hichi.

Mhe. Mwenyekiti, nimeuliza hivyo kwa sababu nikijibiwa hapa pengine huko mbele itakuwa haina shida tena katika baadhi ya vifungu. Kwa sababu kuna vifungu vingi sana katika sheria hii. Sheria inaanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi na kifungu cha 6 kimeanzisha Mwenyekiti.

Sasa kuna Mwenyekiti kama kiongozi wa taasisi, lakini vile vile, kuna tume yenyewe kama taasisi. Sasa nikajiuliza katika sheria hii mara nyingi anatajwa Mwenyekiti peke yake katika kusikiliza katika kufanya maamuzi, sasa nikajiuliza ni Mwenyekiti au ni chombo ambacho kinajumuisha wale Makamishna wengine wawili?

Lakini kifungu cha 8 ndiyo kimewataka hao Makamishna, lakini ndio hapo hapo huoni tena nini majukumu yao zaidi ya kuambiwa kwamba watakuwa ni wasaidizi na watatekeleza majukumu kwa maelekezo waliyopewa na Mwenyekiti.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, huoni pahala popote kwamba katika kusikiliza malalamiko na kumsikiliza mlalamikiwa ajitetee kwamba ni tafsiri ya tume ambayo inajumuisha na makamishna wake. Ndio maana nikasema hebu waziri atuwekee wazi kwamba Makamishna hawa *roll* na uwezo wao ni nini katika tume hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kama si hivyo tukisema kama ni wasaidizi na watatekeleza majukumu watakayopangiwa na kazi kwa maelekezo watakayopewa na Mwenyekiti, inawezekana kabisa Mwenyekiti asiwashirikishe katika shughuli zake na ikawa ndiyo imeishia hapo, kwa hivyo, wapo wapo tu. Naomba hilo tupate maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mhe. Ismail Jussa Ladhu, aliuliza hilo swali na nimemjibu. Lakini kama anavyosema hakukubaliana na majibu yangu. Lakini huo ndio ukweli kwamba mwenye dhamana ya tasisi hii ya Tume hii ya Maadili ni Mwenyekiti, hawa ni wasaidizi wake kama taratibu za Mahakama zilivyo nyengine, hawa ni wasaidizi na sifa kwa kisifa ni zile zile ambazo ukiacha ile mwenye sifa ya kuwa Jaji wa Mahakama Kuu.

Lakini tumesema kwamba bila ya kuathiri masharti ya kifungu 7(2) kinasema;

> "Mtu hatateuliwa kuwa Mwenyekiti mpaka awe mwenye hekima, uweledi, uaminifu".

Mhe. Mwenyekiti, tumeeleza vizuri kabisa hapa na "Uteuzi wa Makamishna kifungu namba 8 watateuliwa na Rais na watakuwa ni wasaidizi wa Mwenyekiti katika kufanya kazi za tume na watatekeleza majukumu na kazi kwa maelekezo watakayopewa na Mwenyekiti", imewekwa wazi katika kifungu namba 8.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, tukirejea katika kifungu cha 5 kinasema; "Tume itajumuisha Mwenyekiti na Kamishna wawili". Kwa hivyo, hiyo ndio tume kwa tafsiri ya sheria hii.

Sasa hoja yangu ilikuwa imejikita katika kifungu cha 8, kwa sababu kama ulivyosema hapa wameambiwa watakuwa ni wasaidizi wa Mwenyekiti katika kufanya kazi za tume na watatekeleza majukumu na kazi kwa maelekezo watakayopewa na Mwenyekiti.

Hoja yangu ilikuwa kwamba tukiwa *limit* kwamba wao kazi yao ni pale tu watakapopata maelekezo ya Mwenyekiti, ndipo ninapopata wasi wasi hapo. Kwamba na huku mbele sheria hii vifungu vingi baada ya kutaja neno "tume" katika kufanya kazi, imemtaja Mwenyekiti. Ikiwa Mwenyekiti hakuwajumuisha Makamishna hawa, yaani hakuwapa maelekezo haya, kazi yao itakuwa nini, labda nitoe mfano Mhe. Mwenyekiti.

Hicho chombo tukikitizama ni *a quasi-judicial* na hata Mahakamani ambapo Mhe. Mwenyekiti, umeshawahi kuwa hakimu, mara nyengine katika ngazi za juu za Mahakama wanakuwepo kwa mfano wale wazee wa Mahakama na vitu vyengine kama vile. Lakini *roll* yao inajulikana. Sasa hapo ukisema kwamba wao mpaka watakapopata maelekezo, hofu yangu ni kwamba wanaweza wasishirikishwe.

Kwa hivyo, nasema tusaidiwe tu ili kikae vipi vizuri ili kuona kwamba baada ya kumpa *discussion* kubwa Mwenyekiti kwamba yeye ndie atatoa maelekezo, iwe kwamba tume itakapokaa kufanya kazi zake za kupokea na kusikiliza malalamiko kwamba tume hiyo inajumuisa Mwenyekiti na Makamishna hawa.

Lakini tukiacha kama ilivyokuja huku mbele huku tutajakuona kwamba Mwenyekiti peke yake anaweza akabisha asiwashirikishe hawa, ndio maana nilikuwa nataka ufafanuzi huo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ismail Jussa Ladhu, wewe uliopendekeza iweje ili ilete maudhui hiyo ambayo unayoipendekeza.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningependekeza isomeke kwamba; "Makamishna watateuliwa na Rais na watakuwa ni wasaidizi Mwenyekiti katika kufanya kazi za tume na watakuwa ni sehemu ya tume inaposikiliza na kupokea malalamiko kuhusiana na maadili ya viongozi".

Mhe. Mwenyekiti: Hayo ndiyo mapendekezo yako.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Naam!

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Kwa mantiki hiyo Mhe. Mwenyekiti, nakubalia ushauri wake. (*Makofi*)

Kifungu 8	Uteuzi wa kamishna pamoja na marekebisho yake
Kifungu 9	Sifa za Kamishna
Kifungu 10	Kula kiapo
Kifungu 11	Wafanyakazi wengine pamoja na marekebisho yake
Kifungu 12	Kazi za Tume

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 12 na hasa najikita kwenye 12 (1) (f) na (l), lakini vile vile, kwenye 12(2) na (3) kama nilivyosema. Hapa kila palipotajwa kazi, *marginal note* inasema za tume. Lakini madaraka ukitizama kwa mfano 12(1)(f), kinasema;

> "Kuchunguza kazi kitendo cha kiongozi yeyote ambacho kwa maoni ya Mwenyekiti kinapelekea au kinachangia uvunjwaji wa maadili chini ya sheria hii".

Vile vile, ukienda katika12 (1) (l), inasema;

> "Kufanya uchunguzi juu ya jambo lolote ambalo kwa maoni ya Mwenyekiti inastahili kufanyiwa uchunguzi".

Lakini ukija kusoma 12(3), kinasema;

> "Katika kufanya kazi za tume chini ya sheria hii, Mwenyekiti hatolazimika kufuata maelekezo na hatokuwa chini ya udhibiti wa mtu au mamlaka yoyote".

Mhe. Mwenyekiti, sasa hii inahusiana na ile hoja liyoizungumza punde kwamba tunazungumza Mwenyekiti au tunaizungumza tume ambayo kwa mujibu wa kifungu cha 5 ni Mwenyekiti na Makamishna wawili? Kwa hiyo, mimi ningependeza baada ya Mwenyekiti kama *marginal note* inavyosomeka katika kazi za tume, basi mote humu ikae pia kwamba ni tume, ambayo tafsiri yake imeshatolewa kwamba Mwenyekiti na Makamishna wake wawili. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Yaani itoke ile kwa maoni ya Mwenyekiti, iwe kwa maoni ya tume, ni sawa?

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Sawa sawa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, haina tatizo, sisi tuliweka Mwenyekiti kwa kumuona yeye ndiye ana *authority,* lakini kwamba tume basi mimi nasema haina tatizo, tumeikubali.

Kifungu 12 Kazi za tume pamoja na marekebisho yake

Kifungu 13 Uwezo wa mwenyekiti pamoja na marekebisho yake

Kifungu 14 Mashirikiano na taasisi nyengine pamoja na marekebisho yake

Kifungu 15 kutangaza mali pamoja na marekebisho yake

Kifungu 16 Mali zinazopaswa

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakwenda kifungu cha 16(2), kinasema;

> "Waziri atakuwa na uwezo wa kuongeza au kupunguza juu ya mali zinazopaswa kutangazwa".

Mhe. Mwenyekiti, nilipendekeza kwamba suala la kupunguza mali hizi lingeachwa, kwa sababu leo Waziri yupo Dr. Mwinyihaji Makame atalinda, kesho nakaa mimi mambo yamenigusa, nasema punguza haya mambo. Kwa hiyo, hiyo naomba neno "kupunguza" iondoshwe baada yake ibakie "kuongeza mali ambazo zinastahiki kutangazwa". Hii kupunguza tuondoshe ibaki kuongeza.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, umempata sawa sawa.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, sisi mtizamo wetu kwamba wakati mali ile inatofautina thamani yake. Sasa tulihisi waziri apewe uwezo wa huo kupunguza na kuongeza kwa mujibu

mabadiliko. Thamani ya leo ya shilingi tafauti na kesho ya mali ile, ndio mtizamo wetu. Sasa asiwe na upande mmoja tu, awe kote kote ana uwezo huo waziri na waziri afanye kama Mwinyihaji. Waziri pale yeye ana washauri ni taasisi atashirikia na hichi chombo na tume, sio kama mimi nitaondoka leo ita-*influence* kusudio langu, aah! Sisi ndio mtizamo wetu huo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, hapa hatuangalii thamani ya mali, tunaangalia mali ambazo zinapaswa kudhibitiwa ndani ya nchi, sio thamani. Kwa hiyo, ingelikuwa thamani ningesema basi itafutwe tume ya kutathmini *value*, lakini sio thamani, imejatwa majumba, mashamba na mambo mengine, ndio haya ambayo yapunguzwe.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nasema kwamba kuna siku waziri atakuwa sie yeye, kwa maana hiyo ya uaminifu, basi anaona kwamba hili jambo limegusa basi tupunguze. Hapa hatuzungumzi thamani, tunazungumzia mambo ambayo yanagusa kwamba haya yadhibitiwe ndani ya maadili ya umma na sio masuala la thamani.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, muda unakaribia kumalizika, tuko kwenye nusu ya Mswada, hebu Mwanasheria Mkuu unasemaje kuhusu muda.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwa vile ni siku ya Ijumaa na kazi ambayo iko mbele yetu inahitaji muda zaidi wa kuishughukia na kumaliza. Hivyo, naomba nitoe hoja ya kuakhirisha kikao chako hichi kuweka Kanuni kando hadi saa 11:00 jioni ili tuweze kurudi na kuendelea kufanya shughuli hii ya kupitisha mswada huu kifungu kwa kifungu.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Nafikiri kwa muda ulivyo na kipindi kilichobaki, ni dhahiri kazi hii hatuwezi kuifanya kwa umakini. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria tu ni kazi inayoweza kwisha upesi nikaona labda tunaweza tukakopa muda, lakini moja kwa moja serikali inaona kwamba tulifanye kwa umakini, wala hoja hii haina haja ya kuulizwa kama mnakubali au laa. Hebu nigae hiyo *note* ya tangazo.

Waheshimiwa Wajumbe, shughuli yetu tutamaliza jioni kwa sababu muda uliopo hautoshi kwa hivi sasa. Kuna tangazo moja. Kamati Tendaji ya UWAWAZA inaomba kukutana mara baada ya kikao hichi kuakhirishwa hivi asubuhi katika ofisi ya umoja huo. Kamati Tendaji ya UWAWAZA wakutane na katika ofisi ya umoja huo mara baada ya kuondoka humu ndani na wale Wajumbe wenye viti wa Kamati mbali mbali nao pia waonane na Mwenyekiti wao wa Wenyeviti ili wakashauriane baadhi ya mambo.

Baada ya hayo, basi Waheshimiwa Wajumbe naakhirisha kikao hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 5:55 kikao kiliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

KUTUNGA SHERIA

MSWADA WA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA NA KUANZISHA TUME YA MAADILI YA VIONGOZI NA MAMBO YANAYOHUSIANA NA HAYO

Kifungu 16 Mali zinapaswa kutangazwa pamoja...

Mhe. Mwenyekiti: Katika hoja hii ilikuwa ni zamu ya Mhe. Hija Hassan Hija sijui yupo? Tuendelee Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 16 niliorodhesha mambo kadhaa kwa Mhe. Waziri, lakini ili kufupisha muda wa mjadala na kwa kutambua kwamba Kanuni zetu zinataka Mjumbe mmoja au hoja moja isizidi nukta tatu, naomba nizichanganye zifanye kuwa ni mbili tu.

Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru Mhe. Waziri alipokuwa akifanya majumuisho amenisaidia kidogo, lakini labda hili niliulize kwa pamoja, kwamba tukiangalia kifungu cha 16 (1) (f), (e) na (g), utakuta vimeelekezwa zaidi kwenye masuala yanayohusu mali inayohusika na biashara. Kwa mfano riba inayotokana na biashara ambao mkataba wake haukuingiwa na Serikali au mashamba yanayoendeshwa kibiashara au mali zisizohamishika ambazo zinamilikiwa kwa faida.

Sasa nikasema msingi wa sheria hii ni kumfanya kiongozi atangaze mali zake zote alizonazo, lakini kipimo kikiwa kwa wananchi kujua kwamba kwa nafasi yake kiongozi huyu wa umma. Je, anao uwezo wa kuzimiliki kihalali na kama hana aeleze amezipata vipi?

Sasa unapotizama kifungu cha 16 hasa kifungu cha 16 (1), zaidi msisitizo umeekwa kwenye biashara. Nilikuwa naomba Mhe. Waziri, atusaidie, kwa nini asiwe mali zote ili kuchunga kwamba mtu anaweza kuwa na mashamba kama Dodoma, Kigombani, Selem, Pwani Mchangani, lakini ikawa haendeshi kibiashara, lakini kayamiliki anayapata wapi fedha ya kuweza kuhalalisha kuwa nayo mashamba hayo na vitu hivyo. Nilikuwa hiyo moja nipate maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ni lile ambalo pia lilikuwa limegusiwa punde kwamba kifungu cha 16 (2) kinaonesha, kwamba Waziri kapewa mamlaka ya kupunguza au kuongeza orodha ya mali zinazopaswa kutangazwa. Sasa hoja yangu hapa ilikuwa ni kwamba kwa sheria nyengine ni sawa na kama alivyosema Mhe. Waziri mwenyewe kwamba lazima sheria iwe na mtu. Lakini nikadhani kuna sheria nyengine nzito kama hizi, ni utaratibu wa nchi nyingi za Jumuiya ya Madola kwamba marekebisho yake hata majeduali, hata akipewa Waziri basi ni lazima apate ama idhini ya Kamati ya Baraza au idhini ya Baraza kwa mtizamo wetu.

Sasa nilikuwa nasema kwa sababu Waziri mwenyewe ni miongoni mwa watu wanaopaswa kutangaza mali zao katika jeduali la pili. Kwa hivyo, je, kwa mfano amemiliki mali ambazo kwa wingi wake anahofia zitamu-*expose,*hawezi kupunguza masharti ya jeduali huyu ili kujilinda mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, haya yapo katika nchi ambayo Waziri wametumia vibaya nafasi zao. Mfano mzuri sana upo Uingereza mara baada ya Tony Blair kuwa Waziri Mkuu mwaka 1997, Waziri wake mmoja wa nchi Robson alitumia nafasi yake kwa kuwa alikuwa anahusika na masuala ya fedha, akajua mapema kwamba kuteremsha viwango fulani vya kodi, akachukua mikopo kujinuisha kwa nafasi yake.

Sasa nasema haya mambo ya Mawaziri kujinufaisha nafasi zao yapo duniani. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri akubali kwamba kama tunakibakisha kifungu cha 16 (2), basi iwe ni kwamba kubadili orodha iliyokuwemo katika jeduali au jeduali lolote, basi iwe baada ya kupata idhini ya Baraza zima ili kupata uhalali hasa kwa *sensitivity* ya sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na hayo mawili. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nianze na hili alomalizie Mhe. Ismail Jussa Ladhu la Waziri kuwa na uwezo wa kuongeza au kupunguza juu ya mali zinazopaswa kutangazwa. Ni kweli tumezingatia hilo suala tukaona kupunguza kama alivyoshauri Mhe. Hija Hassan Hija, tumeona siyo sahihi, lakini huu ushauri aliokuja Mhe. Jussa, kupata idhini ya Baraza, huu tumeuwafiki na tumekubali kwamba ibaki kwa idhini ya Baraza.

Halafu kifungu cha 16 (1) (f) kwa nini mashamba yanayoendeshwa kibiashara tu, kwa nini isiwe mashamba yote? Kweli nalo tumezingatia hili tukaona kweli kuna wakulima wengine wana mashamba ya kibiashara na wengine wana mashamba isiyokuwa ya kibiashara. Kwa hivyo, tumehisi kweli tunakubali ushauri wake yote tuyataje, haina tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa *understanding* ya Mhe. Waziri na kwa hapa nasema tuendelee. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hija Hassan Hija, umerudi, eeh! hoja yako ile hebu irudie ulikawia kufika, lakini ilikuwa hoja yako ni kwanza.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilikawia kidogo lakini huu muda niliofika na kwa maelezo ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Waziri wameelewana, nadhani imekaa sawa. Kwa hivyo, tuendelee kwa hoja hii.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana.

Kifungu 16 Mali zinapaswa kutangazwa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 17

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 17, nashukuru Mhe. Waziri kajitahidi kufafanua kwamba neno lilotumika ni kwa kiingereza ku-*declare interest* wakati wa maamuzi. Kwa hivyo, nashukuru kwa hilo.

Lakini kidogo ningeomba anifafanulie nitosheke na Baraza litosheke na wananchi watosheke ili tuendelee, pale aliposema kwamba anapaswa kutangaza maslahi yake kwa mkubwa wake. Hapa kidogo imenikwaza. Kwa hivyo, ningependa ama yeye au Mwanasheria Mkuu atuweke wazi ili turidhike na tunachokitunga hapa *intension* ya *Parliament when making a legislation* iwe wazi na hoja yangu ni kwamba ingekuwa maelezo zake ni sahihi, najiuliza katika viongozi ambao wanapaswa kutangaza mali zao na kwa hivyo, wanaweza kuwa ni *subject* ya *investigation* ni pamoja na Mhe. Rais, jina nambari moja kabisa katika jeduali la pili la Rais, sasa huyu hana mkubwa tena zaidi, mkubwa wake ni mkubwa wetu wote ambaye ni Mwenyezi Mungu *Subuhuna Wataallah.*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, nilikuwa naomba atusaidie Mhe. Waziri kwamba huku kutangaza maslahi ni wakati gani, ni wakati ule wa kufanya maamuzi, lakini ikiwa ni hivyo, hofu yangu hapa ndiyo ninataka anitosheleze na naomba nieleze kwa utulivu kidogo, kwamba chukulia Mhe. Waziri kwa nafasi yake au Katibu Mkuu ambao wote wametajwa hapa au Meneja au Mkurugenzi au Mkuu wa *ZIPA*, anafanya maamuzi ambayo ni *dispersion* yake yeye mwenyewe *personally* na kwa hivyo, hana kikao anachokaa kufanya maamuzi, maamuzi kisheria au taratibu za kiutawala ni yake.

Sasa pale kama kuna mgongano wa kimaslahi baina ya maslahi ya umma na maslahi yake binafsi, ana-*declare* kwa nani? Ndiyo ilikuwa hoja yangu. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri ama yeye au Mwanasheria Mkuu anitosheleze kwamba kutangaza namna gani ili ku-*avoid* ile *conflict of interest* ambayo tunayotaka kuiondoa hapa isiwepo kwamba akifanya maamuzi yawe kwa maslahi ya umma kweli, yasiwe kama yale ya Waziri wa Uingereza niliyemtaja ambaye alipitisha mapema maamuzi, akajua kwamba viwango vya riba vitashuka, akajinufaisha yeye kwenda kuchukua mikopo na wenzake hawakunufaika, wakati sheria inafanya kazi, tayari kanufaika zamani. Sasa sitaki tufike huko. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, labda ile *version* ya kiswahili tafsiri kidogo haikwenda moja kwa moja kama ilivyopaswa. Ningeshauri na kumuomba Mhe. Jussa, hebu aitazame ya kiingereza, naona hii ipo zaidi *straight forward*. Naomba niisome kwa kupata vizuri;

> Kifungu cha 17, inasema;
>
> *"In order to avoid conflict of interest, where the Public Leader has direct financial or any other interest in any public matter which has got authority of making decision on such matter he shall declare his interest there on".*

Mhe. Mwenyekiti, ndiyo pale tuliposema ata-*declare* kwa mkubwa wake yule wa maamuzi. Labda kwa kiswahili kidogo haikuweka sawa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru na nataka nimuhakikishie Mhe. Waziri kwamba kwa Mswada huu ambayo najitahidi kuupitia kwa kina, kile ambacho nimekitolea maoni nimejitahidi kuangalia na

kiingereza. Sasa nili-avoid au niliepuka kutumia Mswada wa kiingereza kwa sababu mimi kwa maoni yangu huu Mswada wa kiingereza kuna maneno pia yanaonekana kama vile yameachwa kuchwa. Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, ukisoma kifungu cha 17 kama alivyosema mwenyewe inaanza;

> *"In order to avoid conflict of interest, where the Public Leader has direct financial or any other interest in any public matter which has got authority of making decision on such matter he shall declare his interest there on".*

Hii "*which has got authority of making decision"* huioni katika kifungu kizima inarejea wapi, hapajatajwa *institution* hapa, wala hapajatajwa *decision making board before*, pametajwa *public leader* ambavyo kwa kiingereza hakiwezi kwamba ni *which*. Lakini hata ingelikuwa hivyo inarudisha pale pale kwamba tuna tatizo la kujua kwamba ikiwa ni chombo kinachofanya maamuzi ambacho yeye ni sehemu yake, hapo nafahamu kama anatakiwa kutangaza maslahi yake ndani ya kile chombo. Lakini hivi kilivyoandikwa kwa kiingereza na hivi kivyotafsiriwa kwa kiswahili inaonesha kama ni katika kutekeleza madaraka yake.

Kwa hivyo, kama nilivyosema tuchukulie katika hali ambapo hakuna chombo cha maamuzi, yeye mwenyewe ndiye mtoaji maamuzi na pakawa na mgongano wa maslahi, tunahakikishaje kwamba huyu atakuwa ametangaza maslahi yake na anayatangaza kwa nani. Nadhani tuwe *clear* tu katika hii sheria.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nimefahamika.

Mhe. Mwenyekiti: Eeh! tuanze na Mhe. Waziri halafu baadae Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nimemfahamu vizuri Mhe. Jussa.

Mhe. Mwenyekiti, nalifikiri niligusia wakati wa asubuhi kwamba ku-*avoid* hiyo *conflict of interest*, huyu muhusika atatangaza mali zake kwa mkubwa wake. Yule mkubwa wake ndiyo a-*declare* mbele yake, siyo kama atatangaza tu kama kwenye vyombo, lakini mbele ya mkubwa wake, yule ndiye atakuwa *authority* na anamjua yule kwamba huyu anavyosema kweli au uwongo kwa mkubwa wake, hii *immediately* bosi wake.

Nafikiri hapo ndiyo ninapokusudia, lakini kama haikukaa vizuri ile mantiki yenyewe, ile *substance* yenyewe tumeshaifahamu tutairekebisha.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ni ya msingi kwa kweli, kwa sababu ukisoma kifungu hicho na kama ambavyo yeye ametoa mifano kama wale ambao wametajwa kwenye ile sheria ya pili, kuna mawaziri na viongozi wengi ambao inabidi wa-*declare* hizo *interest* hizo.

Sasa kinacho-*mis* hapa ni ile sasa taarifa kupelekwa kwa nani? Mimi nadhani kwa sababu tunaunda hichi chombo ambacho ndicho kitakuwa haya maadili, basi tuseme kama hiyo *interest* yake atai-*declare* kwa Tume ambayo inasimamia maadili. Nadhani tukifanya hivyo labda itaondoa wasi wasi ambao Mhe. Jussa, aliyekuwa nao wa kwamba hakuna pahali inapoonesha huyu atapeleka wapi, yaani ata-*declare* ile *interest* yake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ushauri wa Mhe. Mwanasheria Mkuu utatuletea matatizo zaidi, utafanya ufanyaji maamuzi uwe mgumu kweli kweli katika Serikali kwamba kila Waziri, hawa orodha ya viongozi 79 tuliowataja kwamba na si 79 hawa, maana yake ni *category*, kwa hivyo, ndani yake ukisema Waziri si mmoja, wapo 17 na wengine na wengine.

Kwa hivyo, nadhani ukisema kwamba kila mmoja akitaka kufanya maamuzi aiarifu Tume patakuwa na kazi kweli kweli. Mimi nilikuwa nadhani Waziri kaipata *concept* yangu vizuri. Mimi ningeshauri na pengine hatuna haja ya kuingia undani kukubaliana mpaka *wording* iweje, tukubaliane ile *concept* baadae bila shaka Wanasheria wa Baraza kwa niaba ya chombo hichi wanaweza kukaa.

Nadhani tuweke katika kifungu cha 17 kwamba kama alivyo Mhe. Waziri kwamba kama maamuzi yanafanywa katika chombo basi ata-*declare interest* yake ndani ya chombo kile na kama maamuzi yake yanahusu madaraka aliyonayo yeye kwa nafasi yake peke yake, basi itakuja ile aliyosema Mhe. Waziri kama basi angalau atangaze maslahi yale kwa chombo kilicho juu yake na pengine baadae si vibaya tukaweka kwamba ata-*notify* Tume ili ikae katika *record*, kwa sababu *notification* inaweza kuwa haina *problem*.

Lakini ukisema kwamba kila mukitaka kufanya maamuzi mwende Tume ya ufanyaji maamuzi katika Serikali ukawa mgumu sana. Kwa hivyo, nadhani tuiweke hivyo kwamba kama maamuzi yanafanywa na chombo kwa maana ya kikao au taasisi, basi atatangaza maslahi yake pale na kama ni yake mwenyewe, kwa hivyo, kutumia nafasi yake basi kwa mkubwa wake. Utapata matatizo na Rais na labda Rais kasema atatangaza ndani ya *cabinet* ambacho bila shaka ndiyo chombo kinawajibika kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Sijui kama tumeipata sawa sawa. Mhe. Waziri, unasemaje.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nimeifahamu anavyoelekea Mhe. Jussa na tumekubali ushauri wake tutarekebisha.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa kwamba hiyo *interest* kwa mfano kuna jambo linahusu Bodi, basi huyu mtu ambaye *interest* aseme pale kwenye Bodi yenyewe, nadhani anavyozungumzia, lakini kama inahusu jambo ambalo kuna *authority* juu yake basi a-*declare interest* kwa huyo mtu aliye juu yake. Nadhani ndiyo suala lenyewe Mhe. Jussa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika nukta ya kwanza upo sahihi. La pili, nafikiri kuna kitu kidogo umekiacha ambacho ni muhimu kikae katika *record* za Kamati hii ya Kutunga Sheria, kwamba pale anapofanya maamuzi ambayo amepewa yeye kwa nafasi yake. Kwa mfano katika Sheria ya Utumishi wa Umma kuna maamuzi mengi wamepewa yale mamlaka Makatibu, kuna mamlaka Wakurugenzi, lakini pia, sheria mbali mbali tunatunga hapa kuna mamlaka kapewa kwa mfano Mkurugenzi Mkuu wa Bandari, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka wa Viwanja vya Ndege pengine, wengi, wengi tu, kila siku tunatunga taasisi hapa tunaanzisha yale mamlaka yake.

Kwa hivyo, nadhani pale ambapo madaraka ya maamuzi au uwezo wa kimaamuzi upo kwa kiongozi, sitaki kutumia neno "mtu" kwa sababu siyo yeye binafsi, upo kwa nafasi yake kama kiongozi na *decision* ile anafanya bila ya kushirikisha chombo, basi pale atatangaza maslahi yake kwa kiongozi wa juu yake na pale ambapo maamuzi yanafanywa na chombo kama Bodi, kama Baraza la Mawaziri, kama ni Kamati, kama ni Kamisheni, basi hapo atatangaza na yeye kile chombo ambacho kinafanya maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri tupo sawa sawa. Nadhani tunawafikiana Mhe. Waziri, tunawafikiana?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naam! Tumewafikiana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria Mkuu, nadhani upo sawa?

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kubisha, lakini nilivyosema kama sasa kwa sababu ndiyo yale yale ambayo tumejadili kwenye kifungu cha (2) na tuka-*avoid* haya mambo fulani ya kwenye taasisi humo humo. Ndiyo maana mimi nikasema kama kuna lile jambo ambalo sasa inabidi badala ya kupelekwa kwa mtu aliyekuwa juu yake, ambaye anaweza pia na yeye akawa *bias* kwenye yale maamuzi, basi ipelekwe kwenye hiyo Tume ambayo ndio kazi yeke hiyo.

Kama ile Tume sasa baada ya yule mtu kuamua ofisini kwake pale yakaisha. Kama ni mimi nitapeleka kwenye jambo nitasema ofisini kwangu, bwana hili jambo nina *interest* nalo, mimi nitajitoa sitoshughulikia jambo hilo. Lakini kuna mwengine ambaye sasa hakuna wa juu yake ndio apeleke kwenye ile Tume, hakuna haja sasa ya Katibu Mkuu apeleke kwa waziri wake, hakuna.

Na kama ikitoka kwa Katibu Mkuu, akishasema kama yeye ana *interest*, basi ile *interest* yake aipeleke kwenye Tume moja kwa moja, badala ya kumpelekea waziri wake yule yule ambaye anafanyanaye kazi kila siku. Mawazo yangu mimi yalikuwa ni hayo kusema kweli. Sasa kama yeye Mhe. Ismail Jussa Ladhu, anaona yale mbayo Mhe. Waziri wamekubaliana iwe itakidhi haja, mimi sina tatizo nalo.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani tuwafikiane kwamba kama kuna jambo kwa mfano linazungumzwa ndani ya *cabinet* ambayo inafanya maamuzi na kuna mjumbe mmoja wa *cabinet* ana *interest* juu ya jambo hilo. Kwa hivyo, suala hilo ata-*declare interest* pale kwenye *cabinet*, nadhani ndio maana yake. Moja hilo.

Lakini kama jambo lenyewe sasa linahusu madaraka ya mtu na huyu mtu ndio mwenye maamuzi na katika jambo hilo kuwa ana *interest*. Anachokisema Mhe. Mwanasheria Mkuu sasa *declaration* ya *interest* hii aifanye kwenye Tume yenyewe. Nadhani ndivyo alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu. Tunawafikianaje hapo, maana inaonekana kama inamantiki.

Mhe. Ismail Jussa Ladh: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo na kama serikali inaridhika na hivyo, mimi nitasema tuendelee. Nilikuwa natahadharisha tu kwamba nilikuwa nahofia kuwa tusijekufika pahala kwamba huu ufanyaji wa maamuzi ukawa mgumu. Maana yake nini *concept* au msingi wa mtu ku-*declare interest*, ni kwamba pasitokezee mgongano wa maslahi asitumie nafasi yake.

Sasa ninachojiuliza ni kwamba kwa maana hiyo ikiwa orodha ya *categories* 79, ikiwa wote watakapotaka kufanya maamuzi na hali yetu Mhe. Mwenyekiti, unaijua ukichukulia uzoefu wa Kamati Teule zilizoundwa humu ndani na maripoti yaliyokuja, haya mambo yako mengi ambayo tunataka tuyaondoshe kwa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tukichukulia kwamba wote hawa kwa nafasi ambazo wanazo, maamuzi yatakuwa wanafanya wao, wa-*declare interest* kwenye Tume. Naona ile shida ya rundo la kazi ambalo litakuwepo katika Tume. Lakini kama serikali kwa kupitia mshauri wao Mhe. Mwanasheria Mkuu anaona kwamba hiyo ni sahihi, mimi sina tatizo, nilitaka nione tu kwamba ile *interest* inakuwa *declared* wapi. Kama serikali inaridhika na hilo basi sina tatizo.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi Mhe. Mwanasheria Mkuu sikumfahamu hivyo. Tuchukuwe kwa mfano tu, Mhe. Jaji Mkuu; Jaji Mkuu katika *judiciary* ndio *top.* Kuna jambo ambalo ana *interest* nalo. Sasa yeye ndiye mwenye mamlaka, anachosema Mhe. Jaji Mkuu ili huyu a-*declare interest* kwenye Tume yenyewe, kwa sababu huyu ndiye *top*. Lakini kwa mfano kama kuna watendaji wengine chini yake, hawa wata-*declare interest* kwa Jaji Mkuu, nadhani ndivyo alivyozungumza.

Wale ambao kuna chombo fulani chenye mamlaka ya maamuzi na kuna mmoja ndani, yaani mjumbe wa chombo kile ambaye ana *interest*, ata-*declare interest* yake kwenye chombo chenyewe. Nadhani ndivyo unavyozungumza.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Ndiyo Mhe. Mwenyekiti, nadhani umeipata *concept* yangu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Haya, Waheshimiwa Wajumbe, tunakubaliana na hilo. Haya, tuendelee.

Kifungu 17 Mgongano wa Kimaslahi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 18 Kuzingatia Miiko ya Kijamii pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nachangia nilizungumzia kifungu cha 18(3), ambacho kinasema kwamba;

> "Kiongozi wa umma atatakiwa kuepuka kauli za kibaguzi" na nikamshauri Mhe. Waziri kifungu hiki kisomeke;
>
> "Kiongozi wa umma atatakiwa kuepuka kauli na vitengo vya kibaguzi".

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nilimsikia akijibu, lakini yale majibu ya mwisho sikuyapata. Alitaja hiki kifungu na habari ya vitendo vya kibaguzi, lakini sikujua kama kakubali iingie katika hii sheria au vipi. Kwa hivyo, naomba kidogo Mhe. Waziri aniweke sawa, ikiwa kaikubali tuendelee, ikiwa hakukubali iingie ndio bado nitakuwa na hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nilisema nafikiri kwa uwezi kabisa, labda Mhe. Salma Mohammed kidogo alikuwa mbali tu. Nilisema kwamba nimekubali ushauri wake kwamba tuongeze kwenye kifungu cha 18(3), kwamba kiongozi wa umma atatakiwa kuepuka kauli za kibaguzi na vitendo vya kibaguzi kama alivyosema yeye. Mimi nikamalizia yale maneno yaliomo mule mule, kwamba zitakazoleta mgawanyiko katika jamii, kiitikadi na kimajimbo. Yamo kwenye kifungu cha 18(3), kwa hivyo nimekubali ushauri wake Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Kwa maana hiyo tunaweka (iv)?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: Tuongeze tu maneno, sio (iv).

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, tunaendelea amekubali.

Kifungu 18 Kuzingatia Miiko ya Kijamii pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 19 Rais kukuza Maadili katika Ofisi ya Umma pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 20

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hapa swali langu lilikuwa dogo sana likaambatana na pendekezo. Ningemuomba Mhe. Waziri anisaidie *position* yake, kwa sababu kama alivyokuwa akijibu, alisema kwamba hoja zangu zilikuwa nyingi, alizijibu baadhi, nyingi nikajua nitapata nafasi katika kupitisha vifungu.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hapa ilikuwa kifungu cha 20 maneno ya pembeni, kwa maana ya *marginal note*, yanasema uvunjaji wa maadili. Sasa yameorodheshwa 20 (a) mpaka (h). Halafu (i) ikasema kakiuka kifungu chochote cha sheria hii. Yaani mtu atahesabika au atachukuliwa kama amevunja maadili ikiwa kwa makusudi amefanya yafuatayo, yakatajwa (a), (b), (c), (d), (e) mpaka (h), halafu (i) ikasemwa kakiuka kifungu chochote cha sheria hii.

Sasa hoja yangu ni kwamba kwa nini tumeyataja yale (a) mpaka (h) na haya ni baadhi tu ya mambo mengi ambayo yamo katika sheria hii ya maadili, hasa ukienda katika jadweli la kwanza kuna mambo mengi sana. Sasa mimi nilidhani kwamba madamu imeorodheshwa na maadili, akikiuka au akivunja yoyote katika yale basi atakuwa amekiuka au amevunja maadili. Kwa hivyo, nikasema kama tumeweka (i), nilikuwa nadhani kwa uandishi mzuri tu, kwa nini tusingeweka kifungu cha jumla tukasema kwamba kiongozi wa umma atachukuliwa kuwa amevunja maadili, ikiwa kwa makusudi amevukiuka kifungu chochote cha sheria hii ikaishia hapo. Kwa nini tuorodheshe (a) mpaka (h) halafu (i) tuje tujumuishe yote mengine kwa pamoja. Naona kama isirafu ya maneno Mhe. Mwenyekiti. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, (O R), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, (a) mpaka (h) ni *specific* imegusa hasa ule uvunjaji wenyewe wa maadili umetaja. Sasa (i) kimezungumza kwa ujumla, kakiuka kifungu chochote cha sheria hii. Lakini huku tumekipambanua hasa kimoja kimoja. Nafikiri kuweka *more clarity,* kuweka *more* uwazi, basi ndio haja yenyewe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilitaka sana nifahamu hivyo alivyosema Mhe. Waziri nilipokuwa nikikisoma, kwamba kuna *specific* na kuna *general times*. Lakini kama nilivyosema kwangu mimi na kama sivyo naomba Mhe. Waziri kwa sababu ndiye mwenyekuelewa hasa madhumuni ya mswada huu kwa niaba ya serikali atusaidie.

Mimi kwa ufahamu wangu nilichukulia kwamba yote yaliyomo humu yana uzito sawa na kwa maana ya msingi hasa wa maadili, kwa sababu hata ukichukulia kifungu tulichokipita punde pale kifungu cha 16 tulichojadiliana, kile kimetaja mambo ambayo kiongozi ya umma anataka ataje mali zake, lakini yale maadili yenyewe kwa upana wake hasa yamefafanuliwa katika jadweli la kwanza, ambayo ni sehemu ya sheria.

Sasa ukiyachukua yaliomo katika jadweli la kwanza Mhe. Mwenyekiti, ambayo ni takriban kurasa 10 za maadili, halafu ukayaweka kwamba ni (a) mpaka (h) haya ndio maalum *specific*, halafu mengine kwa jumla tu. Nafikiri Mhe. Mwenyekiti, unafahamu katika mahakama itakuja kutoa uzito tofauti haya ikitokezea kufika huko. Lakini pengine hata kwa tume, inaweza ikawa *focus* au msingi wa kutizamwa ukawa ni (a) mpaka (h) ile (i) ya kifungu

chochote isipewe uzito, wakati yeye anavyosema kwa jumla anachukulia yote haya ni maadili yaliyokuwa yametajwa. Kwa hivyo, ndio maana nikawa nimependekeza.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme mwanzo, ikiwa serikali imeng'ang'ania hivyo sina tatizo, kwa sababu kimsingi haifuti kitu, lakini atasema tu kwa nini tuwekeane vifungu vingi kuchukua *space*, wakati mwisho tumeweka *general time* kwamba yote yakikiukwa yanakufanya kwamba umevunja maadili. Sasa kwa nini tutaje mengine halafu mengine tuyawekee kifungu cha jumla. Ndio hoja yangu ilikuwa hivyo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeshukuru kwamba Mhe. Ismail Jussa kaiona ile mantiki yenyewe na kama nilivyosema, tumejaribu hapa kuweka kwa uwazi zaidi yamekwenda kwenye jadweli, lakini mbali ya kwenye jadweli, lakini hapa hasa tumeweka (a) mpaka (h) kakiuka miko, katoa tamko, kashindwa bila sababu, katoa taarifa rasmi. Haya yako *very specific*, lakini mwisho ndio tukasema, ikiwa kakiuka kifungu chochote katika sheria hii, yaani tumezidi kutilia mkazo tu basi. Nafikiri hakuna sababu nyengine, ni kutilia mkazo tu, ikiwa kakiuka kifungu chochote katika hii basi kavunja maadili, ndio hasa tulivyokusudia.

Mhe. Mwenyekiti: Ninavyoiona hofu ya Mhe. Waziri na pengine inaweza kuwa ni hofu ya wote sisi hapa, kwamba unapowaita ma-
..... moja, mbili, tatu, nne, kuna uwezekano ikawa kuna jambo hukuliona ukawa umelisema. Sasa unapoweka kifungu cha jumla namna hii ina- *exhaust* mambo mengine yote ambayo hayakutajwa kwenye ile orodha. Nafikiri ndio kinachoonekana. Mhe. Mwanasheria Mkuu ulikuwa unataka useme kitu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani anayosema Mhe. Waziri na anayosema Mhe. Ismail Jussa, yote ndio hayo hayo kusema ukweli, maana yake hakuna hata mmoja anayepinga kutokuwepo kwa kifungu hiki. Mhe. Ismail Jussa anasema ni utiriri wa maneno, lakini yakiwepo hayaathiri kitu na Mhe. Waziri anasema na pia yakiwepo hayaathiri kitu.

Kwa hivyo, na mimi nadhani hayaathiri kitu pia Mhe. Mwenyekiti, lakini *of course* yanaonekana yanaweka msisitizo

Mhe. Mwenyekiti: Kwamba yanaweka msisitizo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Kuna mengine ambayo yanawezekana hayakutajwa, lakini hiki kifungu cha mwisho sasa kinafunga yale yote ambayo yamo ndani ya sheria hii. Kwa hivyo, madhumuni ya hiki cha kukiuka kifungu chochote cha sheria hii. Maana hata yale majadweli yamewekwa kwa mujibu wa vifungu vilivyotoka ndani ya sheria hii. Kwa hivyo, ukikiuka lolote ambalo limo ndani ya jadweli, maana yake wewe umekiuka kifungu chochote kilichotajwa ndani ya sheria hii. Kwa hivyo,

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, unanielewa vizuri kwamba panapokuwa hapana suala la msingi wala huwa sina kawaida ya kung'ang'ania jambo. Kwa hivyo, kama nilivyosema mwanzo, nilishasema kwamba ikiwa kwa mtazamo wa serikali wangependa ibakie hivi hivi sina tatizo. Lakini mimi nilikuwa nadhani ingependeza tukawapa wote wakatawala. Lakini kama mtazamo wa serikali ni kwamba yakae hivi basi tuendelee Mhe Mwenyekiti.

Kifungu 20 Uvunjaji wa Maadili
Kifungu 21

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 21 kimetofautisha na kifungu cha 20 kwa kusema kutovunja maadili. Hapa kumetajwa suala la utolewaji wa zawadi na bahati nzuri sio peke yangu tu, wajumbe wengi waliochangi walieleza hisia zao na mimi nilieleza zangu, kwamba kwa kutumia mfano wa hivi karibuni tu wa kashfa ya Tegeta Escrow Account, kwamba zawadi zinaweza zikatolewa kwa madhumuni ya kushawishi maamuzi fulani, hata kama haikuhusishwa moja kwa moja na maamuzi yale.

Mhe. Prof. Anna Tibaijuka aliposema kwamba kaingiziwa bilioni 1.6 kwa ajili ya msaada wa skuli ya wanawake, pengine haikuhusiana na masuala ambayo rafiki yake aliyompa zawadi bwana Rugamarira alikuwa anahusishwa nayo. Lakini haikufanya hiyo jamii kutokuamini kwamba kima kikubwa kama kile cha zawadi hakikuwa na sababu nyengine nyuma yake ambayo haikuwa njema kwa jamii.

Kwa hivyo, nilikuwa nasema nilipendekeza ningemuomba Mhe. Waziri, kuna kitu alikikubali katika pendekezo langu, kwamba tutaje thamani ya zawadi ambayo ikifika hiyo basi itakabidhiwa serikalini na itakuwa ni mali ya umma kwenye jadweli. Kwa hivyo, ningeomba hilo Mhe. Waziri aliweke vizuri zaidi, ili tukubaliane kwamba hiyo ndio *record* ya Hansard.

Lakini la pili, kile kifungu cha 21(5) nilipendekeza tukifute kwa sababu kimesema kafanya jambo lolote kwa nia njema kwa kadiri tume itakavyojiridhisha. Sasa nilisema nia njema good face ni vigumu kidogo kupimika hasa katika masuala ya zawadi na mambo mengine kama haya ya maadili. Kwa hivyo, mimi nikapendekeza kwamba kwa sababu mswada wetu ni *exhaust,* umetaja mambo mengi hatupaswi kuweka mwanya kama huu na tume yenyewe Mhe. Mwenyekiti, haiongozwi na malaika hii.

Mhe. Ali Mzee Ali alisema jana hapa kwamba huyu mganga anatakiwa pia atafutiwe mganga, yeye alitumia lugha ya Israel na kutoa roho, kwamba yeye mwenyewe anapaswa achunguzwe na ataje mali zake, ndio maana kumewekwa utaratibu tutaufika baadaye. Kwa hivyo, nilikuwa nasema kwa sababu haiongozwi na malaika hata yeye anaweza kuja kuwa- *compromise*. Kwa hivyo, kuwapa wao madaraka kwamba waamuwe kuwa hili ni kwa nia njema au sio kwa nia njema, nilikuwa nadhani ni matatizo.

Kwa hivyo, nilifikiri kuondosha utata tungekiondosha kifungu cha 21(5) kabisa, kwa sababu mswada wenyewe ni *exhaust* na tukiona kumejitokeza mazingira mapya basi tutarudi Barazani kuja kufanya marekebisho Mhe. Mwenyekiti. Tumekuwa tukifanya marekebisho ya sheria mbali mbali, hasa kwa suala zito kama hili, nilikuwa nadhani sio vyema kuacha mwanya kama huu. Kwa hivyo, kwenye zawadi naomba ili ikae katika *record* vizuri, tukubaliane kwamba zawadi ikifikia thamani itakayotajwa ndani ya jadweli, *describe nominal value* kama ilivyokuwa Uingereza basi itakuwa sio mali aliyopewa zawadi, itakuwa ni mali ya serikali na atatakiwa aitangaze. Lakini pili hiki kifungu cha 21(5) kinachohusu nia njema tukiondowe, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utajaji wa thamani ya zawadi iliyokubalika kwenye jadweli, nakubaliana na Mhe. Ismail Jussa kwamba tutaweka kwenye kanuni hizo thamani kuweza kujua, hii aachiwe mwenyewe na hii ibaki kwa serikali au ibaki ofisini, nakubaliana na ushauri wake hiyo tuiweke kwenye kanuni.

Lakini kwenye nia njema, mimi nafikiri tuiwachie tume. Unajua watakapokuwa wanajadili kitu, unajua nia njema hakifichiki kinaonekana wazi wazi na utaona hasa uelekeo huu una nia njema au huyu anatudanganya. Mimi nafikiri tuiwachie tume hapa, iko wazi kabisa. Mtu mwenye nia njema utaonekana wema wake na mwelekeo wake, hakuna kificho, hakuna pakujificha hapa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza tumalize lile moja ambalo kimsingi tumeshakubaliana la zawadi na thamani kutajwa. Nataka iwe *clear* katika *record* ya chombo chako hiki Mhe. Mwenyekiti, kwamba kimsingi kakubali itaingizwa katika kanuni. Lakini nadhani ama hapa na mimi ningependa nisiseme ama, niseme hapa hapa katika kifungu cha 21 tuongeze *subclose* ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu anaweza wakasaidiana baadae kuiweka hiyo yenye dhana hiyo, kwamba zawadi itakayofikia thamani ya kiwango kilichotajwa katika kanuni zitakazotungwa na Waziri au sijui niseme jaduweli, maana yake mimi hii ya kumpa Waziri naiogopa sana kama nilivyosema mwanzo kwa sababu yeye mwenyewe ni Subject ya Sheria hii, lakini tuchukulie hivyo kwamba itatajwa kwa hivyo ipate *enabling provision* hapa ndio hoja yangu.

Other wise, tukisema tukubuliane tu itakwenda katika kanuni itakuwa haina msingi wa Sheria, kwa hivyo nilikuwa naomba hiyo moja tukubaliane kwamba itawekewa *sub prose* ili ipate *an enabling provision* katika hapo, tukikubaliana hivyo sina lazima kwamba tukubaliane hapa *drafting* yake itakuwaje tumeshafanya sana huko nyuma Mhe. Mwenyekiti kwamba tunaiachia ofisi ya *AG* ikashakuwa imefahamu nini madhumuni ya watunga sheria hapa ambayo ni hayo.

Hili la pili Mhe. Mwenyekiti, bado napata tabu kumkubalia Mheshimiwa Waziri kwamba nia njema inaonekana na kila mtu itadhihirika, katika maoni niliyompelekea Mheshimiwa katika mchango wangu nilisema kwamba nia njema si rahisi kuwa na maana moja kwa watu tofauti *Professar* Tibaijuka mpaka kaondolewa anasema kwamba yeye kapokea kwa nia njema kabisa, lakini hata mamlaka iliyomteua haikuridhika na ndio maana ikamwambia akae kando. Kwa hivyo, nasema suala hili kidogo lina matatizo kwamba unaposema ukaweka kitu na kiingereza najua yapo maneno *in good face* lakini angalau mswada huu ungekuwa katika tafsiri umetafsiri *good face* kwa maana ya kifungu hichi ni nini, hakutafsiri nia njema ni nini.

Kwa hivyo, unaachiwa badala ya kuwa *objective superstation* tunaajicha *subjetive superstations* ambayo Mheshimiwa Mwenyekiti mimi naiogopa sana hasa katika masuala haya, sababu kuna nafasi kubwa ya juu kwa hivyo nilikuwa naomba Mhe. Waziri kama nilivyosema hoja yangu kubwa ni kwamba mswada wenyewe ni *exhaustic* na kama kutakuja jambo jengine tutaona kwamba kuna haja ya kurekebisha watatuletea marekebisho hapa.

Sheria ya *public service act* Mhe. Mwenyekiti tuliipitisha, ndani ya mwaka mmoja tukaja tukairekebisha baada ya kuifanyia kazi kwa sababu tuliona ina matatizo na hii vile vile, lakini kuachia mwanya hapa kwamba tume ina mamlaka ya kuamua nini *good face* na nini si *good face* naogopa sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu na nimemfahamu kwa hivyo maana yake hata ile dhamira ambayo tulikuwa nayo mwanzo Serikalini ni hiyo, kama sasa mtu huyu hiyo nia njema itajulikana je. Sasa ndio maana ikawa ile tume sasa ikaamua kama hii mfano kwa nia njema au hapana kwa sababu ya zile kazi ambazo hiyo tume yenyewe imepewa ya kusimamia maadili, sasa mimi sina tatizo kama hichi tunakubaliana kitoke hakina *affect* yoyote.

Lakini dhamira ya Serikali ilikuwa ni hiyo kama ile sasa *good face* asiachiawe yule mtu mwenyewe sasa aamuwe hii nilifanya tu kwa nia njema kwa hivyo sikuvunja maadili, ndio maana sasa ikawa ile tume aiamue kwa sababu ile tume ndio yenye mamlaka ya kusikiliza haya mashauri yoyote yanayofunguliwa dhidi ya mtu ambae atadaiwa kama amevunja hayo maadili ndio madhumuni yake yalikuwa hayo Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa waheshimiwa wajumbe tunafanyaje, kuna suala la nia njema kuondoka yaani hiyo *statement* ya nia njema iliyoko kwenye 21(5) iondoke, au ibaki na mamlaka ya kutafsiri jambo hilo kwamba nia njema iachiwe Tume Waheshimiwa Wajumbe tunasemaje tunaiondoa tunabakisha. Habu nione wale ambao wanasema ibaki maana ndio hoja iliyopo hapo ibaki hapa wanyanyue mikono, suala la nia njema kwamba libaki kama ilivyo kwenye mswada hapa wanyanyue mikono. Na wanaosema kwamba tuiondoe hebu tuhesabu, habu tuanze upya maana naona. (*Kicheko*)

Katibu hisabu wale wanaosema kwamba suala la nia njema libaki kama ilivyo ndani ya mswada wanyanyue mikono hesabu, hoja ni hivi wale ambao wanataka suala nia njema libaki kama ilivyo ndani ya mswada wanyanyue mikono.

Haya wanaosema tuondoe ni 24, wanaosema ibaki ni 27. Kwa hivyo, inabaki kama ilivyo ndani ya Mswada huu. (*Makofi*)

Kifungu 21 Kutovunja maadili pamoja na marekebisho yake

SEHEMU YA NNE - UTAWALA NA UTEKELEZAJI

Kifungu 22 Daftari

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Asante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikipongeze kitu chako kwa kusimamia demokrasi nataka nikuhakikishie wala sina kinyongo, inapopita demokrasi ya wazi kama hii mimi naheshimu maamuzi yaliyotolewa. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nimesimama kuhusiana na kifungu cha 22 na katika hichi Mheshimiwa nadhani Serikali na chombo chako hichi kama wawakilishi wananchi hapa ndipo tutakapopimwa na wananchi, kwamba sheria hii kweli tumekusudia kuweka maadili na kuwafanya viongozi wawe na uwazi, uwajibikaji na uadilifu na wawajibike kwa wananchi ambao ndio wenye mamlaka, au tunawafanyia mzaha tu wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili niliwasilisha jaduweli na marekebisho hasa ambacho kwenye sehemu (b) pale nilipendekeza kifungu cha 22(4) ambacho kama kilivyo katika mswada kinasomeka daftari la kumbu kumbu litakuwa ni siri na halitoruhusiwa kuonekana na mtu asiyehusika bila ya ruhusa ya Waziri au kwa amri ya Mahakama.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mtazamo wangu tukipitisha kifungu hichi kama kilivyo tunaufanya mswada huu na sheria yake yote itakayaotokana na mswada huu iwe ni kama vile haina maana, kwa sababu wale tuliowakusudia hasa wajue tunawawekea vizingiti vingi kuweza kujua taarifa zinazowahusu viongozi wao, kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba tukirekebishe tukifute na tukiandike upya kama nilivyopendekeza kwenye jaduweli la marekebisho kwamba daftari la kumbu kumbu litakuwa wazi kwa mtu yoyote kuliona baada ya kutoa taarifa kwa tume angalau siku moja kabla ya kuliona.

Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, najua Mhe. Waziri alipojibu alisema kwamba kuna masuala ya haki ya faragha ya mali za mtu, lakini hapa waliotajwa wameitwa *public leaders* na wengi walioandika nyaraka vitabu na maandishi mbali mbali wanakwambia ukishaamua kuwa kiongozi wa umma *public leaders* maana yake baadhi ya haki zako za *private* hazipo, yale yako mwenyewe binafsi ya nyumbani na chumbani huingiliwi. Lakini kama kuna masuala ya umma umekubali kuwa *bublic leaders* lazima kuna *obligation* za kuwa mali ya *public* kwa maana *public leader* uzitimize.

Kwa hivyo, nilikuwa nasema niwaombe sana wajumbe wenzangu niiombe Serikali ilikubali pendekezo hili, kama kweli tumedhamiria msingi wa mswada huu si kubabaishana babaishana basi mali inayohusu viongozi wa umma ziweze kukaguliwa na wananchi, baada ya kutoa taarifa katika tume na daftari liwe *public document* kwa sababu linahusu *public leaders* naomba tuweke *underline* Mhe. Mwenyekiti, neno *public* naomba sana kutoa hoja hiyo ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi.(OR), Ikulu na Utawala Bora: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hili nilimjibu Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu kwamba haipendezi kweli tupo kwenye *transparent* mpaka ndio utawala bora uwazi, lakini kwa hapa kwa mantiki hii ya maadili nahisi kuliweka daftari la kumbu kumbu za mali za viongozi kila mmoja aende tu akaliangalie na nilitoa mfano kama daftari la wapiga kura linabandikwa kwa kweli haipendezi, tutasababisha kero, tutasababisha kutokufahamiana zaidi na vurugu kubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, hata katiba yetu ya Zanzibar kwenye kifungu cha 15 kwenye mabano (1, 2) kimeeleza wazi kabisa naomba ninukuu;

> *"Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kwa mujibu wa kifungu hiki, mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria kuhusu hali, namna ya kiasi ambacho haki ya mtu na faragha na usalama wa nafsi yake, mali yake na maskani yake yanaweza kuingiliwa bila ya kuathiri kifungu hichi cha katiba hii".*

Utaratibu huu utawekwa na hawa viongozi hawa wa Tume lakini sio iwe *free* tu kwa wengine hata katiba imetuwekea wazi kidogo nafikiri tutapata matatizo zaidi hapa, lile lengo tulilokusudia hasa litapotoka, Mheshimiwa naomba anifahamu Mheshimiwa Jussa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nasikitika kwamba Mheshimiwa Waziri katumia ibara y 15 ambayo inahusu kinga ya haki za lazima, Wajibu na uhuru wa mtu binafsi katika mjadala huu, ingelikuwa kifungu hichi ndio kinatoa uhalali ambao Mhe. Waziri anausema basi mantiki ya sheria hii nzima inaporomoka, kwa sababu nilichokidai mimi utaratibu uondoshwe ule urasimu wa namna ya kuona taarifa lakini bado kwa sheria hii hii umewekwa utaratibu, ni *respective* wa kuona, kwa hivyo hiyo faragha anayozungumza si kama imelindwa kwa asilimia mia moja.

Lakini zaidi Mheshimiwa naomba tukisome pamoja kifungu alichokisoma hakiwezi kutumika kujengea hoja hiyo. Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu alichokisema kinasema;

> *" Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kwa mujibu wa kifungu hichi, mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria kuhusu hali namna ya kiasi ambacho haki ya mtu na faragha halafu yamekuja maneno na sio au faragha ya na usalama wa nafsi yake mali yake na maskani yake yaweza kuingiliwa bila ya kuathiri kifungu hichi cha Katiba hii".*

Hoja yangu Mheshimiwa ni kwamba hii mali hapa ilivyotumika inahusikana na usalama wake lakini faragha zaidi ukisoma Mheshimiwa na kwa sababu ili kifungu hichi kifahamike tukirejee kifungu cha 15(i) cha Katiba kinasema;

> *"Kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake maisha yake binafsi na ya nyumbani kwake na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake".*

Haya ndio ambayo msingi wa kifungu cha 15 cha Katiba umewalinda na 15(ii) kimeweka utaratibu kwa hivyo ninachosoma mimi narudi pale pale Mheshimiwa hawa ni *public leaders* na tumeambiwa sote ukishaamua kuwa *public leaders* maana yake umekubali sehemu ya baadhi ya faragha zako na kasema si faragha za nyumbani, ni mali msingi wake nini Mheshimiwa kuzuia mtu nafasi yake asiweze kujitajirisha sasa kama tuna m-*rise teak* huyu mwananchi hapa tunasema ajue mali za viongozi wake.

Kwamba je, zinakwenda sambamba na mshahara anaoupata na kipato chake, tunamwambia kwamba ili azione mpaka apate kibali cha Waziri au kibali cha Mahakama tunaweka *restriction* kuna mambo mengi. Pengine Waziri hapa ndiye anayetaka kuchunguzwa unafikiri Mheshimiwa atatoa kibali, lakini kama ni kwenda Mahakamani kuna mlolongo wa taratibu pengine na gharama zake mpaka kuweza kupata haki kwa nini tumuwekee mwananchi vikwazo hivi kama kweli nia ya Serikali kuleta uwajibikaji, uwazi na uadilifu mimi sijaridhika na hoja za Mheshimiwa Waziri nasema na kama hatuelewani kwa hili tufanye maamuzi kwenye demokrasia ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, (O R), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kifungu kimeweka wazi kwamba daftari la kudumu litakuwa ni siri na halitoruhusiwa kuonekana na mtu asiyehusika, bila ya ruhusa ya Waziri au kwa amri ya Mahakama, kwa hivyo, *room* ya kuonekana kwa ruksa ipo, lakini sio liwe *open public* tu kidogo ile maana tunayoitaka hasa hapa, lazima tukumbuke ni mali hizi. Haizuru ndio kweli tunatak *open nests* uwazi lakini sasa lazima tukumbuke ni mali hizi, mambo yote, ugomvi wote na hasama zote ziko hapa Mhe. Ismail Jussa Ladhu utakuja kuniangalia mie daa! Mwinyi huyu kapata nyumba hizi unakwenda angalia tu keshokutwa imekuwa hivi natoa mfano tu.

Lakini wewe unahusika kuniangalia mie yule anayehusika Tume, Waziri au mwengine kama anataka aombe ruhusa hakuna tatizo, lakini sio *public view* kila mmoja aende kama anasoma gazeti hiyo haipendezi Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mhe. Spika: Mh! kuna maelezo zaidi Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwenasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, okozi ukisema kifungu hichi cha 22(4) maana yake kwanza usome kifungu cha 16 ujue hizo mali ambazo zinataka kutangazwa, halafu sasa ziwekwe *public* kama kila mtu sasa aende pale asome mali hizi ambazo kila mtu anazo na kila mtu ametangaza, *of course* kuweka hivyo navyo kuna *point* zake maana yake huwezi tu ukasema uweke kitu *public* halafu sio kuwe kuna *point* zake lazima zitakuwepo. Kuna wale ambao watakwenda kwa nia njema na kuna wale ambao watakwenda sio kwa nia njema lakini mimi sitaki kwenda huko.

Mimi ninachosema hata ukisoma hicho kijifungu kidogo cha nne ni kwamba pamoja na usiri ambao umewekwa, lakini pia yule ambaye atataka kwenye kuona basi lazima aombe kama huwezi ukataka tu kwenda kutizama mali za mtu ambazo amezitangaza kwenye kifungu cha 16 zote hizi, na zile ambazo tayari Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu amependekeza ziengezwe halafu ukawacha tu zitizamwe kama vile ambavyo mtu anatizama taarifa nyengine zozote, madhumuni yake ni kwamba toa taarifa watu wakutambue wewe ni nani kwa madhumuni gani halafu utapewa hiyo *access* ya kuona ndio madhumuni ya kifungu hichi kidogo cha nne Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mheshimiwa Mwenyekiti, nareje pale pale kwamba kwanza tujiulize mantiki ya mswada huu kuletwa hapa ni kutu gani, mantiki yake ni kuleta uwazi, uwajibikaji na uadilifu serikalini na kwa viongozi wa umma katika mihimili yote iliyokuwa imetajwa hapo kwa Serikali Baraza la Wawakilishi na Mahakama, sasa nasema kama lengo ni hilo kwa nini tunawawekea vikwazo wananchi kidogo kupata taarifa hizo, naona kama tumetiwa *the holl purpose* na msingi wote wa kuleta mswada huu Mheshimiwa, kama vile tunawacheza shere wananchi sasa.

Nitoe mfano Mheshimiwa kwa sababu Waziri kazungumza kwa mfano mimi leo nataka kujua mali anazomiliki Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, sasa nakwenda kufanya *application* ambayo Waziri lazima ndio atoe idhini, Waziri ambae kiuwajibikaji ndani ya Katiba katika Baraza hili anawajibika chini ya Makamo wa Pili wa Rais kwa misingi ya *responsibility* unadhani kweli Waziri huyu atanipa kibali mimi nikakague mali za Mhe. Balozi Seif Ali Iddi. Kwa hivyo mimi nasema kama tumejikubalisha kama mali umezipata kihalali kwa nini uogope mwananchi kukukagua. Kwa hivyo mimi nasema kama kweli madhumuni yake ni haya la madhumuni yake ni kukamilisha asilimia ya ilani tu basi tuendelee Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tuamua pengine hoja zote mbili zina msingi ukiangalia kwamba wakati mwengine kuweka kila kitu wazi kwa tabia zetu wakati mwengine hujenga choyo na choyo kina matatizo yake. Lakini wakati mwengine ukisema kwamba watu wasijue nayo inakuwa sivyo. Hoja zote mbili zina mantiki, kwa hiyo sasa ni kuamua je, daftari la kumbukumbu linakuwa *open to the public* au kwa ruhusa ya Waziri au kwa amri ya Mahakama, ambavyo ndivyo ilivyo kwenye Mswada kwa hapa. Kwa sababu kuweza kuangalia kumbukumbu inawezekana siyo siri ya moja kwa moja, ila iwe kwa sababu ya ruhusa ya Waziri au kwa amri ya Mahakama.

Sasa tuamua Waheshimiwa Wajumbe wale ambao wanaona ibaki kama ilivyo kwenye Mswada iwe ni siri mpaka pale ambapo Waziri ataruhusu au kwa amri ya Mahakama wanyanyue mikono. Wanaosema kwamba kumbukumbu hizo ziwe wazi kwa *public* moja kwa moja wanyanyue mikono. Wanaosema iwe siri mpaka pale ambapo Waziri ataruhusu au amri ya Mahakama wameshinda. Kwa hiyo inabaki kama ilivyo kwenye Mswada hivi sasa.

Kifungu cha 22 Daftari la Kumbukumbu za Mali na Maslahi
Kifungu cha 23

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Asante Mhe. Mwenyekiti, Mwenyekiti Wajumbe wako wasione dhiki ndio utaratibu wa kulipwa fedha na walipakodi kufanya kazi yao hapa. Ndio tunatengeneza maadili ili tupate fedha kwa jasho halali tufanya kazi ya wananchi hapa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 23 niliona neno katika 23(1) pake mwishoni, ambalo nilimuomba Mhe. Waziri kwamba turekebishe. Lile la mwanzo lilikuwa linawalinda wananchi, hili la pili lengo langu ilikuwa nikumlinda huyu anaelalam ikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, 23(1) imeweka utaratibu kwamba mtu anayewasilisha malalamiko aandike jina lake, anuwani yake na maelezo ya uvunjwaji wa maadili. Lakini pana ile *provision* inaanza isipokuwa inasema kwamba;

> Kifungu 23(1) "Isipokuwa kwamba Mwenyekiti hatokataa madai yaliyopelekwa mbele yake, kwa sababu tu yamekosa saini jina na anuani ya mlalamikaji."

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hii *proviso* hii mimi kidogo siiwafiki. Mwanzo nilipousoma Mswada nilifurahi sana nikasema pengine kuna mtu anajua kwamba kuna matatizo fulani katika mali za mkubwa fulani, kwa hivyo akawasilisha malalamiko. Ili kulindwa basi anaweza asiandike jina wala anuani, wala saini. Lakini niliposoma Mswada huu mbele unasema kwamba siku ya kusikiliza malalamiko anatakiwa mlalamikaji awepo na mlalamikiwa awepo. Kwa hivyo sababu ya kumlinda haipo tena, kwa sababu itabidi a- *appear in personal*. Kwa hivyo nikasema kama msingi ndio huo kwa nini tuweke kwamba malalamiko yanaweza kupokelewa hata kama hayana saini, jina na anuwani.

Kwa hivyo, mimi nilikuwa napendekeza kwamba kifungu hiki kimalizikie pale kwenye paragrafu ya mwanzo unaodaiwa. Lile sharti la kwamba Tume inaweza kupokea malalamiko hata kama haina jina, saini au anuwani tuyaondoshe. Ili iwe ni utaratibu kwamba anaewasilisha malalamiko andike jina lake, saini yake na anuwani yake. Kwa sababu mwisho wote wawili wanatakiwa wawepo mbele ya Tume katika kusikiliza malalamiko hayo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, tumelizingatia sana hoja hii ya Mhe. Ismail Jussa, tukafikiria kwamba kwa hali ya nchi yetu kuna watu wengine wapo mbali, vijijini, wengine kuandika na kusoma hawezi kujieleza vizuri. Sasa unamwambia kwamba tukatae madai yake kwa sababu tu yamekosa saini nafikiri sio barabara.

Mimi nakubali hili jina na anuani la mlalamikaji hili linaweza likaandikwa na anuani ikaandikwa. Lakini kwamba imekosa saini tu tukatae nafikiri si busara. Tuchukulie kidogo nchi yetu hatuko Marekani, hatuko wapi tuko Zanzibar, lazima tuangalie hali yetu kidogo. Mwengine kuandika anaweza lakini sasa saini yake mpaka umshike, ndio mantiki yenyewe hasa tukasema isiwe sababu hiyo tena ya kukataa malalamiko yake.

Lakini jina mimi nakubaliana nae kwamba jina litaandikwa na anuani pia inaweza ikaandikwa ya mlalamikaji, lakini saini inaweza ikawa ngumu. Ndio hivyo tukasema isikataliwe kwa sababu ya kukosa vitu hivi viwili. Hili nakubaliana nae, lakini saini isionekane kwamba imekosekana saini kwamba tena ikataliwe? La la la! Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani kimsingi keshakubaliana na mimi Mhe. Waziri, kwa sababu nadhani kwa kiwango chake anajua kwamba saini sio kama ile yako wewe Mhe. Spika ya kuanguka ikawa haiwezi haiwezi kunakiliwa mwengine. Hata alama ya dole ni saini kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo, hapa halindwi yeyote mimi ningelielewa kwamba tunaruhusu kwamba mtu anaweza kupeleka malalamiko kwa mdomo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini msingi wa sharti katika kifungu hichi cha 23, ni kwamba malalamiko yawe kwa maandishi. Ilichokifanya hapa ni kwamba malalamiko yenyewe inawezekana yasiwe na saini jina wala anuwani yakapokelewa. Ndio kama nilivyosema kwamba mwanzo ilikuwa lengo ni kumlinda asijulikane jina ili Tume iweze kuchunguza.

Mimi nikasema sawa, kwa sababu tunataka kuwalinda watu fulani na nafasi zao. Lakini huku mbele tunasema kwamba malalamiko yatasikiliwa awepo mlalamikaji na mlalamikiwa, kwa hivyo, hatumlindi huyu. Sasa kama hatumlindi kwa nini apeleke waraka na tumesema mwanzo kwamba Tume hiki ni chombo *first judicial* ni kama vile kina mamlaka ya Kimahakama Mahakama. Kwa nini tusiondoshe sharti hili ni kwamba anaewasilisha malalamiko ajumuishe jina lake, saini yake.

Mhe. Mwenyekiti, saini kwa maana ya kisheria ufahamu ni pamoja na alama ya dole kwa aliyekuwa hajui kusoma na kuandika. Kwa sababu kwa msingi huo unaweza ukampata mtu akakuandikia malalamiko yako. Lakini yakawa ni yako kwa sababu umetia alama ya dole kwamba haya ni yako. Nilikuwa nadhani iyondoke, ibakie kwamba lazima pawe na jina, saini kwa maana hiyo inajumuisha na alama ya dole na pia anuwani ya mlalamikaji. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani anavyosema Mhe. Ismail Jussa ni sawa, tutakiondoa hichi. Ni sawa kwa sababu ile ya mwanzo tayari yule mtu atapeleka ametia saini yake, ametia jina lake imeshaeleza, hii ilikuwa inawezekana mtu sasa akasahau lakini akapeleka. Sasa kama inaonekana, mimi sioni kama ni tatizo.

Mhe. Spika: Ni sawa na nadhani kweli, kwa sababu kuna watu wana tabia ya kutaka kumtia dowa mtu, kwa hiyo akajiandikia tu wala hakuna msingi wowote ilimradi Pandu Ameir Kificho aingie dowa. Lakini akiweka saini yake hiyo ndiyo itathibitisha kweli kuwa malalamiko ni ya msingi. Nadhani tukubali. Kwa hiyo tunakubaliana kwamba saini iwepo na alama nyengine kama hiyo dole ikubalike kuthibitisha kwamba kuna malalamiko ya msingi.

Kifungu 23	Malalamiko ya Uvunjwaji wa Maadili Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 24	Upatikanaji wa Taarifa na Ushahidi.
Kifungu 25	Ushauri wa Kitaalamu Katika Usikilizaji wa Madai au Malalamiko Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu 26	Utaratibu wa Kusikiliza Madai au Malalamiko Pamoja na Maekebisho Yake.
Kifungu 27	Tume Kutoa Maamuzi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba turejee tena katika jaduweli la marekebisho nilolitoa kwenye kifungu cha 27(a) ambapo nimependekeza tuongeze vijifungu vidogo cha 3, 4, vitakavyosomeka kama ifuatavyo:

> "27(3)Endapo Kiongozi hakuridhika na maamuzi ya Tume yaliyotolewa dhidi yake, chini ya kifungu cha 27(1) cha Sheria hii, atakuwa na haki ya kukata rufaa au kuomba mapitio ya uamuzi huo wa Tume katika Mahakama Kuu ya Zanzibar".

(4)Kabla ya kuchukua hatua dhidi ya Kiongozi wa Umma aliyelalamikiwa kuvunja maadili mamlaka inayohusika itahakikisha kuwa Kiongozi huyo anapewa fursa ya kusikilizwa".

Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo haya yangu au pendekezo langu langu hili lenye kuongeza vijifungu cha (3) na cha (4) limetokana na mchango wangu niliposema kwamba: Katiba yetu ya Zanzibar kifungu cha 12(6)(a) kimeweka utaratibu wa haki za msingi za binaadamu na 12(6)(a) inasema Mhe. Mwenyekiti, kama hivi ifuatavyo:

"Wakati haki na wajibu wa mtu yeyote inahitaji kufanyiwa uwamuzi wa Mahakama au chombo kinginecho kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa na pia haki ya kukata rufaa au ya kupata kitulizo kinginecho cha kisheria kutokana na maamuzi ya Mahakama au chombo hicho kinginecho kinachohusika".

Nipo hapa chombo kinginecho kinachohusika. Sasa msingi wa hoja Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba mambo haya mawili. Kwanza kama nilivyosema kwamba Tume hii imepewa *role* au nafasi kama ni *first judicial*. Kwa hivyo nilikuwa nadhani kifungu hiki cha Katiba 12(6)(a) kinaingia hapa kwamba unapokuwa umehukumiwa na Mahakama au na chombo kama hichi lazima upate haki ya kukata rufaa au kitulizo chengine yaani *any other remedy* na katika mfumo wa Jumuiya ya Madola kuna suala la *judicial review*. Kwa hivyo ndio maana nimependekeza kwamba tuwe na kijifungu kidogo cha 3 ili kutoa haki ile iliyokuwemo ndani ya Katiba kuingiza ndani ya sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, kile cha 4 hoja yangu ilikuwa ni kwamba tume itasikiliza malalamiko na bila shaka hii sheria imesema itampa nafasi ya kumsikiliza huyu anayelalamikiwa. Lakini mwenye mamlaka ya kuchukua maamuzi ni mamlaka inayohusuka, ambayo katika Mswada huu imetafsiriwa katika tafsiri kwamba mamlaka inayohusika maana yake ni Rais, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi na Taasisi nyengine yoyote ya Umma ambayo kiongozi wa umma anawajibika kwayo.

Kwa hivyo, nilikuwa nasema pamoja na kwamba keshasikilizwa na hicho chombo kilichopokea malalamiko, lakini na huyu anayefanya maamuzi sasa ya kumchukuliwa hatua ambazo zimeorodheshwa ndani ya kifungu cha 30, ikiwemo onyo na tahadhari, kushushwa cheo, kusimamishwa kazi, kuachishwa kazi, kuondolewa madarakani, kushauriwa kustaafu na kukatwa mshahara. Nilikuwa napendekeza na hapa vile vile papatikane haki ya kusikilizwa katika ile *principle natural of justice* cheo chake.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, niliombe Baraza lako wakubaliane na pendekezo langu kwamba tuongeze vijifungu hivyo vya (3) na (4) nilivyovipendekeza katika majuweli ya marekebisho. Nashukuru naomba kutoa hoja Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, kuna mapendekezo hayo kuongeza vifungu vidogo viwili kifungu kidogo cha (3) na cha (4).

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, sina pingamizi na mapendekezo yake kwa kuongeza kifungu cha (3) ambacho kitasomeka;

"Endapo kiongozi hakuridhika na maamuzi ya Tume yaliyotolewa dhidi yake chini ya kifungu ya 27(1) cha sheria hii atakuwa na haki ya kukata rufaa ya uwamuzi huo wa Tume katika Mahakama Kuu ya Zanzibar".

Sina pingamizi hapo nakubaliana. Lakini namba (4) Mhe. Mwenyekiti, mimi sioni mantiki kwamba hichi cha (4) anachosema kwamba,

"Kabla ya kuchukua hatua dhidi ya Kiongozi wa umma anaelalamikiwa kuvunja maadili, mamlaka inayohusika itahakikisha kuwa Kiongozi huo anapewa fursa ya kusikilizwa".

Hapana, kusikilizwa keshasikilizwa kwenye Tume, keshapewa fursa, keshasikilizwa, kwa nini *to review* tena kusikiliza. Mimi nafikiri hapa si sahihi, fursa keshapewa huyu ya kutosha kabisa, tena turudie tena tumpe fursa nyengine, hapana hapo nafikiri si sahihi. Lakini kukata *appeal* baada ya adhabu kutolewa kwenye Mahakama hiyo ni sahihi haina tatizo, hiyo ni haki yake ya Kikatiba tena. Ndugu Mwenyekiti asante.

Mhe. Spika: Ehee, Mhe. Mwanasheria Mkuu unataka uongeze kitu kidogo, hebu zungumza.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Nizungumze kidogo tu, ni kuweka sawa Mhe. Mwenyekiti ule utaratibu kwa sababu kabla ya mapendekezo ya Mhe. Ismail Jussa ya kuongeza kifungu kidogo cha (3) na cha (4).

Pale mwanzo baada ya Tume kusikiliza na kutoa uwamuzi wake, ule uwamuzi wake ulikuwa unakwenda moja kwa moja kwenye mamlaka husika. Ile Mamlaka husika sasa itatekeleza na kutoa maamuzi yake kwa mujibu wa ripoti iliyotoka kutoka kwenye Tume. Anachopendekeza Mhe. Ismail Jussa ni kwamba hapana, tuongeze kifungu kidogo cha (3) kitakachompa huyu mtu sasa nafasi ya kuomba rufaa, kabla ya yale maamuzi hayajapelekwa kwenye mamlaka husika. Hilo halina tatizo ni sawa sawa.

Lakini kifungu kidogo cha (4) ndio hapa sasa inabidi tukubaliane Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba sasa yale maamuzi, au ile rufaa ikishakutoka Mahakamani, maana Mahakama ina uwezo wa kukubaliana na yale ambayo yameamuliwa na Tume au ina uwezo wa kukataa yale ambayo yameletwa na Tume, hiyo ndiyo kazi ambayo inaweza kufanya. Sasa kile ambacho kinaamuliwa na Mahakama hakiwezi tena kujadiliwa na Mamlaka husika. Mamlaka husika itabidi sasa itekeleze yale ambayo yametoka Mahakama aidha kwa njia ya Rufaa au kwa njia ya mapitia kama ambavyo Mhe. Ismail Jussa amependekeza kwenye kifungu kidogo cha (3). Sasa hiki kifungu cha (4) kidogo kitaleta matatizo, cha (3) hakina matatizo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimeiyona mantiki ya serikali na kwa misingi hiyo kwa sababu imekubali tukaongeza kijifungu cha (3), nakubali kwamba cha (4) tukiondoe na kwa hivyo nadhani tunaweza tukaendelea. Asante.

Mhe. Spika: Lakini labda tuelewana madhumuni hasa ya pendekezo la (4) kwamba baada ya hii hatua inayochukuliwa, baada ya rufaa au ni baada ya nini hapa. Maana hapa kabla ya kuchukua hatua, hii baada ya yule anaelalamikiwa uwamuzi uliotolewa na Tume kwa mfano, lakini baadae akaomba rufaa ambayo tunakubaliana chini ya kifungu kidogo cha (3) kwamba iwepo hiyo.

Sasa baada ya pale, baada ya rufaa utekelezaji ndio huu unaozungumzwa kwamba huu sasa uende moja kwa moja baada ya rufaa. *Okay*, kama tunakubaliana iwe baada ya rufaa kweli hii itakuwa haina haja. Nadhani tumekubaliana. Kama maamuzi yenyewe ya kuchukuliwa hatua ni yale baada ya rufaa basi haina haja tena kuisikiliza tena.

Kifungu cha 27 Tume Kutoa Maamuzi Pamoja na Marekebisho Yake.

Mhe. Spika: Marekebisho ya hapa ni ile kuongeza kifungu kidogo cha (3).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Siongezi jambo lolote Mheshimiwa nataka *records* zikae sawa tu kwamba tunaongeza hichi kijifungu cha (3) lakini pia kuweka sawa ile uloomba ufafanuzi punde nadhani pia Mwanasheria Mkuu tukiiangalia namna ya kukiandika vizuri zaidi 27(1). Kwa sababu hapa kilivyokaa ni kasema;

> "Baada ya kusikiliza madai au malalamiko na ushahidi uliotolewa, Tume itatoa maamuzi ama kiongozi kavunja maadili au hakuvunja na kupeleka taarifa kwa Mamlaka inayohusika kwa hatua zaidi."

Kwa hivyo, nadhani hichi kidogo inabidi kiandikwe vizuri ili ki-*reflect* hii ya kuingiziwa kijifungu cha (3) nadhani hatuna haja ya kufanya hapa, Mwanasheria Mkuu anaweza akakaa na Wizara ili kukiweka pengine na Wanasheria wa Baraza kuweka mkazo zaidi ili ki-*reflect* lile ambalo umelisema punde kwamba pana *processes* inaingia katikati katika 27(1), kabla ya kupeleka kwa Mamlaka husika.

Hofu yangu ni kwamba ukiwahishwa tu kwa mamlaka husika unaweza kuja kukuta kwamba tayari imechukuliwa hatua wakati wewe bado una - *strugle* na rufaa. Sasa rufaa ukifika hapo itakuwa sio tena dhidi ya Tume, itakuwa dhidi ya Mamlaka husika. Kwa hivyo nilikuwa nataka ikae vizuri zaidi katika *drafing* ningeomba hilo tu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Sawa Mhe. Mwenyekiti, tumeelewana.

Kifungu 27 Tume kutoa maamuzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 28

Mhe. Muhammedraza Hasanali Muhamedali: Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu wa jana katika kifungu cha 28 ukurasa wa 62 na kutoa hoja yangu kwamba ikiwa Tume hiyo inaundwa ya maadili ya sheria ambayo itakubalika katika uwasilishaji wake mahkamani, hoja yangu niliyoisema Mhe. Mwenyekiti, kwamba kwa nini Baraza hili la Wawakilishi, Baraza Tukufu ambalo linaongozwa na wananchi wa Visiwa vya Unguja na Pemba lisiwe na nguvu ya kamati zinapotoa ushahidi ikawa moja katika ushahidi wake mahkamani.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, sikumfahamu Mhe. Raza kusema kweli labda arudie.

Mhe. Mwenyekiti: Anasema ule ushahidi unaotolewa mbele ya Tume, huu unakubalika kama ushahidi mahkamani lakini ushahidi unaotolewa kwenye chombo hiki huo haukubaliki kutumika mahkamani kama ushahidi. Hebu tupe habari.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kifungu cha 28 hayo ambayo ameyauliza Mhe. Raza si sehemu yake. Sasa kama Serikali italeta mswada mwengine ambao utazungumza hoja ya Mhe. Raza nayo itakuwepo, mimi nadhani itakuwa siku yake ni hiyo. Lakini kwa leo madhumuni ya kifungu cha 28 nadhani kama kilivyoandikwa kiko sawasawa.

Kifungu 28 Ushahidi kutumika katika mahkama
Kifungu 29

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilitoa pendekezo kwamba Mhe. Waziri aondoshwe na jukumu la kuandika ripoti na sababu zangu zilikuwa ni kwamba mwenye Tume ni Mwenyekiti na ndie Mtendaji Mkuu, kwa hivyo kama ikiwa ndie Mtendaji Mkuu wa Tume yeye awe na wajibu wa kuandika ripoti na kuiwasilisha kwa Rais na Rais katika kuleta Barazani ampa Waziri wake ailete Barazani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, ninafikiri nilipokuwa ninajibu labda Mhe. Omar alikuwa nje kusema ushauri wake tumeukubali kwamba twende sambamba na utaratibu uliopo isiwe Tume inakwenda kinyume na utaratibu mwengine. Na huyu Mwenyekiti ana role mbili kama Mwenyekiti wa hiyo Tume, lakini pia anawajibika katika suala zima la kuandika ripoti kwa Mhe. Rais, kama leo alitoa mfano wa CAG halafu hiyo ripoti iletwe na sisi tukakubali ushauri wake twende sambamba na utaratibu huo.

Kifungu 29 Ripoti ya mwaka wa Kazi za Tume pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tano
Makosa na Adhabu

Kifungu 30 Hatua za kinidhamu.
Kifungu 31 Makosa chini ya sheria hii pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 32

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia kifungu hiki nilimshauri Mhe. Waziri kwamba adhabu iliyowekwa kifungu cha 32 kwa makosa ambayo yamewekwa hapa nilihisi madogo ukilinganisha na yale makosa ya kifungu cha 31 na adhabu zake. Kifungu cha 31(1) mpaka (2) mfanya kosa atalazimika kufungwa mwaka mmoja isidi miaka miwili na faini ya milioni moja isiozidi milioni mbili lakini ni makosa madogo zaidi kuliko yale makosa ya kifungu cha 32 ambayo kwa mtazamo ni makubwa zaidi. 32 makosa yake ni kutoa taarifa za uongo, mfano mtu anamiliki mali kubwa lakini amedanganya Tume, kwa adhabu yake miezi 6 kuliko yule ambaye kuwa amefanya makosa madogo cha 31. Kwa hivyo nilishauri kwamba 32 adhabu yake iwe kubwa zaidi kuliko 31.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka pia nilitoa maelezo Mhe. Hija labda bahati mbaya alikuwa nje lakini naomba nisisitize sisi mtizamo wetu kwamba kutoa siri tulihisi ni kosa kubwa zaidi kuliko kusema uongo kwa mtizamo wetu, ndio maana tukaweka adhabu kubwa kwenye kifungu 32, yeye anashauri iwe 32 kubwa sisi tumeona aa 31 tumeweka kubwa kuliko 32 kwa kosa hilo la yeye mfanyakazi, maana yake kama mfanyakazi anachukua siri anazitoa yeye ninafikiri hafai kufanya kazi hapo. Ndio maana tukasema aa bora yeye awe na penalti kubwa kuliko kusema uongo, kusema uongo kweli nalo ni kosa lakini pia nikamsisitiza kwamba hata ukitizama hizo adhabu zenyewe hazikupitana sana zimeshabihiana kidogo. Kwa hivyo

mimi nikamnasihi nikamshawishi Mhe. Hija akubali hilo pendekezo liliopo kwa sababu hazikupishana sana, lakini ile *magnitude* ya kosa la kutoa siri
ni kubwa zaidi na baya zaidi tena wewe ni mfanyakazi. Yaani unachukua mambo ya pale unayamwaga nje, kidogo ni kinyume cha maadili.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli mambo ya ndani kuyamwaga nje ni mtihani lakini ni kwamba 31 mfanyakazi ametoa siri nakubaliana na adhabu aliyoekewa kwamba milioni na si zaidi ya mbili, mwaka mmoja usiozidi miaka miwili. Lakini 32 sio mfanyakazi ni mtu yoyote tuchukulie mfano yule ambaye kuwa amezawadiwa 1.6 bilioni akae mbele ya Tume akasema kwamba mimi nimepewa milioni tatu ni mkosa. Kwa hivyo hata mimi kwa kunizawadia bilioni mbili baadae nikisema uongo adhabu yangu miezi 6 nitakubali. Kwa hivyo huyu ambaye amesema uongo kifungu cha 32 mtu yoyote sio mfanyakazi mtu yoyote ana mali kubwa ya umma lakini amesema uongo mbele ya Tume akijua yeye kwamba adhabu yake miezi 6 mtu wa kawaida atakubali aadhibiwe miezi 6 lakini akirudi miezi 6 basi akafaidi keki yake na watoto wake kwa bilioni kumi, kumi na tano.

Kwa hivyo huyu apewe adhabu kwa sababu amedogosha wizi alioufanya au ubadhirifu alioufanya kwa maslahi yake, sio mfanyakazi wa kawaida, mfanyakazi wa kawaida akitoa siri kufungwa mwaka mmoja lakini huyu ambaye kuwa amedanganya mali aliyonayo kwa maslahi ya umma halafu tunamfunga miezi 6 au faini yake milioni moja lakini ameiba bilioni tatu, nne nadhani Mhe. Waziri kwa mtu aliyezoea gerezani basi atakubali afungwe miezi 6 halafu akifunguliwa aje afaidi matunda na watoto wake. Nadhani adhabu iongezeke.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, hayo ambayo anayosema Mhe. Hija yeye hakupendekeza juu ambayo sasa yeye anaona iwe ambayo yeye anaona kubwa ni ipi sasa. Maana kama hii iliyokuwepo kwenye kifungu cha 32 yeye anaona ndogo iwe kubwa ya kiasi gani. Nadhani hiyo ndio hoja yeye amesema tu hii ni ndogo lakini hiyo kubwa anayopendekeza yeye ni ya kiasi gani ili sasa tujuwe tuweze kujadiliana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tuseme tu kwamba adhabu isiopungua mwaka mmoja na faini isiyopungua milioni tatu, kwa nini. Tunajua kwamba watasema uongo kwa shilingi elfu ishirini lakini je wale ambao kuwa na ha watu ishirini Mwenyekiti, sio wengi hawa hawasemi uongo, hawa hawasemi kitu wala sidhani kama hawa watakwenda kwenye Tume. Lakini wale ambao kuwa ni mang'we ng'we waliozoea kufanya mambo ndio wataosema uongo. Kwa hivyo adhabu iwe si chini ya mwaka mmoja na maamuzi mengine ya mahkama hata miaka ikiwa kweli amehujumu uchumi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hija unapoweka adhabu za aina hiyo maana yake chombo kinachotoa maamuzi kinaweza kuwa kuwa na miaka kumi, kumi na tano, ishirini, thalathini ukisema isiopungua maana yake unaacha mwanya mkubwa sana huko mbele tusije tukamuweka mtu pahala tukamsahau. Hebu tuizingatie vizuri kama nia ni hiyo tumsahau mtu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Hapana Mwenyekiti, sio kumsahau mtu wasiwasi wangu ni kwamba Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni kwamba huyu ambaye kuwa atasema uongo kwa mali kwamba yeye anajua kuwa mali aliyoibadhirifu kwa Serikali au kwa umma ni kubwa zaidi, akijua kwamba adhabu yake ni miezi 6 Mwenyekiti, watu wengine tofauti mimi na wewe. Mimi siku moja pale gerezani nitakufa, lakini kuna watu pale ndio maisha yao kwa kuchukua milioni mia tano, ukamfunga miezi 6 Mwenyekiti, hujamfanya kitu. Kwa hivyo busara Ofisi ya Mwanasheria Mkuu iangalie lakini isiwe miezi 6 sawa sawa na yule aliyetoa siri. Kutoa siri maana yake Hija ameiba na muda wa taarifa ukimhadithibia Mhe. Haji kwamba Hija ameiba lakini ni sahihi yeye ndio anafungwa zaidi kuliko yule aliyeiba akasema uongo. Nadhani Ofisi ya Mwanasheria Mkuu iangalie zaidi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kwenye eneo hili hakuna *blue-print* ya kusema kwamba bwana aa mtu anapofanya adhabu hii maana yake penalti apewe hii na kifungo chake kiwe hivi. Nadhani hayo tumekuwa tukiyazungumza muda mrefu hata kwenye miswada iliyopita ni kwamba ilikuwa sisi kama Serikali tutayarishe ile *sentence in policy* kama sasa iwepo ili ijulikane sasa kwa makosa haya adhabu yake itakuwa ni hii na faini yake itakuwa ni hii. Sasa ukisoma haya mengi yana lakini mimi tu nimkumbushe Mhe. Hija kama hiyo miezi 6 anaiona yeye kidogo kwa sababu yuko Barazani sasa hivi ndani, lakini kwa wale ambao wapo kule miezi 6 hii.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani miezi 6 hii inatosha kusema kweli.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli aliyeko ndani siku moja nimesema ni kubwa lakini hawa walioko ndani ni wale walioiba doriani na ndizi lakini chukulia milionea aliyetuangamiza kwa hivyo huyu aliyeko gerezani wa mwizi wa doriani na ndizi ndio akina Hija. Kwa hivyo mimi *concept* yangu ni kwamba wale ambao kuwa wameibia Serikali wameibia umma na nimetoa mfano niliangalia ile ya juzi kesi ndogo tu ya juzi 1.6 *billion* hivyo yule ukimwambia asamehe vile na aende miezi 6 mimi naona atasamehe miezi 6 afungwe ni tofauti na yule mtu wa kwetu bahati mbaya akachukua mkungu wa ndizi kwa mantiki hiyo Mwenyekiti. Lakini ikiwa mtizamo wa Serikali ni huo tuendelee lakini ninahisi adhabu zile Mwenyekiti ni ndogo kuliko ile ya kutoa siri. Maana siri jambo lipo lakini nimebahatika kulisema nimefanya umbea nimesema haraka ninapigwa mwaka mmoja. Lakini huyu aliyedanganya aliyeficha maovu ambao akishayafanya yeye miezi 6. Naona Mhe. Mwenyekiti, ni padogo lakini kama busara ya Mhe. Mwanasheria Mkuu ni hiyo sasa tuendelee.

Kifungu 32 Taarifa ya Uongo
Kifungu 33 Adhabu

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaendelea nadhani nimtoe wasiwasi wangu jirani yangu Mhe. Hija kwamba kifungu cha 32 sidhani kama kinahusu yale makosa ya viongozi kwa sababu yale yamewekewa taratibu zake mbali. Hawa ni wale wameitwa mbele ya Tume wametoa taarifa, kumtosheleza tu kwamba asiwe na wasiwasi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu mimi imejikita katika kifungu cha 33 kwa msingi mmoja, katika maoni au mapendekezo nililyompelekea Mhe. Waziri, nilipendekeza kifungu hiki kiondoke kwa sababu kinaweza kikatumia vibaya. Hoja yangu ni nini Mhe. Mwenyekiti. Ukikisoma kifungu hiki kinasema:

"Mtu yoyote ambaye atatiwa hatiani kwa kufanya kosa chini ya sheria hii ambapo adhabu yake haikuelezewa atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tatu za kitanzania au kifungo kichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka 3, au adhabu zote mbili za kifungo na faini".

Ukitizama Mhe. Mwenyekiti, kwanza adhabu iliyowekwa hapa ni kubwa kuliko iliyoko katika 31 na ile iliyoko katika 32. Lakini haya yametajwa makosa ambayo hayakutajwa adhabu yake. Sasa ninajiuliza kwanza Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeitizama sheria hii kwa kina kama sana kama nilivyosema. Pahala pekee ambapo panazungumzwa makosa na adhabu ni sehemu ya Tano hii tunayoijadili sasa hivi au tunayoipitisha sasa hivi. Na tayari imeweka utaratibu wenye makosa ya hatua kinidhamu katika kifungu cha 30, makosa chini ya sheria hii kifungu 31 na taarifa ta uongo kifungu 32, sasa kuna makosa gani tena nje ya haya ambayo yanawekea adhabu hii. Hofu yangu ni abuse Mhe. Mwenyekiti ya kifungu hiki na hasa kwa mambo haya tunayoyazungumza hapa.

Mhe. Mwenyekiti, ukisema kwamba mtu yoyote atatiwa hatiani kwa kufanya kosa chini ya sheria hii *is too general*, kufanya kosa ni kupi ni *offence* ama hata kukiuka maadili na miiko. Sasa hapo ninapoogopa kwa sababu anayekiuka miiko na maadili kaekewa taratibu zake tayari na bila shaka baada ya kuridhika baada hatua za kinidhamu kwamba pana suala la kupelekwa mahkamani akapelekwa mahkamani na akipelekwa mahkamani sheria sio inayofanya kazi itaingia sheria pengine ya rushwa na uhujumu uchumi na vitu vyengine kama vile.

Sasa mimi nilikuwa ninapendekeza Mheshimiwa kwa kuogopa *abuse* kifungu hiki kiondoke kwa mfano ili wajumbe wanifahamu, kifungu cha 18 Mhe. Mwenyekiti, kimetaja miiko ya kijamii. Sasa hapa umetajwa kwa mfano imeondoshwa ule ulevi wa kupindukia lakini imetajwa kiongozi asiwe na tabia za ulevi, uasharati, urupokwaji, utoaji wa siri, uzembe na kutojali matatizo ya wananchi, kushindwa kutunza familia na wazee wake, kushirikiana na watu wenye mienendo isiyokubalika, kushindwa kulipa madeni, kutumia kauli na lugha isiyofaa, ugomvi, unyanyasaji wa kijinsia na mengine mengi.

Sasa ukenda mbele katika kile kifungu cha 20 tulichokisoma imesema, kukiuka kifungu chochote cha sheria ni uvunjaji wa maadili. Hofu yangu tusije tukamfikisha mtu akaingia katika kifungu 33 kwa sababu tu ni mlevi au mropokwaji au muasharati au mengine ambayo yametajwa katika kifungu hiki. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kutoa indhari kwamba kwa kifungu hiki tutakuwa tumekwenda mbali sana Mhe. Mwenyekiti. Nadhani makosa ni yepi kwa sheria yashatajwa ndani ya sehemu hii 5 kwa kifungu cha 30, 31, 32 na adhabu ni zipi, kwa hivyo, kuwa na vifungu kama hivyo Mwenyekiti, naogopa sana kwa utaratibu kama huu tunaanza kuuzoea si mzuri. Kwa hivyo, tunasema kifungu cha 33 ningependekeza Serikali itukubalie kwamba kiondoke kwa sababu tayari makosa yametajwa na adhabu zimetajwa kwa ujumla wake Mhe. Mwenyekiti, na hatua za kinidhamu tayari zimewekewa

utaratibu wake, tukitoka hapa kuna mfumo wa kimahkama utachukua taratibu zake chini ya kanuni ya makosa ya adhabu na mengine kama hayo. Kwa hivyo nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, katika hili Serikali ione mantiki yake na ikubali kukiondoa kifungu cha 33.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, si makosa yote yaliyotajwa katika sheria hii kwa sasa ninafikiri utakubaliana na mimi Mhe. Jussa na hapa kwamba yeye ni mwanasheria basi akumbuke kwamba kwenye *penal act* namba 6 ya mwaka 2004 imeweka waziwazi kwamba si makosa yote yaliyotajwa adhabu zake, hilo ndio jawabu letu. Kwa hivyo haiku-*exhaust* na mfano nimempa hata hiyo penal act ya mwaka 2004 namba 6 si makosa yote yaliyotajwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi sikumfahamu labda nimuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu atusaidie zaidi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu sheria hii kufanya kazi yake inafanya kazi na sheria nyengine kama rushwa, uhujumu uchumi na sheria nyengine ambazo tayari adhabu zake zimeshawekwa kusema kweli. Sasa na kwenye hili *normal* tunafanya kwenye sheria nyingi ambazo tunapitisha hapa, tunaweka adhabu ya jumla kwa sababu inawezekana wakati mwengine kwenye vile vifungu ambavyo tumevitaja ndani ya sheria, lakini inawezekana adhabu yake ikawa hatukuitaja *than* unaweka kifungu kile cha mwisho cha adhabu ya jumla kama itapaotokezea kama hukutaja kifungu chochote, umetaja kifungu lakini hukuweka adhabu yake. Anachosema Mhe. Waziri ni kwamba kuna makosa mengine yametajwa na yamewekewa adhabu zake, lakini kuna mengine ambayo hayakuwekewa adhabu zake hiki ndio kifungu ambacho sasa kitashughulikia vile vifungu vyengine ambavyo havikuwekewa adhabu yake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimeelewa na ndio maana nikasema nimeupitia kwa kina mswada huu, ni kawaida mara nyengine unaweza kuwa na vifungu vya sheria katika sheria fulani vinavyosema kwamba ni kosa kufanya kadha, kadha, kadha halafu ikaishia pale isitaje adhabu. Kwa hivyo, kifungu kama hiki ndio kitakuwa kina-*cover* maeneo kama yale. Lakini mswada huu mzima Mhe. Mwenyekiti ukiondoa sehemu hii ya tano haina kitu kama hicho, ndio nikasema nimeusoma nimejiridhisha. Sasa hofu yangu nimesema ni nini? Ni kuja kuipa nafasi iwe pengine Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, iwe pengine ni Mahakama au mamlaka nyengine yoyote kuja ku-*abuse* kifungu hiki kwa kusema kwamba mtu yeyote ambaye atatiwa hatiani kwa kufanya kosa chini ya sheria hii. Hapa halikutajwa akachukulia kwa mfano kukiuka miiko ya kijamii akasema ni kosa chini ya sheria hii, na kule limetajwa kwamba ni kuvunja maadili.

Sasa haya maneno kosa ndio ninaloliogopa ndio maana nikasema ingelikuwa kuna kifungu chochote cha jumla kimesema kwamba kutenda kadhaa au kwenda kinyume na kifungu hiki ni kosa halafu ikasita pale, haitotaja adhabu kwa hivyo kifungu hiki ndio kingeingia. Lakini mswada mzima huu Mheshimiwa kuanzia mwanzo mpaka kwenye majadweli yake hapana pahala pengine popote palipotaja kwamba kuna makosa zaidi ya makosa ambayo yametajwa huku kwenye 31 na 32. Ndio maana nikasema hofu yangu ni hiyo tu na Mheshimiwa tuyatazame mambo haya dunia inabadilika kwa kasi anaweza mtu akataka kuja kumkomoa mtu katika sisi sisi humu ndani. Kwa hivyo, kama nilivyosema sheria hii inatuhusu sote humu, akaja akataka kumkomoa akatumia kifungu hiki akasema kwamba wewe ni mlevi kwa hivyo ulikosa chini ya sheria hii, kwa hivyo kifungu cha 33 kinafanya kazi wakati hilo si kosa la jinai.

Kwa hivyo, nilikuwa nasema Mhe. Mwenyekiti ndio maana nikasema tukitazame sana kwa kina sana, kwamba kuona utaratibu vifungu kama hivi katika mswada ambao haujataja popote kosa zaidi ya ilipotajwa hapa, kuna sababu ya kuendelea na kifungu kama hiki ndio nilikuwa nataka nisaidiwe hilo tu.

Mhe. Mwenyekiti: Hebu tuondoke kwenye *bad lock* hili Mhe. Jussa anachosema ni kwamba zipo baadhi ya sheria ambazo huwa zinataja kwamba mtu akifanya jambo fulani amefanya kosa, lakini kumbe adhabu ikawa haikusemwa pale kwamba mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa hili adhabu yake itakuwa hii. Ile adhabu ikaja ikataja jumla kwenye kifungu kingine ambayo itakuwa ina-*cover* pamoja na vifungu vile. Anachosema ni kwamba katika mswada huu hakuna kifungu cha aina hiyo ambacho kimetajwa kufanya jambo fulani ni kosa lakini adhabu yake ikawa haijatajwa. Makosa yaliyotajwa humu adhabu zake zimetajwa chini ya 31 na 32. Sasa ina haja gani kuwa na kifungu hiki, ndicho ambacho anauliza, inavyoonekana yeye hoja yake anasema hiki kifungu hakina haja Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, wala mimi sina haja ya kubishana na Mhe. Jussa kusema kweli, mimi nilichosema na ile mantiki niliyotoa mwanzo ni hiyo kwamba mara nyingi tunaweka kifungu hiki kwa sababu yake ni hiyo na yeye aliielewa. Lakini sasa inawezekana amejiridhisha yeye tu peke yake, na yeye ndio amesoma naona hakuna maeneo mengine ambayo haikutajwa adhabu ambayo haikuwekewa adhabu yake, yote yametajwa. Mimi nasema inawezekana yeye amesoma vizuri na amejiridhisha hivi na mimi wala sina haja ya kubisha wala haina haja ya kuweka mjadala kwenye mambo haya, kwa sababu kama nilivyosema sheria hii inatumika pia na sheria nyengine ya rushwa, sheria ya *penal*, ya *criminal* sheria nyingi zinatumika kwenye sheria hii. Kwa hiyo, mimi nakubaliana naye kusema kweli Mhe. Mwenyekiti kwenye hoja hii tuiondoe.

Kifungu 33 Adhabu nyingine pamoja na marekebisho yake

Mhe. Mwenyekiti: Marekebisho ni ile kuondolewa kifungu hicho.

Sehemu ya Sita

Masharti ya Fedha

Kifungu 34 Bajeti na Fedha

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hapa hoja yangu ni nyepesi mno tu kwa maana ya kwamba kufahamika ujue kwamba haina uzito. Kifungu cha 34 (2) Mhe. Mwenyekiti, na hili nafikiri rafiki yangu Mhe. Waziri wa Fedha atanifahamu suala linalohusu masharti ya fedha. Kinasema 34 (2) mlipaji mkuu wa serikali atateua Ofisa Muhasibu atakayesimamia fungu la bajeti la Tume na Muhasibu Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa masharti ya sheria hii atateua maofisa wa kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za uhasibu katika tume, nataka niishie hapo.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hapa niliyomuandikia Mhe. Waziri katika mchango wangu ambayo bahati mbaya haya ndio katika mambo hayakuwahi kufikia kuyatolea ufafanuzi, ilikuwa ni kwamba nahisi kwanza kuna mgongano wa maslahi. Kwa sababu sehemu kubwa ya sheria hii ikipita Mheshimiwa inahusu mambo yanayohusu mali zaidi, yako miiko ya kijamii, lakini kule kwenye maadili kwenye mgongano wa maslahi utaona imetajwa zaidi *financial interest* na vitu vyengine kama hivyo. Sasa katika hao watu ambao wametajwa katika jadweli la pili ni pamoja na hawa ambao wametajwa hapa, kwa sababu mlipaji mkuu wa serikali ninavyofahamu mimi ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha sijui kama alisaini *Paymaster General*.

Na Muhasibu Mkuu ametajwa katika hili jadweli la pili katika hao jumla ya watu ambao wanapaswa ku-*declare* mali. Sasa hofu yangu ni kwamba utaratibu tuliozoea ni kwamba masuala ya fedha ya taasisi yoyote yanakuwa wana mtendaji katika tume. Tume hii Mwenyekiti katajwa kwamba ndiye mtendaji mkuu, lakini bado wanao-*staff*, sasa nikasema kwa nini katika *staff* wake asiweko mmoja ambaye atakuwa ni dhamana kwa masuala ya utawala *including* kusimamia masuala ya fedha, badala yake kukiweka kifungu kama hiki kwamba huyu msimamizi wake wa masuala ya kibajeti na ya kifedha kwa sababu imetajwa ndiye atakayesimamia fungu la bajeti hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojua ukisoma kawaida katika mabuku haya ya bajeti, mimi yangu ninayo hapa ya mwaka uliopita, yanasema fungu hili la bajeti litasimamiwa na kwa mfano Katibu Mkuu wa Wizara. Sasa nahofia kwamba pakija pakitokezea *conflict of interest* pengine tume inamchunguza bosi wake yule aliyeteuliwa kutoka kwa *Paymaster* na kwa Muhasibu Mkuu kwa je hataingilia utaratibu kwa kuzuia bajeti tu Mheshimiwa kwa sababu yeye ndiye dhamana wa bajeti, na kwa sababu huyu kiutaratibu wanaoteuliwa na Muhasibu Mkuu wanawajibika kwake itakuwa vigumu sana kumuajibisha kupitia kwenye Mwenyekiti wa Tume, ndio maana nikasema kwamba *simple* tukawa tunakubaliana wala haina haja kukaa hapa na kuandika ikiwa ile itakubalika kwamba tuseme kuwa tume itateua katika watumishi wake Ofisa Mtendaji Mkuu ambaye atakuwa dhamana masuala ya utawala na fedha na ndiye atakayesimamia fungu la bajeti la tume ile badala ya kumuachia Muhasibu. Nilikuwa naomba mtazamo wa serikali katika hili.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, haya ambayo anayasema Mhe. Jussa kama ingekuwa hatuna sheria ya *Public Financial Act* Nam. 12 ya mwaka 2005 ingekuwa ni sahihi kusema kweli. Lakini ukisoma *Public Finance Act* kwenye kifungu cha 8 ambacho kinazungumzia *Accounting Officers* kinasema. *There shall be appointed by name and office and in writing by the Paymaster General an Accounting Officer* wa hiyo. Kwa hiyo, *accounting*

officer anayechaguliwa kwenye taasisi yoyote anachaguliwa na *Paymaster General*, yeye kwa mujibu wa sheria hii ndiye aliyetoa mamlaka ya kuchagua *accounting officer* ndio madhumuni ya kifungu hiki kusema kweli. Sasa tutapoandika vyengine vyovyote itakuwa tunakwenda kinyume na masharti ya sheria hii ya usimamizi wa fedha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani tutafautishe baina Muhasibu na *Chief Accounting Officer* na ndio ilikuwa hoja yangu. Ingelikuwa hakuna haya maneno katika kijifungu hiki kwamba mlipaji mkuu wa serikali atateua Ofisa Muhasibu atakayesimamia fungu la bajeti, ndio hofu yangu ipo hapo tu, wale wahasibu wengine aliowataja katika *Public Finance Act* ni wale wahasibu ambao wanakuwa *attach* atika wizara lakini hawasimamii fungu.

Mhe. Mwenyekiti, mabuku haya tunayoletewa hapa, haya ukiona katika fungu la bajeti kila mmoja katajwa nani dhamana. Kwa mfano, wizara ni Katibu Mkuu kama kwa mfano Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katajwa ni Mkurugenzi wa Mashtaka mwenyewe ndiye anayesimamia fungu la bajeti na inaandikwa hivyo. Sasa hapa ingelikuwa ni Muhasibu *general unless* kama wamekosea wao ku-*draft* itabidi atwambie hivyo tukubaliane kwamba hiyo ndio *intention* ya parliament katika kutunga sheria hawezi kusimamia fungu, kwamba fungu ni la Mwenyekiti kama ni mtendaji tuelewane hivyo.

Lakini hofu yangu kwa kubakisha maneno atakayesimamia fungu la bajeti la tume inawezekana kabisa Mhe. Mwenyekiti akawa *sabotage* Mwenyekiti na Tume yake *simple* kwa sababu kuna afisa ambaye kateuliwa na mtu ambaye anataka kumchunguza ni tofauti na *Chief Accounting Officer* kusimamia fungu la bajeti la mawizara na mengine kwa sababu hawa wanateuliwa na Rais hawateuliwa na *Paymaster General*. Kwa hivyo, nadhani kifungu cha *Public Finance Act* kwa maana ya maneno haya atakayesimamia fungu la bajeti itakuwa haingii ndio maana nataka tuelewane vizuri Mhe. Mwenyekiti hapo ili sheria yetu iwe safi, nzuri kadiri ya uwezo wake binadamu anavyoruhusu isiweke mianya ya kuja kuingilia utaratibu wa tume chombo kikubwa sana, kina kazi kubwa sana hicho Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, *ofcourse* ukisoma ile ya Kiswahili kidogo ndio inaleta utata. Lakini ukisoma ile ya Kiingereza *the Paymaster General shall appoint and accounting officer* na ambaye huyu uteuzi wake huyu *accounting officer* ndio unafanywa na kile kifungu cha 8 cha sheria ya *Public Finance Act.* Sasa inawezekana ya Kiswahili ni kweli inawezekana ile ukifanya tafsiri ile lugha iliyotumika sio sahihi. Lakini yaliyokusudiwa hapa ambaye msimamizi wa fungu hili ni huyu atateuliwa na *Paymaster General* kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha sheria Nam. 12 ya mwaka 2005. Kwa hiyo, hii ya Kiingereza iko sawa sawa anayeteuliwa hapa ni *accounting officer* (afisa mas-ul) nadhani siku hizi ndio lugha inayotumika ni afisa mas-ul ndiye aliyekusudiwa hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hiyo, sasa hapa kwenye mswada huu wa Kiswahili isomekeje Mhe. Mwanasheria Mkuu tusaidie.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Atateua Afisa Mas-ul hii mlipaji mkuu wa serikali atateua afisa mas-ul ndiye huyu *accounting officer* kwa lugha ya karibu nadhani ndio anavyoitwa labda Waziri wa Fedha anisaidie kama kuna lugha nyengine, ni huyu *accounting officer* ambaye ndiye atakuwa sasa dhamana wa hili fungu la tume. Sasa ukisoma kifungu cha 8 cha *public finance* ndio kinasema sasa *Paymaster General* atateua. Mimi nakubali kuna sheria nyengine tunaandika hivyo moja kwa moja kama mtu fulani ndio atakuwa yeye msimamizi wa hilo fungu. Lakini masharti ya sheria ya utumishi wa umma kwenye masharti ya sheria hii ya Nam. 12 ya 2005 inaelekeza hivyo kama *accounting officer* yeyote anateuliwa na *Paymaster General* tena imesemwa *by name and office and in writing* ndio anateuliwa. Kwa mfano Wizara ya Fedha Katibu Mkuu Wizara ya Fedha sio *accounting officer, accounting officer* ni Naibu Katibu Mkuu ambaye ndiye amechaguliwa.

Sasa nasema ni hivyo inavyokwenda ndio madhumuni ya kifungu hiki kusema kweli, sasa iliyokusudiwa hapa ni huyu *accounting officer* na wala sio Afisa Muhasibu hili neno Afisa Muhasibu limechanganya ni Afisa Mas-ul.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa hakika mimi hasa hata lingebakia hilo Afisa Muhasibu halinipi shida kuliko haya maneno yaliyofuatia atakayesimamia fungu la bajeti la tume. Hili jina awe Afisa Mus-ul, Afisa Muhasibu mimi hata halinipi shida, haya maneno yanayofuata atakayesimamia fungu la bajeti la tume ndio linapokuwa na matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwa sababu sheria tunaisoma kwa ujumla wake hatuisomi kifungu kimoja peke yake. Ukiangalia kifungu cha 36 kinasema Mwenyekiti ndani ya miezi mitatu kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha atatayarisha na kuwasilisha kwa waziri makadirio ya mapato na matumizi ya tume ya mwaka uliofuata. Kwa hivyo, unamuhisi kwamba mwenye fungu la bajeti ni Mwenyekiti wa Tume kama ambavyo pengine *DPP* analo kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, kama vile ambavyo Mwanasheria Mkuu analo pengine katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kwa hiyo, ndio maana nikasema kwamba nadhani hapa tunaweza tukapata shida katika ku-*draf* lakini tukielewana kama mantiki ndio hiyo tuachiwe, lakini ieleweke kwamba huyu si *accounting officer* kwa maana ya kulisimamia fungu kama vile inavyoandikwa humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti, labda ili nifahamike tuangalie mfano mmoja hapa, inasema kwamba Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati makadirio ya fedha zinazohitajika kwa mwaka kwa ajili ya mishahara imetajwa, halafu anasema vifungu vya vifungu hili vinavyooneshwa hapo chini matumizi yake yatasimamiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na hii iko hata kwa ambao si mawizara. Sasa ndio maana nikasema tatizo langu si jina, tatizo langu haya maneno atakayesimamia fungu la bajeti la tume. Nilivyoelewa mimi kwa kukisoma kifungu cha 36 ni kwamba Mwenyekiti ndiye anayesimamia fungu la bajeti sio *accounting officer*. Kwa hivyo, tukiyarekebisha haya nafikiri unaweza kurekebisha baadae tunaweza tukapata msingi mzuri wa sheria hii ili kuja kuondosha kuja kutumika vibaya Mheshimiwa. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa tunakwendaje kwa sababu maana humu inavyoonekana kwamba mwenye dhamana hiyo ni Mwenyekiti kwa humu, lakini sasa kunaingia hapa kwamba kuna Katibu Mkuu Fedha, sasa hebu tupeni maelezo tukae vizuri.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mimi nasema kwa mfano hiki kifungu cha 34 (2) tungeweka moja kwa moja Mwenyekiti ndiye atakayekuwa Afisa Mas-ul atayesimamia fungu la bajeti la tume, nadhani ingeeleweka moja kwa moja. Anachosema Mhe. Jussa ni kwamba huku kwenye kifungu kidogo cha (2) tumemuachia mamlaka mtu mwengine wa kuteua *accounting officer*, lakini unaposoma kifungu cha 36 *as if* yule *accounting officer* tayari tumeshamteua kama atakuwa Mwenyekiti. Sasa inawezekana ikaleta mgongano kama kifungu cha 34 (2) akawa mtu mwengine, lakini sheria imeshataja tayari kama kwamba Mwenyekiti huyu ndio atakuwa…

Sasa mimi nasema cha 36 hatukufika lakini tutapofika itabidi sasa kisomeke kama ambavyo kinasomeka kifungu cha 34 (2) kama badala ya Mwenyekiti iwe sasa *accounting officer*.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sasa Mhe. Mwanasheria Mkuu kanikoroga zaidi, kwa sababu msingi wa hoja yangu ulikuwa ni *conflict of interest* hiyo nimejengea hoja tu, msingi wangu ni *conflict of interest* kwamba ukimfanya *Chief Accounting Officer* ni muhasibu anayeteuliwa na *Paymaster General* unakaribisha mgongano wa *master* itapotokezea kwamba anayechunguza pengine iwe *Pay Master General* au Muhasibu Mkuu. Sasa mimi nilidhani pale mwanzo alivyoanza nilikuwa nataka kumfahamu nilidhani anakwenda kule, kwamba tuseme kuwa hapa Mhe. Mwenyekiti labda ili tufahamiane ukisoma hii sehemu imesema masharti ya fedha na *marginal note* inasema bajeti na fedha za tume. Na kifungu cha 34 (1) kimeanza kusema tume itakuwa na fungu lake la bajeti kwa ajili ya fedha zote zitakazoidhinihswa na kutumika na tume.

Kwa hivyo, unaifahamu unakuja 34 (2) kwamba ina-*support* 34 (1). Sasa ndio maana nikasema kwamba tukimuweka hapa tuna matatizo kwa nini Mwenyekiti kama ambavyo *DPP*, kwa sababu Mwenyekiti huyu ana mamlaka tofauti na Mwenyekiti wa Kamisheni na vitu vyengine asiwe yeye mwenyewe ndiye *Chief Accounting Officer*. Na kama alivyosema sana Mhe. Waziri katika kujibu vifungu vyengine kwamba Mwenyekiti ndiye mtendaji mkuu wa chombo hiki ndio hoja yangu. Na kama hoja aliyoisoma Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba hapa panahitajika kuteuliwa mhasibu tu, hatuna haja ya kuweka hapa, kwa sababu *Public Finance Act* aliyoisoma punde hivi tayari ina kifungu cha jumla kinacho-*cover* taasisi zote za serikali, sasa kwa nini tutaje hapo. Yeye anasema hapa kwa sababu panazungumziwa fungu la bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, *vote* tutakuja kuipitisha humu ndani. Nadhani wala sidhani kama kuna *precedent* ya namna hiyo, kwamba kuna mhasibu wa kawaida aliyetolewa *Paymaster General* akawa ndio mwenye *vote* haijapata kutokea. *Vote* siku zote humu ndani ukisoma Mheshimiwa ni wateule wa Rais kwa uzito wake.

Kwa hivyo, nadhani akubali tu Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba hapa tuseme mwenyekiti ndiye mwenye fungu na kama kunahitajika kuwa na kifungu cha kuzungumzia *accounting officer* tayari *Public Finance Act* ipo ina-*cover*

wote, kwa hiyo haina haja ya hata kuwekwa. Nadhani lile pendekezo la awali ndio likubali kwamba 34(2) ianze kwa kusema mwenyekiti ndiye atayekuwa msimamizi wa fungu la bajeti kwa nafasi yake, kama mtendaji mkuu wa tume kama ilivyosemwa kule mwanzao kabisa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kama nimemfahamu Mhe. Ismail Jussa kwa maneno mafupi sana ni kwamba, mwenyekiti wa tume atakuwa na *roll* mbili, moja kama mwenyekiti wa tume lakini ya pili kwamba yeye pia ndiye atakuwa *accounting officer*. Sijui kama ndio unavyozungumzia hivyo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ndiyo na ili nikusudie zaidi naomba urejee kifungu cha 5(1)(a) kinachosema: "Mwenyekiti atakuwa ni mtendaji mkuu na atakuwa na dhamana ya utekelezaji wa kazi za kila siku za tume". Huyu si mwenyekiti kama wenyeviti wengine na ndiyo maana ana-*lead* hii taasisi maalum. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Mhe. Mwanasheria Mkuu tuwekee sawa ili tuendelee.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, hayo kifungu hiki kinazungumzia masharti ya fedha, kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa kwamba ile *vote* ambayo inapitishwa na Baraza lazima iwe na msimamizi wake ndivyo kinavyosema kifungu hiki, kwamba tume itakuwa na fungu lake la bajeti kwa ajili ya fedha zote zitakazoidhinishwa na kutumika na tume. Kifungu cha 34(1).

Kifungu cha 34(2) hiki sasa ndicho kinamteuwa huyo ambaye atahusika kusimamia hizo fedha ambazo zitaidhinishwa na Baraza, kwa Kiingereza anaitwa *Accounting officer*. Mimi nikasema kwa Kiswahili inawezekana ninachosikia cha kila siku anaitwa ni Afisa Mas-uli, yeye ndiye atakuwa anasimamia sasa hilo fungu lililopitishwa na Baraza. Sasa utaratibu uliowekwa na sheria hii ya *Public Finance* ni kama *Paymaster General* ndiye aliyepewa mamlaka ya kuteuwa hao *Accounting officers* na ndio kifungu hiki cha 34(2) kinavyosema. *Paymaster General* kwa mujibu wa masharti ambayo amepewa na sheria hii ya *Public Finance Act* ndio atateuwa *Accounting office*.

Mimi natambua tuna sheria nyengine nyingi tunazozitunga tunaandika kabisa kama mtu fulani, hata ile sheria yetu tunayoitunga ya Ofisi ya *AG* haisemi kama *AG* ndiye *Accounting officer* inasema kama ilivyoandikwa hii. Kwa sababu tumetambua kama kuna masharti ya sheria ya *Public Finance Act* kama *Paymaster General* ndio sasa atateuwa mtu, ngoja nikisome.
Kifungu cha 8(1) kinasema:

> *"There shall be appointed by name and office and in writing by the Paymaster General an Accounting office who shall be normal the Principal Secretary", normal ndiyo inavyosema. "of the respective Ministry or head of department in respect of each expenditure vote, who shall control and be accountable for the expenditure...",*

Hivyo ndivyo kinavyosema. Sasa huyu mtu uteuzi wake lazima ufanywe *by name, by office and in writing by the paymaster general* ndio inasema. Kwa hivyo, hiki kifungu kilivyoandikwa kiko sawasawa hakijakosewa.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri tatizo linalokuja hapa ni kwamba madara ya utendaji amepewa mwenyekiti ndio suala linalokuja hapa, yeye ndiye mwenye madara ya utendaji. Barazani hapa madaraka ya utendaji kapewa huyu katibu na yeye ndiye *Accounting officer*. Sasa nafikiri ndio tatizo linalokuja hapa, sijui tunafanyaje. Kwa sababu utendaji tumeuzungumza kwenye ibara ya 5 kwamba huyu mwenyekiti ndiye atakuwa mtendaji mkuu na atakuwa na dhamana ya utekelezaji wa kazi za kila siku za tume, ukimsema kwamba ni mtendaji mkuu hebu tuiangalie hiyo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba sana nisionekane mbishi nataka kusaidia chombo chako. Hivyo ulivyozungumza Mheshimiwa naomba turejee katika mswada wa Kiingereza sasa ili tufahamu vizuri zaidi, hicho kifungu ulichokisema cha 5(1)(a).

Kifungu cha 5(1)(a) kinasema kwamba;

> *"The chairman shall be the chief executive officer, CEO and shall be responsible for the day to day function of the commission".*

Mhe. Mwenyekiti, ndiyo nikasema kwamba huyu ni tofauti na wenyeviti wengine, lakini kama ninavyosema msingi wa hoja yangu hasa wala hauko huko, msingi wa hoja yagu ilikuwa ni *conflict of interest*. Lakini nataka nimwambie, nafikiri tunapopishana lugha baina yangu na Mwanasheria Mkuu ni pamoja yeye ananisomea *Public Finance Act* ambayo mimi sina matatizo nayo kabisa, hawa ni Wahasibu Wakuu wa taasisi, hawasimamii *vote* Mhe. Mwenyekiti. Naomba anitajie yeye *precedent* katika nchi hii ya taasisi ipi yenye *vote* ambayo ina afisa wake anayesimamia *vote* aliyekuwa si mteule wa Rais, kwa maana ya mkuu wa chombo kile akawa ni mteule wa *paymaster general*, anitajie pamoja tu akinitajia nitasema tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti, msimamizi wa *vote* sio mhasibu, Mhasibu Mkuu wa taasisi najua wapo na najua wanaongozwa na *paymaster general* wanateuliwa na yeye chini ya *Public Finance Act*, huyu si Mhasibu Mkuu. Hapa wanapotajwa kwamba watasimamia fungu la bajeti tunampa dhamana ya *vote*.

Sasa kama katumika na aliyemteuwa kwa sababu anataka kuchunguzwa akamzuilia *vote* na tume yake nani atabeba jukumu hilo, ndio maana nasema tuna-*create precedent* ambayo haipo. Mhe. Mwanasheria Mkuu katika hapa anaposema kwamba tunayo ni sawa, lakini anai-*miss* kabisa *point* yangu sizungumzii wahasibu wakuu nazungumzia mwenye dhamana ya *vote*.

Mhe. Mwenyekiti, Mhasibu Mkuu wa taasisi yoyote hana dhamana ya *vote*. Mhasibu Mkuu wa taasisi yoyote hana dhamana ya *vote* mwenye dhamana ya *vote* aliyetajwa katika kitabu cha *vote* hiki hapa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani nimezungumza mengi na nilichozungumzia mimi kwa mfano, kuna tofauti ya *accountant general* na *accounting officer*. *Accountant general,* Mhasibu Mkuu wa Serikali sasa hivi ni Ndugu Omar Hassan, yeye ndio anateuwa sasa wale wahasibu wa kuja kufanya kazi zetu maofisini kuandika *voucher* na mengineyo, lakini zinapotoka kwa wale wahasibu zinakwenda kwa *Accounting officer*, Afisa Mas-uli yeye ndiye aliyepewa dhamana ya kusimamia ile *vote* ya ile taasisi yake ndio kifungu hiki kinavyosema, wala hatuzungumzii wahasibu, tunazungumzia ni *Accounting officer* mwenye dhamana ya ile *vote*.

Sasa labda mimi sieleweki kwa sababu si lugha yangu mambo ya fedha, lakini kwa sababu Mhe. Waziri wa Fedha yupo ningemuomba atusaidie kwenye hili.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusikia mjadala labda niseme tu wasiwasi wa Mhe. Ismail Jussa katika kifungu hiki ambacho Mwanasheria Mkuu anakizungumzia. Katika hii sheria ambayo tunaizungumzia kutakuwa na mtendaji ambaye anashughulikia na masuala ya fedha, ambaye huyu ndiye tutakaemwita Afisa Mas-ul. Huyu atateuliwa na Katibu Mkuu wa Fedha hata hawa Makatibu Wakuu nao huwaona Rais anawatangaza, lakini zile kazi za kusimamia fedha wanapata barua kutoka kwa Katibu Mkuu Fedha za uteuzi kwamba sasa wewe nimekuteuwa kusimamia mafungu ya Wizara ya Afya, nimekuteuwa kusimamia mafungu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na huyu vile vile atateuliwa kusimamia mafungu yaliyomo katika tume. Hilo la kwanza.

La pili, Mhasibu Mkuu sasa ambaye kwa sasa hivi ni Ndugu Omar Hassan maarufu tunamwita Kingi, na yeye anapaswa kumteuwa mhasibu atakayefanya hizo kazi za uhasibu ndani ya hii taasisi na huyu huyu ndiye anayewateuwa hawa wahasibu katika taasisi zetu, anayeteuwa wahasibu wakuu kwenye mawizara yetu, anateuwa wahasibu wakuu katika mamlaka, ndiye yeye. Kwa hivyo, hizo kazi mbili zitafanyika kwa watu wawili tofauti.

Ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu alisema kwamba, huyu mwenyekiti ni *CEO*. Hata ukitizama hizi *private company* zenye ma-*CEO* kuna *director* wa *finance*, wakurugenzi wa fedha ambao wanasimamia zile fedha. Sasa hapa kwa sababu kwetu sisi tunaita Maafisa Mas-uli ndiye huyu ambaye atakaeteuliwa kwanza na Katibu Mkuu Fedha halafu Mhasibu Mkuu atateuwa mhasibu wa kushughulikia hizo fedha.

Kwa hivyo, hiki kifungu ukikifanya vyenginevyo tutakwenda tafauti na sheria ya fedha, *The Public Finance Act*. Kwa hiyo, mimi nadhani Mhe. Ismail Jussa tukubaliane tu kwamba hii ndio taratibu na kila mmoja atapewa majukumu yake kwa mujibu wa kushughulikia hii na lazima tukubali kwamba hii taasisi bado itaendelea kuwa ni taasisi ya serikali na hii taasi bado itakuwa inapata *sub version*, inapata ruzuku kutoka serikalini na lazima zisimamiwe zile ndio hawa ambao walikuwa wanaelezwa katika sheria hii.

Sasa kama kuna cha ziada sijui tusaidiane vipi ili Mhe. Ismail Jussa tuweze kufahamiana, lakini kwa mujibu wa sheria hii ilivyokaa ndio hivyo ambavyo ninavyoiona mimi, inatakiwa kuelekezwa huko. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Tuwe pamoja sote ili tuweze kufahamiana. Mwenyekiti wa Tume hapa ndiye aliyetajwa kwamba ndio *chief executive office*. Je, ni huyu huyu ndiye atapata barua ya Katibu Mkuu kusimamia hiyo *voucher*?

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Anaweza akawa yeye au Katibu Mkuu Fedha akaamua awe mwengine, *it is not necessary* awe ni yeye, *it is not* kusema kweli.

Mhe. Mwenyekiti: Ili kumpa mamlaka ya uendeshaji wa tume yake sisi tunaona iweje, sisi watunga sheria humu ndani na ndio tunafanya kazi hiyo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwamba umeelewa hasa msingi wa hoja yangu katika swali ulililoliuliza. Hoja yangu nasema nimemuelewa sana Mhe. Waziri wa Fedha aliposema wale watendaji wakuu wa taasisi wanapewa barua na *Paymaster General* utaona anachofanya ni *nearly formality* ni ile kwamba ana-*confirm,* lakini utakuta hakuna hata mmoja wale kwamba anapata uhalali wake kutoka kwa *Paymaster General* kwa sababu wana sheria zao, iwe ni sheria ya utumishi wa umma au ni sheria nyengine iliyoanzishwa ambayo inataja wateuliwe.

Mara nyingi hawa kama alivyosema Mhe. Mwenyekiti, sijui kama ni mara nyingi au mara zote kwamba watakuwa ndio *chief accounting officer* wanasimamia *vote*. Lakini ni wateule wa Rais. Sasa kama nilivyosema katika hili pengine tatizo limekuja katika ***world*** *drafters* wa hii sheria, kwamba mwenyekiti wamemfanya ana *staff* lakini hawakumpa katika wale *staff* nani mkuu wa ma-*staff* ambaye ndiye pengine angeteuliwa akawa huyu *chief accounting officer*, badala yake wamemwita mwenyekiti ni *chief executive officer* tena sio *chief executive officer* ni *responsible for the day to day function of the commission*.

Mhe. Mwenyekiti, wewe ukiwa katika mamlaka yako mengie sio ya kamati hii ni Spika, lakini wewe *you are not responsible for the day to day function of the* Baraza, mwenye *responsibility* ya *day to day function* ni katibu wetu wa Baraza. Hivyo hivyo waziri ni kiongozi wa wizara lakini sio *chief executive officer, chief executive officer* ni Katibu Mkuu na hivyo hivyo kwa taasisi nyingine. Kama ninavyosema ziko taasisi kwa mfano, Ofisi ya *DPP* natoa mfano tu, ambao *DPP* mwenyewe mkuu wa ofisi ndiye pia anayesimamia *vote*. Sasa hapa napata mashaka kwamba chombo kikubwa kama hiki kinachokwenda kusimamia maadili ya viongozi ambayo mengi yanayohusiana na masuala ya mgongano wa maslahi na masuala ya kifedha, halafu wale watendaji wakuu wa masuala ya fedha na tunajuana humu ndani sitaki kusema mengi, ingawa hatupaswi kutizama watu.

Kwamba leo unamfanya *Paymaster General* na Mhasibu Mkuu na hasa kama ilivyo yuko kwa *Paymaster General* kwamba ndiye anayepeleka mkuu wa kusimamia *vote* katika chombo kama hiki, akiamua huyo anapofika kuchunguzwa yeye aka-*sabotage* tutakuwa na mamlaka gani ya kuendesha tume Mhe. Mwenyekiti.

Pia, kuna nukta nyengine nilikuwa naambiwa hapa kwamba *chief executive officers* wote kwa maana ya *chief accounting officers* wanatakiwa wajieleze mbele ya *PAC*. Je, najiuliza mwenyekiti wa tume ile ambayo inatuchunguza sote anaweza kuitwa mbele ya *PAC*? Kwa hivyo, tuna matatizo ndio maana nikasema kuna mgongano wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema najua binadamu mara nyingi hatutaki kukiri kwamba tumepitikiwa na jambo, lakini tangu nilipokuwa nikiusoma mswada huu nilikuwa najiuliza hii seketerieti ya tume wale watumishi mkuu wao ni nani? Hatukumuweka katika mswada hapa, badala yake tumesema mwenyekiti ndiye mtendaji wao mkuu. Sasa kama ndio yeye mtendaji wao mkuu abakie kuwa *responsible* na fungu lake na kama tunataka kuweka Ofisa Mas-uul wa maana ya uhasibu tuseme hii iko kwenye *Public Finance Act.* Lakini kumfanya ofisa anayeteuliwa sio kuwa *confirmed* tu kwamba Katibu Mkuu wa wizara fulani wewe ndiye mkuu wa *vote* kwamba yeye ndiye anamteuwa afanye mawasiliano. Mhe. Mwenyekiti, mimi hilo siwezi kuliunga mkono hata kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Mwanasheria Mkuu. Nataka tuondoke hapa mana tumechukua muda mkubwa sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli lakini mimi nasema haya yaliyoandikwa hapa sio mara ya kwanza kuandikwa kusema kweli, hayo yaliyoandikwa kwenye kifungu hiki kidogo cha (2) sio mara ya kwanza yameandikwa hapa. Mimi nataka nisome sheria ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kifungu cha 8.

Kifungu cha 8(1) kinasema:

> *"The Office shall hold its own budget vote through which all the funds appropriated or accrued for the use of the Office shall be disbursed"*.

Hicho ni kifungu cha 8(1).

Kifungu cha 8(2) kinasema:

> *"The Paymaster General shall appoint an accounting officer for the Office Vote and the Accounting General..."*

Hakutajwa *DPP* humu, hivyo ndivyo kinavyosema. Sasa hiki kifungu kilivyo hakina makosa, hiki cha 8(2) ni sahihi na kimekuwa sahihi kwa sababu usahihi wake umepatikana kwenye sheria ya *Public Finance Act* ndio inavyosema.

Sasa hayo mengine yote anayosema Mhe. Ismail Jussa ndio hali ilivyo. Mimi nasema natambua wala sibishi kwenye sheria nyengine tunaandika moja kwa moja maana yake ile kazi aliyopewa *Paymaster General* tunamfanyia kwenye sheria wakati utaratibu sio huo. Utaratibu ni ule uliowekwa kwenye sheria ya fedha kwamba *Paymaster General* ndiye ata-*appoint* na nimetoa mfano, Wizara ya Fedha Katibu Mkuu wa wizara sio *accounting officer,* Mhe. Waziri wake yupo hapa, Naibu Katibu Mkuu ndiye *accounting officer* wa ile wizara. Sasa haina maana yule kiongozi ndio yeye awe *accounting officer*.

Mwenyekiti: Basi tufikie pahala tufanye maamuzi kwamba kifungu kwa mtazamo wa serikali hivi kilivyo ndio sawa sawa, ehee taarifa.

TAARIFA

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, walivyokuwa wakizungumza Waheshimiwa wote wawili nilikuwa nimetulia sana nasikiliza, hoja zote mbili zina uhakika. Sheria ya fedha haijakosea wala hoja ya Mwanasheria Mkuu na ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu haijakosea. Tatizo lililokosewa hapa ni kwamba mlipaji mkuu wa serikali atateuwa afisa mhasibu, hakuna mlipaji mkuu wa serikali na hateui afisa mhasibu anateuwa *accounting officer*. Afisa Mhasibu huteuliwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu Yahya Khamis wa Baraza la Wawakilishi ni mlipaji Mkuu *Accounting Officer*. Lakini Shekhe Hassan ni Muhasibu Mkuu Baraza la Wawakilishi aliteuliwa kwa barua na Muhasibu Mkuu wa Serikali, kwa hivyo ni watu wawili tafauti na hivyo ndivyo Mhe. Waziri alivyozungumza.

Nimekaa kwenye *PAC* na Kamati ya Fedha miaka yote lazima *Accounting Officer* ateuliwe na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kwa barua. Sasa hii kwanza Afisa Muhasibu iondoke iwe ni Afisa Mas-ul na nini maana yake. Maana yake ni yule ambaye anawajibikia mbele ya Baraza la Wawakilishi kwa utendaji. Sasa wala lisikupe tabu kwamba huyu mwenyekiti huyu ukiwapelekea hii Sheria Wizara ya Fedha ukimwaambia Wizara ya Fedha uteuwe Mas-ul yeye atakuwa anajua kwamba Afisa Mas-ul atakuwa anawajika na shughuli za fedha katika taasisi fulani.

Kwa hivyo, nina hakika mia juu ya mia, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha atamteuwa mwenyekiti wa Tume hii kuwa ndie Afisa Mas-ul na Muhasibu Mkuu nina hakika atamteuwa Mhasibu wa Tume hii kuwa Muhasibu wa Tume. Kwa hiyo, hii iondoke hii Afisa Muhasibu ibaki *Accounting Officer*.

Ukiachilia mbali Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya CAG kwa sababu maalum hata hiyo Ofisi ya Mtunza Mashtaka nina hakika Murugenzi Mashtaka ndie *Accounting Officer*. Ukiwachia mbali ofisi hizi mbili na kwa sababu zake maalum ambazo Wizara ya fedha wametusomesha kuna sababu maalum za msingi ndio Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha akasema hii *Power* nai-*delegate* kwa Naibu wangu kwa sababu ya msingi maalum.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangi tusiipoteshe hii sheria kiasi hicho, tukubaliane hivi iandike:-

Mkupaji Mkuu wa Serikali atateuwa Afisa Mas-ul wa Tume. Ukiwapelekea Wizara ya Fedha nina hakika watakuwa wanajua hawa kwa sababu wao sheria za fedha wanajua, huu ndio ushauri wangu. Hii Afisa Muhasibu tuiondoshe

tuweke Afisa Mas-ul ili wao Wizara ya Fedha watakuwa wanajua nani Afisa Mas-ul Mhe. Mwenyekiti, huu ndio ushauri wangu.

Mhe. Mwenyekiti: Haya unataka kusema kitu Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Nasema ana hivyo ndiyo tulivyokuwa tukisema tokea muda huo wote. Kwamba hii Afisa Muhasibu iondoke iandikwe Afisa Mas-ul. Mimi nakubaliana na Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hiyo, sasa tunarekebisha kwamba mlipaji Mkuu wa Serikali atateuwa Ofisa Mas-uli sio Ofisa Muhasibu sawa. Basi wacha tuingize hiyo kama ndio msimamo huo waulize Wajumbe kama wanakubaliana nayo.

Kifungu 34 Bajeti na Fedha za Tume pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Mwenyekiti: Marekebisho ndiyo hiyo kuweka Ofisa Mas-ul. Baada ya Ofisa Muhasibu haya.

Kifungu 35 Hesabu na Ukaguzi

Kifungu 36 Makadirio

Kifungu 37 Ripoti ya mwaka wa fedha pamoja na marekebisho yake

Kifungu 38

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hichi naomba maneno yaliopo katika mstari wa pili kwa amri iliyotolewa na kusainiwa na waziri yaondolewe.

Mhe. Mwenyekiti, hapa pana mamlaka ya Mwenyekiti na ili ifahamike hoja yangu naomba kisome kinasema:-

Kinasema 38(1) mwenyekiti, anaweza kwa madhumuni ya utekelezaji wa kazi zake chini ya sheria hii. Sasa hapa imeandikwa kwa amri iliyotolewa na kusainiwa na waziri kukagua na hesabu ya mtu yoyote ambaye Tume ilitaka kuthibitisha kuhusu akiba yake ya benki, hisa mamuzi, matumizi, kasha lolote au daftari la kuwekea kumbukumbu za kifedha katika Taasisi ya Fedha na 38(2) inasema:-

Mara ya waziri kutoa amri chini ya kifungu cha kwanza cha kifungu hiki mwenyekiti ataipeleka amri hiyo kwa mkuu wa Taasisi ya Fedha inayohusika na Mkuu huyo atawajibika kutoa taarifa hizo.

Hoja yangu ni kwamba kama nilivyosema mwanzo Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi wa sheria hii najua amra nyingi sheria nyingi zinawapa mawaziri. Lakini kwa uzito wa sheria hii waziri mwenyewe akiwa ni *subject* wa sheria hii nadhani kumfanya Mwenyekiti wa Tume kwamba hawezi kukagua haya yaliyotajwa hapa mpaka apate amri iliyotolewa na kusainiwa na waziri tunaingiza matatizo.

Kwa hiyo, kwamba 38(1) kwa amri iliyotolewa na Mhe. Waziri maneno haya yaondoke lakini vile vile cha 38(2) kiandikwe katika hali ambayo itaondoa ile sharti la kupata amri ya wazirin ahsante Mhe Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naona hakuna tatizo madhali tumempa dhamana Mwenyekiti wa Tume na kama anavyoshauri basi kuodosha hiyo utata huo basi tuondoe si lazima isainiwe na waziri mie nakubali.

Kifungu 38 Mamlaka ya Mwenyekiti pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 39 Kinga ya Jumla pamoja na marebisho yake.

Kifungu 40 Misingi inayopaswa kukuzwa na Maadili pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 41 Kanuni

Kifungu 42

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hapa nina nukta ndogo na nadhani msingi wake ameshaukubali waziri kule wanzoni kabisa. Kwa hiyo, nilikuwa nataka niukumbushe tu tuweke tena kwamba kifungu cha 42 kinasema:-

"Waziri anaweza kwa kushirikiana na Tume kufanya marekebisho katika jaduweli yoyote katika sheria hii"

Sasa kama nilivyosema Mhe. Mwenyekiti, roho ya sheria hii ni majaduweli. Kwa hivyo, kumpa mamlaka waziri tu na tume bila ya kushirikisha chombo hiki cha Kutunga Sheria nadhani si sahihi na mapema pale nilipotoa hoja kama hii waziri alisema hana pingamizi na kwamba atakapofanya marekebisho ya jaduweli basi apate idhini ya chombo hiki na ni taratibu zinazotumika katika Jumuiya ya Madola Mhe. Mwenyekiti.

Ziko kanuni ambazo kurekebishwa kwake au hata kutungwa kwake hawachiwi waziri pake yake ziko anazoachiwa waziri peke yake ziko nyengine kwa uzito wake anaambiwa ashauriane na Kamati ya Sekta na ziko nyengine kwa unyeti wake anaambiwa ashirikishe Baraza zima au Bunge zima la Kutunga Sheria. Kwa hiyo, nilikuwa nasema hapa vile vile cha 42 tuweke kwamba afanye hivyo baada ya kupata idhini ya Baraza la Wawakishi ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa tunajaribu kuepuka ule urasimu mrefu tu pale tunapohisi kwamba kanuni inahitajika basi apewe mamlaka waziri kwa kushirikiana na taasisi ile aunde kanuni.

Lakini kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa uzito wa suala hili na Sheria yenyewe ya Maadili, mimi sioni tatizo lakini tatizo ni kwamba ule utaratibu uliopo ndio unachelewesha kidogo. Kwa hiyo, kama tunaridhia hiyo hakuna tatizo Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hiyo, tunakubaliana na hiyo haya.

Kifungu 42 Marekebisho pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 43

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 43 nina mswali mawili naomba nisaidiewe moja kwa sababu waziri alisema hawezi kuyajibu yote wakati alipokuwa akifanya majumuisho. Moja hapa pametajwa Naibu Mwenyekiti ambaye katika sheria nzima huku haonekani wala hakuna kifungu kinachosema kwamba ile Tume kwa maana ya Mwenyekiti na wale Makamishna wawili watachagua moja ya miongoni mwao kuwa Naibu Mwenyekiti.

Sasa Naibu Mwenyekiti kaibuka ghafla tu hapa, hatumjui katokea wapi. Nilikuwa naomba hilo nisaidiwe kama ni anatokea kule basi itajwe kule kwamba miongoni mwao.

Mhe. Mwenyekiti, basi na mimi napendekeza kwamba tusiweke. Hoja yangu ni kwamba nahofia kwamba wale Makamishna tumewanyanganya niliweka haja kule ya sifa ya 7(1b) ambayo imesema Mwenyekiti atakuwa na sifa za kuwa Jaji Mkuu sawa sawa na Jaji wa Mahakama Kuu. Sasa sifa hii tumeiondoa kwa wale makamishna wawili.

Kwa hiyo, kuja kuweka Naibu Mwenyekiti hapa hana sifa hii akaja sikiliza maswala kama haya ya kisheria kidogo inanikwaza. Kwa hiyo, hilo moja anipe ufafanuzi kuhusu Naibu Mwenyekiti.

Pili, ndilo linakuja suala ambalo hata mzee wetu analiliuliza jana kwamba inasema waziri ataweka utaratibu utakaowezesha Mwenyekiti na Naibu Mwenyekiti kutangaza mali zao. Naghofia hadhithi ya *I Screech yours Back and you You Screech mind* kwamba waziri mwenyewe ni sehemu ya watu ambao wanaweza kuchunguzwa na tume na nataka ifahamike hiyo Mhe. Mwenyekiti, simzungumzii Waziri Dr. Mwinyi haji Makame juzi alikuwa na wizara nyengine kabadilishwa kati kati kesho kutwa kuna uchaguzi anaweza akaja kuwa Makamu wa Pili wa Rais.

Kwa hiyo, nasema pengine akapanda cheo asiwe yeye akawa baada yake pale Mhe. Hija Hassan Hija. Sasa nasema tusitizame mtu katika kunga sheria. Kwa hiyo, hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ni kwamba huu utaratibu kwamba haukuwekwa ndani ya sheria kidogo mimi umemikwaza na nakubali kwamba na wao wanapaswa kuwa ni *subject* ya shughuli hizi. Lakini kwamba utaratibu wao utawekwa na waziri ambaye wewe mwenyewe baadae hatiame anaweza kuja kutwambia bwana wee mimi yako nayafunika na mimi yangu yafunike.

Ndio nikasema yake kwamba *You Screech my Back and I Screech yours* naogopa sana Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo naomba ufafanuzi Mhe. Mwenyekiti juu ya haya mawili la Naibu Mwenyekiti na hili la kukunana migongo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza pale tulirekesha labda Mhe. Ismail Jussa hakuipata. Tulisema kwamba hata mashahihisho ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati yetu alisahihisha pale, baada ya Naibu Mwenyekiti tumefuta tumesema Makamishna. Kwa hiyo, hata kwenye *Marginal note* isimoke kutangaza mali kwa Mwenyekiti na Makamishna sio Naibu Mwenyekiti, tume- *delete* ile haipo imeondoka.

La pili, nafikiri ki msingi tumekubaliana nae Mhe. Ismail Jussa ushauri wake kwamba utaratibu utaowekwa malalamiko yatamuhusu Mwenyekiti, tunahisi kwa mtizamo wetu yapelekwe kwa Mhe. Rais ndio muajiri wake moja kwa moja yeye ndiye aliyemteuwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu nukta ya pili kama yanapelekwa kwa Mhe. Rais angalau kwa udhoefu wake ni mkubwa nalikubali. Hilo moja nalikubali kwamba limeingia kwenye *Record* ya *Hansard*. Lakini kusema kweli katika waraka ambao tumegaiwa hapa nilijaribu kuangalia mimi sikuliona hilo la Mwenyekiti kama waliondoka. Kama katika hotuba yake inawezekana sikumsikiliza vizuri sitaki kusema lolote. Lakini katika waraka tuliogaiwa huu umeishia kwenye sehemu ya 7 na masharti menagineyo na umekuja mpaka kwenye kifungu cha 39 lakini haukufi kwenye kifungu cha 40.

Kwa hivyo, nasema huu nilionao mimi haukutaja hayo ya marekebisho ya kumuondosha mwenyekiti, lakini kwa sababu sasa amekwisha itamka imeshaingia ndani ya *Hansard* sasa marekesho ni Mwenyekiti na Makamishna sina pingamizi. Mhe. Mwenyekiti, nashukuru tuendelee.

Kifungu 43 Kutangaza mali kwa mwenyekiti na Naibu Mwenyekiti pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Mwenyekiti: Tuelewe tu kwamba marekebisho ya hapa tunaondoa Naibu Mwenyekiti tunaweka Makamishna sawa.

Kwa hiyo, marekebisho hayo ni pamoja na huu utaratibu ambao hapa utajwa utawekwa na waziri lakini sasa utawekwa na Rais.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: Mhe, Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa niwaombe wale wanaokubali mswada huu wa Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar ya Mwaka 2015.

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Zanzibar mwaka 2015 usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa niwaombe wale wanaokubali mswada huu ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Viongozi wa Umma na Kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi Ulisomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana muda unakaribia nadhani tuweke utaratibu wa muda kwanza kabla ya kuendelea.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, naomba nitoe hoja ya kuengeza muda ili tuweze kumaliza shughuli ambazo tunazo Mhe. Mwenyekiti. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanakubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wanyanyue mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Miswada Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kusomwa kwa mara ya kwanza Mswaada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Miradi ya Maridhiano namba Moja ya mwaka 1999 na kutunga sheria mpya kwa ajili ya kuanzishwa na kuendesha mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Binafsi na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mswada umesomwa kwa mara ya kwanza na kwa maana hiyo uko tayari kushughulikiwa na kamati inayohusika. Naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba Mswada wa Sheria wa Kuweka Masharti ya Usajili na Usimamizi wa Wathamini na Mambo Mengineyo Yanayohusiana na Hayo kusomwa kwa mara ya kwanza.

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Spika, vile vile kwa idhini yako naomba Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Kamishna wa Ardhi na Mambo

Mengineyo Yanayohusiana na Hayo kusomwa kwa mara ya kwanza.

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Spika: Ahsante sana Miswada yote hiyo miwili imesomwa kwa mara ya kwanza na kwa maana hiyo sasa ipo tayari kushughulikiwa na Kamati zinazohusika.

Mwisho nimkaribishe Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utali na Michezo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kusoma kwa mara ya kwanza Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Baraza la Sensa, Filamu na Utamaduni Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mswada huo pia umesomwa mara ya kwanza na upo tayari kufanyiwa kazi na Kamati.

Waheshimiwa Wajumbe kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mumeifanya katika Baraza hili. Lakini nichukue nafasi hasa hasa kuwashukuru Mhe. Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza ambao msimu huu wamefanya kazi kubwa sana wakati mimi nilikuwa kidogo napumzika nikiendelea na matibabu. Kazi nzuri imefanyika kwa mashirika makubwa, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe pamoja na viongozi hao waliokuwa wamechukua nafasi ya kuendesha mkutano huu wakati mimi nilikuwa nina dharura. *(Makofi)*.

Lakini pia niwashukuru watendaji wote Katibu pamoja na watendaji wengine na waandishi wa habari ambao wamekuwa pamoja na sisi kwa muda wote pamoja na watu wa televisheni kwa kazi nzuri sana iliyofanyika hadi kufikia tamati ya shughuli yetu ya leo. *(Makofi)*

Baada ya hayo basi machache sasa naomba nimkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, karibu. *(Makofi)*

KUAHIRISHA BARAZA

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uhai, uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii kukamilisha Mkutano wa 18 wa Baraza la Wawakilishi ambao umejadili masuala mbali mbali kwa mustakbali wa nchi yetu na watu wake. Aidha, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuijaalia nchi yetu kubaki katika hali ya amani na utulivu. Pia, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuendelea kuliendesha Baraza letu kwa umahiri na mafaniko makubwa. Uwezo wako, busara zako pamoja na hekima uliyonayo ndivyo vilivyouletea mkutano huu mafanikio hayo.

Mhe. Spika, natoa shukrani za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake wa busara na hekima ambao umechangia sana katika maendeleo tunayoendelea kuyapata katika nchi yetu. Mhe. Dkt. Shein ameendelea kuwa mfano bora wa uongozi makini ambao sote tunatakiwa kuiga mfano huo katika nafasi zetu mbali mbali ili tuweze kuiletea maendeleo ya haraka nchi yetu. Ndiyo maana amekuwa akisisitizia tuache kufanya kazi kwa mazoea *(business as usual)* ili tuweze kupiga hatua kubwa zaidi ya maendeleo nchini mwetu.*(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuendelea kumsaidia na kumshauri kwa hekima Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kwa mashirikiano yake mazuri kwa Ofisi yangu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri kwa kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizotolewa na wajumbe na kujibu maswali mbali mbali kwa umakini, ufasaha na usahihi. Ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu na wananchi waliokuwa wakifuatilia kwa karibu zaidi mijadala ya mkutano huu wamefaidika na majibu na ufafanuzi uliotolewa na Waheshimiwa Mawaziri.*(Makofi)*

Mhe. Spika, nawashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa umakini wao

wa kuhoji na kuuliza maswali na kupata majibu na ufafanuzi juu ya utendaji wa shughuli za Serikali. Vile vile, Waheshimiwa wamekuwa wakitoa maoni na maelekezo wakati wa kujadili Miswada inayowasilishwa hapa Barazani. Ni imani yangu kwamba, kufanya hivyo kutaimarisha utendaji wa Serikali na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, katika Mkutano huu wa 18, jumla ya maswali ya msingi 62 na maswali ya nyongeza 151 yaliulizwa na Waheshimiwa Wajumbe na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri. Aidha, jumla ya Miswada Minne (4) ya Sheria imewasilishwa na kujadiliwa kwa kina hatimae kupitishwa na Baraza lako tukufu, ambayo ni:

i. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo.
ii. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Ulinzi ya Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar na Mambo Yanayohusiana na hayo.
iii. Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu Nambari 2 ya mwaka 1996 na kuweka badala yake Masharti bora ya Kuhifadhi, Kulinda na Kusimamia Mazingira, Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo.
iv. Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi na Mambo Yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo, uliwasilishwa, kujadiliwa na hatimae kupitishwa katika Mkutano wa 18. Mswada huu ulikusudiwa kuweka sheria mpya inayoweka mfumo wa kisheria katika shughuli za kukabiliana na maafa na mambo ambayo yataondosha mapungufu yanayoonekana katika sheria ya sasa. Aidha, Sheria hii mpya itawiana na Sera ya Kukabiliana na Maafa ya 2011 pamoja na Makubaliano na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusiana na masuala ya kukabiliana na maafa iliyoridhiwa na nchi yetu.

Mhe. Spika, Serikali inawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote kwa michango na maoni yao na inawahakikishia kuwa michango na maoni yao yamepokelewa na kuzingatiwa ipasavyo ili kuwa na sheria bora itakayoweza kukidhi mahitaji ya wakati huu katika kukabiliana na maafa.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Ulinzi ya Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar na Mambo Yanayohusiana na Hayo. Mswada huu unapendekeza kuanzisha Shirika la Ulinzi ambalo litakuwa chini ya JKU. Shirika hilo linalopendekezwa litakuwa Wakala wa Serikali na litafanya kazi za ulinzi. Kwa ujumla michango, maoni pamoja na maelekezo ya Waheshimiwa Wajumbe yamepokelewa na kufanyiwa kazi katika kuboresha mswada huu.

Mhe. Spika, katika mkutano huu pia kuliwasilishwa na kusomwa kwa mara ya kwanza Mswada wa Sheria ya Kuhifadhi, Kulinda na Kusimamia Mazingira, Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mswada huu una lengo la kuondoa mapungufu yaliyopo katika utekelezaji wa Sheria ya sasa. Aidha, Sheria hii itazingatia Sera ya Mazingira ya Mwaka 2013, Mazingatio maalum ya Kimataifa juu ya Usimamizi wa Mabadiliko ya Tabianchi na uchimbaji wa mafuta na gesi pamoja na Haja ya kutenganisha shughuli za kiutekelezaji na uzingatiaji wa Sheria *(enforcement and compliance*) na zile za usimamizi (*governance*).

Mhe. Spika, Mswada mwengine uliowasilishwa na kujadiliwa ni Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi na Mambo Yanayohusiana na Hayo. Madhumuni na sababu ya Mswada huu ni kupendekeza kutungwa kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi. Baada ya kutungwa kwa Sheria ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, Serikali imeamua kuwasilisha Mswada huu ambao utasimamia maadili ya viongozi wote hapa Zanzibar kama walivyotajwa katika Sheria hii.

Mhe. Spika, sote tunaelewa kwamba kuwa na maadili kwa viongozi ni jambo la msingi katika uendeshaji wa shughuli za Serikali popote ulimwenguni. Kuwepo kwa Sheria hii kutaiongezea heshima nchi yetu kwa kuimarisha misingi ya utawala bora na uwajibikaji kwa viongozi wa Serikali yetu. Ninaamini utekelezaji wa sheria hii utaleta matumaini mapya kwa wananchi katika upatikanaji wa huduma zilizo bora kupitia taasisi mbali mbali za Serikali.

Mhe. Spika, Wajumbe wengi wa Baraza lako tukufu walikuwa na hofu na Mswada huu. Niwahakikishie Wajumbe wako kuwa hakuna haja ya kuwa na hofu na Mswada huu kwani hauna madhara yoyote kwao, mradi wamekuwa waadilifu, waaminifu na wanatunza heshima zao kama viongozi. Washike njia kuu, wasichepuke. Wakichepuka, sheria hii ndipo itakapo wabana.*(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa wito kwa viongozi wote kuisoma, kuifahamu na kuitekeleza ipasavyo Sheria hii ili iweze kuleta tija kwa jamii kama ilivyokusudiwa. Aidha, niwanasihi watendaji watakaopewa dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Sheria hii wawajibike ipasavyo katika kuhakikisha kuwa lengo na madhumuni ya kuanzishwa Sheria hii yanafikiwa.

Mhe. Spika, tarehe 12 Januari, 2015 nchi yetu ilitimiza miaka 51 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, jambo ambalo ni la kujivunia kwa Wazanzibari wote. Kama ilivyo kawaida, sherehe hizo zilitanguliwa na shamra shamra mbali mbali ikiwemo uzinduzi wa miradi 35 ya maendeleo. Wakati wa kilele cha maadhimisho ya sherehe hizo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein aliwahutubia wananchi na kuainisha maendeleo yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Saba.

Mhe. Spika, katika hotuba hiyo, Mhe. Rais alizungumzia maendeleo yaliyopatikana katika sekta zote zikiwemo Sekta ya Huduma za Jamii, Sekta ya Kiuchumi na Sekta za Uzalishaji. Katika Sekta ya Huduma za Jamii hasa elimu, Mhe. Rais alitangaza kufutwa kwa michango ya aina zote katika elimu ya msingi na ada za mitihani kwa elimu ya sekondari. Tamko hilo lina umuhimu mkubwa kwa jamii kwani litawawezesha wananchi wetu kuwa na uhakika wa kupata elimu kama ilivyoasisiwa na Jemedari wa Mapinduzi yetu Matukufu, Mzee Abeid Amani Karume, ya kutaka kila Mzanzibari awe na fursa ya kupata elimu.*(Makofi)*

Mhe. Spika, Sote Wazanzibari tuna kila sababu ya kumpongeza Mhe. Rais kwa uamuzi huu wa kizalendo unaoijengea sifa nchi yetu na kuongeza imani kwa wananchi wetu na kutoa fursa kwa watoto wetu hasa wanaotokana na familia zenye kipato kidogo kupata haki yao ya msingi ya elimu.*(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya Afya, Serikali inaendelea kusimamia na kuimarisha huduma za kinga na tiba katika hospitali na vituo mbali mbali vya afya Unguja na Pemba. Katika kuimarisha huduma za kinga Serikali imeendelea kuchukua juhudi za kukuza uelewa wa jamii juu ya kujikinga na maradhi mbali mbali. Aidha, Serikali imeyafanyia matengenezo makubwa na kujenga majengo mengine mapya ya hospitali zake pamoja na kuweka vifaa vya kisasa vya uchunguzi na tiba.

Vile vile, katika kuimarisha hospitali ya Mnazimmoja Serikali imejenga Wodi ya Wagonjwa Mahatuti (*ICU*) ya kisasa na Kitengo cha Huduma za Upasuaji wa Vichwa na Uti wa Mgongo *(Neurosurgical Unit)* na kuwekewa vifaa vyote muhimu na tayari vinafanya kazi ya kutoa huduma zilizokusudiwa. Napenda kuwashukuru sana wahisani wetu katika maendeleo kwa msaada wao mkubwa waliotupatia katika kuimarisha huduma hii muhimu ya afya.*(Makofi)*

Mhe. Spika, sambamba na hayo, Serikali imechukua jitihada maalum za kuongeza madaktari na wahudumu wengine wa afya ili kukidhi mahitaji ya kitabibu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hivi sasa jumla ya Madaktari Bingwa kumi na mbili (12) wa fani mbali mbali wako masomoni na miezi michache iliyopita tumeshuhudia madaktari 37 wa Chuo cha Udaktari Zanzibar (*Zanzibar Medical School)* kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha *Matanzas* cha Cuba wakihitimu masomo yao ya Shahada ya kwanza na tayari wameshaanza kufanya kazi.

Pia tutaendelea kushirikiana na nchi marafiki katika kutupatia madaktari bingwa wa maradhi mbali mbali pamoja na kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa madaktari wetu. Hivi sasa tunao madaktari wapatao 40 kutoka Jamhuri ya Watu wa China na Cuba ambao wanaendelea kutoa huduma katika Hospitali zetu. Napenda kuzishukuru nchi za China na Cuba kwa misaada yao hiyo.*(Makofi)*

Mhe. Spika, suala la udhalilishaji wa kijinsia bado ni changamoto katika nchi yetu, kwani pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa za kudhibiti vitendo hivyo viovu bado wapo watu miongoni mwetu wanaoendeleza vitendo hivyo. Ni wajibu wa kila mmoja wetu kuzidisha mapambano dhidi ya waovu hao. Watu hawa wamo miongoni mwetu na tunaishi nao. Viongozi na wananchi kwa pamoja tuwafichue na kuwafikisha katika vyombo vya sheria bila ya

kuoneana muhali kwani watu hao wanavunja utu na heshima ya wenzao na kuwasababishia madhara makubwa kimwili na kisaikolojia. Aidha, natoa wito kwa wale wote wenye taarifa kutosita kufika Mahakamani kutoa ushahidi pale wanapohitajika na kuacha kabisa suala la kumaliza kesi hizi majumbani.

Mhe. Spika, sekta ya kilimo bado ni tegemeo la wananchi wengi katika kujipatia ajira, kipato, chakula na kuimarisha lishe na afya zao. Kwa kuelewa hali hii, Serikali inaendelea kutoa msukumo mkubwa kuisaidia sekta hii na kuwasaidia wakulima ili waweze kuongeza tija na uzalishaji na hivyo kuimarisha vipato vyao. Kilimo cha mpunga katika msimu huu wa 2014/2015 kimeanza na kinaendelea vyema. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili imejiandaa kikamilifu kuhakikisha kwamba huduma za kilimo cha matrekta na pembejeo nyengine zinapatikana kwa uhakika na kwa bei nafuu ambazo wakulima watazimudu. Aidha, Serikali imeongeza kiwango cha upatikanaji wa mbegu bora ya mpunga, dawa ya magugu na mbolea kupitia Program ya Ruzuku Katika Kilimo cha Mpunga.

Mhe. Spika, natoa wito kwa wakulima wote wa zao la mpunga nchini kuungana na juhudi hizi za serikali kutumia fursa ziliopo kuhakikisha wanalima kwa wakati na kufuata kanuni zote za kilimo bora, ikiwemo matumizi ya mbegu bora, matumizi sahihi ya mbolea na kuhudumia mashamba yao kwa kufanya palizi za mapema ili azma ya serikali ya kuongeza uzalishaji wa zao hili iweze kufikiwa. Sambamba na hili, serikali inawahimiza wakulima wote wa mazao mengine kuchukua juhudi stahiki kwa kufuata ushauri wa Mabibi na Mabwana Shamba ili nao waweze kuongeza uzalishaji wa mazao yao.

Mhe. Spika, Sekta ya Utalii imeendelea kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Takwimu zinaonyesha kwamba mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa umefikia zaidi ya asilimia 27. Sekta hii vile vile imechangia kwa kiasi kikubwa katika utoaji wa ajira ambapo hadi mwishoni mwa mwaka uliopita wa 2014 ilichangia kutoa ajira zisizokuwa za moja kwa moja zipatazo 60,000 na za moja kwa moja 22,884. Kutokana na mchango wa sekta hii katika maendeleo yetu, serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri ya kitaasisi na kiuendeshaji ili kukidhi viwango vya kimataifa katika utoaji wa huduma za kitalii. Hii ikiwa ni pamoja na kuimarisha mashirikiano baina ya serikali na sekta binafsi zinazohudumia watalii.

Mhe. Spika, ili sekta hii izidi kukuwa na kuleta tija katika nchi yetu hatuna budi sote kwa pamoja Taasisi za Serikali, sekta binafsi na wananchi kuzidi kushirikiana katika kuimarisha vivutio pamoja na miundombinu itakayowavutia watalii, ikiwemo usafi na utunzaji wa mazingira, uwekezaji katika ujenzi wa hoteli zenye viwango bora na kudumisha amani na utulivu katika nchi yetu na kuhakikisha kwamba mapato yanayotokana na sekta hii yanakusanywa kikamilifu na kuingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, katika kuendeleza dhana ya utalii kwa wote, serikali itazidi kuhamasisha wananchi kuzalisha bidhaa bora na zenye viwango zitakazoweza kuingia katika soko la utalii na hivyo kuifanya sekta hii kuzidi kuwanufaisha wananchi. Hivi sasa wananchi wengi wamepata fursa ya kuuza bidhaa zao kwenye hoteli kadha, hali ambayo imeongeza upatikanaji wa soko la bidhaa wanazozalisha wananchi. Kwa azma hiyo hiyo ya kuongeza ushiriki wa wananchi katika sekta ya utalii, serikali imefanya utafiti wa kuibua vivutio vipya vya utalii vilivyopo katika maeneo ya vijijini. Matokeo ya utafiti huo yatasambazwa kwa wananchi ili kuongeza uelewa wa fursa za sekta ya utalii zilizopo katika maeneo yao. Utekelezaji wa mpango huu unakadiriwa kutoa ajira za moja kwa moja zaidi kwa wananchi hasa wa vijijini. Aidha, sekta zinazohusika zinaagizwa kuandaa na kutekeleza mipango itakayoamsha ari ya wananchi kupenda kutembelea maeneo yenye vivutio vya utalii, ili kukuza utalii wa ndani.

Hata hivyo, kuiimarisha sekta hii hatuna budi sote kuwa wadau wa kudumisha amani na utulivu nchini. Bila ya amani na utulivu hakuna mtalii atakayekuja nchini mwetu kwani atahofia usalama wake.

Mhe. Spika, Sekta ya Miundombinu ya Usafirishaji ni muhimu sana katika ustawi wa nchi yetu. Kwa hapa kwetu miundombinu hiyo inajumuisha barabara, bandari na viwanja vya ndege. Serikali inaendelea kuwekeza fedha nyingi katika sekta hii ili kuhakikisha wananchi na hata wageni wanapata huduma bora za usafiri na usafirishaji wa bidhaa zao kutoka eneo moja hadi jengine. Kama sote tulivyoshuhudia katika kuadhimisha miaka 51 ya Mapinduzi matukufu miradi mbali mbali ya miundombuni ilizinduliwa, ikiwemo barabara za mjini na vijijini, uimarishaji wa viwanja vya ndege na kuimarisha huduma za usafiri wa baharini. Haya yote yanafanyika katika kuendeleza azma ya Serikali ya kuimarisha uchumi na kupunguza umasikini. Serikali itaendelea na hatua za kuimarisha miundombinu ya usafiri Unguja na Pemba kadri hali yetu ya uchumi itakavyoruhusu.

Mhe. Spika, suala la utoaji wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi limekuwa na mjadala mkubwa ndani ya Baraza lako tukufu, kwani kuna baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi wamekuwa wakilalamika juu ya baadhi ya wananchi wao kutokupatiwa vitambulisho hivyo kwa sababu mbali mbali. Naomba ieleweke kuwa, Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi vinatolewa kwa mujibu wa sheria Na. 7 ya mwaka 2005. Hivyo, mlengwa ni lazima atimize matakwa ya sheria hiyo kabla ya kupatiwa vitambulisho. Matakwa hayo ni pamoja na kuwa Mzanzibari wa kuzaliwa au, mwananchi kukaa katika eneo lake si chini ya miezi 36 mfululizo na ambae ametimiza umri wa miaka 18.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 13 (1) (2) cha Sheria hiyo kimetoa haki kwa mtu yeyote, kukata rufaa kwa Mkurugenzi wa Vitambulisho dhidi ya Afisi ya Usajili, na pindipo hakuridhika na uamuzi wa Mkurugenzi anaweza akakata rufaa kwa Mheshimiwa Waziri. Bado kama hajaridhika anaweza kukata rufaa Mahakama Kuu.

Mhe. Spika, ni imani yangu kuwa Waheshimiwa Wawakilishi na Wanasiasa na wananchi, hatuna sababu ya kulalamikia, jambo ambalo lina utaratibu mzuri wa kisheria. Suala zima la upatikanaji wa vitambulisho tusilihusishe na siasa, kwani suala hili lina utaratibu wake wa kisheria. Ni wajibu wetu kutumia sheria hiyo katika kutafuta haki zetu.

Mhe. Spika, kama mnavyofahamu hivi karibuni nchi yetu imekamilisha zoezi la kupata Katiba Inayopendekezwa. Kwa mara nyengine tena napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuanzisha na kusimamia kwa umakini mkubwa mchakato mzima wa mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi kufikia kupata Katiba Inayopendekezwa. *(Makofi)*

Aidha, nawapongeza kwa dhati kabisa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wote wa Bunge Maalum la Katiba, kwa ushiriki wao na kazi kubwa waliyofanya iliyopelekea kumalizika kwa zoezi hilo kwa mafanikio makubwa. Ni wajibu wa Viongozi na wananchi sote kuisoma na kuielewa Katiba hiyo, ili hatimae tuweze kushiriki kikamilifu katika hatua ya kuipigia kura ya maoni Katiba hiyo inayopendekezwa wakati utakapofika hapo tarehe 30 Aprili, 2015.

Nawasihi wananchi wote na kwa kila anaepaswa na mwenye haki ya kupiga kura hiyo ni wajibu wake kwenda kupiga kura. Utaratibu maalum utapangwa ili kila mmoja atumie haki na fursa hiyo bila bughudha. Natoa wito kwenu tuitumie fursa hiyo bila ya mikwaruzano, ili kulimaliza zoezi hilo la kihistoria kwa utulivu mkubwa na maelewano. Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba kukushukuru kwa dhati kabisa wewe binafsi kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuliendesha Baraza letu kwa umakini mkubwa. Vile vile, nawashukuru Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu kwa kutekeleza majukumu yao vyema. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, kwa ushiriki wao mzuri katika mkutano huu wa 18 ambao umemalizika salama na kwa mafanikio makubwa. Nawashukuru watendaji wote wa serikali, wakiongozwa na Makatibu Wakuu kwa juhudi zao za kuliwezesha Baraza kuendesha shughuli zake. *(Makofi)*

Namshukuru pia Katibu wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wote wa Baraza hili, kama kawaida yao kwa maandalizi mazuri ya Mkutano huu. Nawashukuru Wanahabari wote na Wakalimani wa alama kwa kazi nzuri wanazozifanya za kuwaelewesha wananchi yanayotokea katika Baraza hili. Nawatakia wajumbe wote kurudi katika sehemu zetu za kazi kwa salama na amani na pia turejee majimboni mwetu kwenda kuendelea kushirikiana na wananchi katika kuwaletea maendeleo na kuiletea maendeleo nchi yetu. Mwisho nawatakia heri na baraka za mwaka mpya wa 2015. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa heshima naomba kutoa hoja ya kuliahirisha Baraza lako tukufu hadi siku ya Jumatano tarehe 11 Machi, 2015 saa 3.00 barabara za asubuhi. *(Makogi)*

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, tunakushukuru sana na nichukuwe nafasi hii kwa niaba ya Waheshimiwa Wajumbe wote, kukushukuru sana kwa hotuba hiyo ya kutufungia Mkutano wetu huu wa 18, ambapo umetuelezea kwa kifupi mambo ambayo tumeyafanya katika Mkutano huu.

Nirudie tena kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa mashirikiano makubwa tuliyotoa, tukahakikisha kwamba shughuli ambazo zilipangwa katika Mkutano huu kumalizika vizuri na kwa ufanisi mkubwa. Yote hayo yamekuja kutokana na ushirikiano wa dhati ambao tumekuwa nao kama kawaida katika shughuli zetu za Baraza.

Kwa hivyo, nawashukuru wote kwa mashirikiano hayo na napenda basi niseme kwamba shughuli zetu hizi zimefanikiwa vya kutosha. Waheshimiwa Wajumbe kabla sijawahoji kuhusu hoja iliyotolewa hapa ya kuahirisha Mkutano huu, naomba nitowe tangazo moja dogo.

Waheshimiwa Wajumbe, mara baada ya kuahirisha Mkutano huu tunatangaziwa na Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi, kwamba Wajumbe wa Upande wa Chama cha Mapinduzi wakutane hapo juu kwenye ukumbi wa juu hapo kuna mambo kidogo ya kuelezana. Kwa hivyo, mara tu tukitoka humu ndani wajumbe wale wa upande wa Chama cha Mapinduzi wanaombwa wakutane hapo kwenye ukumbi wa juu.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kuahirisha Mkutano huu wa 18 hadi 11 Machi, 2015 saa 3:00 za asubuhi, wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Sasa nichukuwe nafasi hii kuahirisha Mkutano huu hadi tarehe 11/03/2015 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Wimbo wa Taifa)